**28 JUNI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Hamsini na Sita – Tarehe 28 Juni, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 716

**Fursa za Ajira kwa Vijana**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza fursa za ajira kwa vijana kwa mfumo wa pamoja kati ya Serikali na wadau wengine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mipango mbalimbali ya kutengeneza fursa za ajira kwa vijana kwa kushirikiana na wadau wengine kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuwezesha vijana kupata mafunzo kupitia Programu ya Taifa ya Ukuzaji Ujuzi ili kuwezesha vijana kupata ujuzi utakaowawezesha kujiajiri au kuajiriwa;

(ii) Kufanya mabadiliko ya sera mbalimbali ili kuweka mazingira wezeshi ya kuongeza uwekezaji katika sekta zinazozalisha fursa nyingi za ajira; na

(iii) Kupunguza au kuondoa kodi na tozo mbalimbali ili kuwezesha wawekezaji wanaotengeneza fursa nyingi za ajira kwa nguvu kazi nchini kuweza kuajiri zaidi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nilikuwa na maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kufuatia vijana wengi kumaliza vyuo na vyuo vikuu na kukosa ajira, sasa ni upi mpango wa Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, kuwasaidia mitaji vijana hawa ili waweze kujiajiri na kuwa wajasiriamali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, ni upi mpango wa Serikali kuwapa kipaumbele vijana wanaojitolea katika ofisi mbalimbali za umma pindi ajira zinapotangazwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Janeth, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, katika utaratibu aliosema wa kuwapa mikopo na kuwasaidia vijana, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa na programu na uratibu wa kazi mbalimbali zinazowasaidia vijana ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa sera na sheria.

Mheshimiwa Spika, moja ya utaratibu ambao unatumika katika kutoa mikopo kwa vijana ambao wanamaliza vyuo vikuu na makundi yote kwa ujumla ni ule utaratibu wa *four, four, two* kwa maana ya asilimia nne kwa wanawake, asilimia nne kwa vijana na asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu katika halmashauri zetu zote nchini katika fedha ghafi. Kwa hiyo, zinatengwa 10% ya fedha zile za halmashauri kwenye mapato ya ndani ili kuweza kuwawezesha hao vijana.

Mheshimiwa Spika, pili, kumekuwa na utaratibu ambao ni maagizo mahususi ya Mheshimiwa Rais na utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba katika kila Wizara za Kisekta, ziweze kutenga fedha kwa ajili ya kusaidia vijana kuajiri na kuajiriwa moja ya mambo ambayo yamefanyika ipo Wizara ya Kilimo, tunayo Programu ya *Building Better Tomorrow*, Wizara ya Nishati tuna programu ambayo inawawezesha vijana hivyo hivyo na mikopo ya *Mining for Better Tomorrow,* lakini pia tunayo programu nyingine katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya *BBT Life* ambayo inawasadia kushughulika na suala la uchumi wa buluu.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu, kupitia Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, hivi karibuni amezindua

utaratibu ambao tutaenda kuutekeleza wa kutengeneza *incubation centers* katika maeneo mbalimbali kikanda au kimikoa kulingana na upatikanaji wa fedha ili kuwatambua vijana kwenye hayo maeneo, lakini pili kuwasajili na kuwasaidia kupata *start up capital* ya kuanza mitaji ikiwa ni biashara au ni masuala ya kiteknolojia kuweza kuwasadia zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali kupitia Sheria ya Manunuzi ya Umma katika 30% ya *tender* zitakuwa zinaenda kwa ajili ya vijana na kwa mwaka wa jana wa fedha zaidi ya shilingi bilioni 300 *tender* hizo zilikuwa kwa ajili ya kuwapa vijana ambao wamefungua makampuni na kuweza kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, swali la pili...

**SPIKA:** Kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, swali la pili, tunao utaratibu kupitia Wakala Ajira *(TAESA)* wa kuweza kuratibu vijana ambao wanamaliza vyuo vikuu kuwatambua, kuwapa *training* na kuwafikisha kwenye maeneo ya kazi na tumeshafanya hivyo kwa vijana zaidi ya 20,334 ambao wamekutanishwa na waajiri na kwenda kufanya mazoezi ya uzoefu kazini ili baadaye kama wakipata fursa za ajira zinavyotolewa na Serikali waweze kuajiriwa, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 717

**Fedha za Makusanyo Kubaki kwenye Halmashauri**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kubakiza 40% ya fedha zinazokusanywa kwenye halmashauri kwani hali ya kifedha kwa halmashauri nyingi sio nzuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura 290, halmashauri zina mamlaka kisheria ya kupanga, kukusanya na kutumia mapato yake. Hivyo, mapato yote yanayokusanywa na halmashauri zote nchini hubaki na kutumika kwenye halmashauri husika kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Aidha, halmashauri zote nchini zimeelekezwa kutenga kati ya 20% hadi 70% ya mapato kulingana na uwezo wa makusanyo wa halmashauri husika kwa ajili ya kuchangia kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato yanayowasilishwa Serikali Kuu ikiwemo kodi ya majengo, kufuatia marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura 290, kuanzia mwezi Januari, 2024 halmashauri zote zimerejeshewa kukusanya chanzo cha kodi ya majengo kama wakala kwa kurejeshewa 20% ya makusanyo yote.

Mheshimiwa Spika, ikiwa kuna uhitaji wa ongezeko la kutoka 20% hadi 40% suala hili linahitaji maoni ya wadau ili kutathmini athari zinazoweza kutokea kabla ya mabadiliko haya kufanyiwa kazi na Serikali, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru Serikali kwa hatua nzuri ya kurejesha angalau 20% ya mapato ya majengo na kwa kuwa sasa majukumu mengi yapo kule chini, ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, shule, hauoni sasa

tukiongeza mpaka 40% itakuwa rahisi kwao kutekeleza miradi ya kimaendeleo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza, fedha ambazo zinatumika kujenga vituo vya huduma za afya, zahanati na hospitali, lakini pia na miundombinu mingine katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatokana na vyanzo vikuu viwili; vyanzo vya mapato ya ndani ya halmashauri zenyewe lakini pia fedha kutoka Serikali Kuu. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zote ni za Serikali hata kama zitaletwa Serikali Kuu, lakini bado kuna fedha nyingi sana zinatoka Serikali kuu kwenda kujenga vituo hivyo katika halmashauri hizo hizo. Kwa hiyo, tutaendelea kuboresha upatikanaji wa fedha ili tuweze kuboresha ujenzi wa miundombinu mbalimbali, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa swali linalofuata ni la kwako au ni la Naibu mwingine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, la kwangu.

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, sasa ulize swali lake na kwa niaba yake, Mheshimiwa Rashid Shangazi.

Na. 718

**Kuigawa Kata ya Kivavi – Makambako**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaigawa Kata ya Kivavi – Makambako?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikizingatia suala la uanzishaji wa kata kwa mujibu wa kifungu cha 16(1) hadi (3) cha Sheria za Serikali za Mitaa, Sura 288 ili kuchochea ukuaji wa shughuli za maendeleo. Katika mfumo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi sasa kuna jumla ya kata 3,956 katika halmashauri 184.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kugawa na kuanzisha kata uko kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura 288 ambapo vikao huanzia ngazi ya vijiji, Baraza la Madiwani, *DCC* na *RCC* kisha kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Ni vema hatua hizo zifuatwe, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, lakini mwaka 2016 wakati wa kuhitimisha mjadala wa Bunge Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa tamko la kusitisha kuanzisha mamlaka mpya za kiutawala.

Je, ni kwa kiasi gani tangazo lile sasa lifike mwisho ili mamlaka mpya za utawala ziweze kutangazwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa zipo baadhi ya kata na halmashauri zimegawanywa, lakini mgawanyo huu hauna usawa. Yapo baadhi ya maeneo unakuta Jimbo A lina kata 20 lakini Jimbo B lina kata nane na hii haileti ulinganifu.

Je, Serikali ipo tayari kufanya *restructuring* ya huo mgawanyo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika,

kwanza kuhusiana na tamko la kutoendelea na ugawaji wa mamlaka mpya, mpaka sasa Serikali inaendelea kupokea maoni ya wadau katika halmashauri zetu maeneo ambayo yanapendekezwa kwa ajili ya kugawa mipaka au kugawa maeneo mengine ya utawala.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kwa sasa tumeweka katika kukamilisha kwanza miundombinu katika maeneo hayo ya utawala yaliyopo, kwa sababu bado kuna upungufu mkubwa sana wa miundombinu kama Ofisi za Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi, Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji, bado tuna changamoto kubwa ya upungufu wa miundombinu hiyo.

Kwa hiyo, lengo la Serikali nikuona kwamba kwanza tunaboresha miundombinu katika mamlaka zilizopo, lakini baadaye tutakwenda kupitia mapendekezo kutoka kwenye halmashauri na mitaa kwa ajili ya kubadilisha mipaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli kumekuwa na mgao wa maeneo ya kiutawala, lakini maeneo mengine ni makubwa maeneo mengine ni madogo na sisi kama Serikali tupo tayari kupokea maoni ya wadau kutoka maeneo hayo ili Serikali ione uwezekano wa kuyafanyia kazi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kata ya Songoro ina kata mbili za kichama ambazo ni kubwa sana, je, Serikali haioni kwamba ni wakati mwafaka sasa kuigawa hiyo kata tuwe na kata za Serikali mbili, yaani Songoro na Nshing'a? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri wa Arumeru kuanza utaratibu kwa mujibu wa Sheria ya 288 ya kugawa maeneo ya

utawala ili vikao husika viweze kuidhinisha na baadaye Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa awasilishe Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya hatua zaidi kwa kadri ambavyo itaonekana inafaa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, mwaka jana Serikali ilitoa maelekezo kwenye majimbo yetu. Kwa hiyo, watu walipendekeza kata, vijiji, vitongoji na mamlaka za miji ili yagawiwe na mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, je, katika maeneo yale ambayo tulipendekeza nini sasa kauli ya Serikali kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo tayari halmashauri zimependekeza kwa ajili ya kugawa na kupata maeneo mapya ya utawala, Serikali itaendelea kuyafanyia kazi kwa kadiri ambavyo itaoneka inawezekana, lakini hata kama maeneo hayo hayatapata idhini ya mgao kwa mwaka huu ambao tunaelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, bado Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaweza kufanyika kwa kufuata mipaka ile ile ya siku za nyuma wakati utaratibu unaendelea.

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imepokea maombi hayo na inaendelea kuyafanyia kazi, lakini hii haitaathiri Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wala Uchaguzi Mkuu ujao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 719

**Fedha kwa Ajili ya Kutengeneza Barabara za Kata – Kishapu**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha Jimbo la Kishapu kupitia Mfuko wa *TARURA* kwa ajili ya barabara zenye urefu wa kilometa 522 ambazo zipo katika hali mbaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya mtandao mzima wa barabara katika Wilaya ya Kishapu na kubaini ukubwa wa uharibifu ambapo shilingi bilioni 2.5 zinahitajika ili kuzifanyia matengenezo.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imekwishapeleka shilingi 190,000,000 kwa *TARURA* Wilaya ya Kishapu kwa ajili ya kuanza kufanya matengenezo ya dharura kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kulipa uzito suala hili na matengenezo yataendelea kufanyika kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini na jitihada ya kurudishia miundombinu kwa hizo fedha kiasi cha shilingi milioni 190 ambazo zimeanza matengenezo.

Mheshimiwa Spika, upo uharibifu mkubwa sana wa Daraja la Itilima - Manonga ambalo linaunganisha kata tatu. Barabara ya

Bulekela - Mwajidalala- Miandualwa – Ukenyenge - Negezi - Mwadui Lohumbo - Nhobora - Muguda barabara hizi zimeharibika sana na kata sita sasa hazina mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isichukue hatua za haraka za dharura ilimradi kuleta fedha za kutosha ili barabara na miundombinu iweze kurudishiwa haraka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri upo tayari kuambatana na mimi baada ya Bunge hili ili ukajionee wewe mwenyewe hali halisi ya uharibifu wa barabara kutokana na mvua kubwa zilizonyesha katika kipindi hiki? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa ya kuwasemea wananchi wake na hasa katika kuhakikisha wanapata miundombinu iliyo bora ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza, sisi tunafahamu kwamba mvua zilizonyesha kati ya kipindi cha Novemba, 2023 mpaka Aprili, 2024 zimeleta uharaibifu mkubwa sana wa miundombinu na Serikali inatambua uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara iliyotekea katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeshatenga shilingi milioni 19 kwa ajili ya kufanya marekebisho ya eneo la kujenga makalavati manne, kuchimba mtaro meta 700, kukarabati Daraja la Bulimba, lakini Serikali imeshatenga shilingi milioni 30 kwa ajili ya kurekebisha Barabara ya Negezi - Mwadui Lohumbo ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imetenga shilingi milioni 24.7 kwa ajili kurekebisha barabara ya Nhobora - Muguda na Serikali imetenga shilingi milioni 38.4 kwa ajili ya kurekebisha barabara ya

Itilima - Manonga ambayo pia Mheshimiwa Mbunge ameitaja. Kwa sasa wakandarasi wapo *site* na wanaendelea na kurekebisha barabara hizi.

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili kuhudumia barabara katika jimbo lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, kwamba kama mimi nipo tayari kuambatana na yeye kwenda kujionea uharibifu uliotokea, nikuhakikishe Mheshimiwa Mbunge tutakaa, tutajadili na tutakubaliana, hivyo nipo tayari kuja katika jimbo lako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam, mmesimama wawili mwenye majibu ya swali hili. Haya Mheshimiwa Issa Mtemvu kwa niaba ya Mheshimiwa Mariam Kisangi. *(Makofi)*

Na. 720

**Ukarabati wa Shule Kongwe - Dar es Salaam**

**MHE. ISSA J. MTEMVU K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia ukarabati shule kongwe za msingi katika Mkoa wa Dar es Salaam ambazo ziko katika hali mbaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uchakavu uliopo kwenye shule za msingi nchini na inaendelea kufanya jitihada za

kutatua changamoto hiyo. Katika mwaka 2023/2024 kupitia Mradi wa *BOOST,* Serikali imetoa shilingi bilioni 2.6 kwa ajili ya ukarabati wa shule za msingi chakavu 26 za Mkoa wa Dar es Salaam na ambapo ukarabati unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa fedha za ukarabati wa shule za msingi nchini kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa ni kweli fedha zimepelekwa kwenye shule takribani 26 katika Jiji la Dar es Salaam, lakini shule ya kongwe ya Rangi Tatu na ya *Mbagala Annex* zina hali mbaya sana. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati kwa haraka?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, shule nyingi za msingi kwenye Jimbo la Kibamba zina changamoto hiyo ya uhitaji wa ukarabati wa majengo yake hasa Shule za Kibesa, King'ong'o, Mshikamano na Luguruni. Je, ni lini Serikali mtapeleka fedha kwenye shule hizi ili kusaidia kupunguza msongamono wa wanafunzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mazuri na kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi Serikali tayari imeshaanza kutoa fedha na imeleta fedha kwa ajili ya ukarabati katika shule katika Mkoa wa Dar es Salaam. Pia Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imetenga fedha tena kwa ajili ya ukarabati wa shule zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuhakikishe Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kuleta fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu ili wanafunzi wetu waweze kusoma katika miundombinu iliyo bora. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kwamba mmeleta fedha hizi Mkoa wa Dar es Salaam, lakini Jimbo la Temeke ni jimbo ambalo lina shule nyingi zaidi kongwe. Je, Serikali hamuoni muweke mkakati maalumu hasa kwa ajili ya shule hizi kongwe za Jimbo la Temeke? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Temeke katika mwaka huu na lenyewe limepelekewa fedha kwa ajili ya marekebisho katika shule sita ambazo ni Shule ya Chamazi, Mbagala Kuu, Mzinga na Toangoma Bukarani na Sandari. Kwa hiyo, kwa sababu tayari Serikali imeshaanza kuleta fedha kwa hiyo itaendelea kuhakikisha inaendelea kuleta fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule hizi katika jimbo lako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Shule za Msingi za Kitengule na Namula ni kama hamna kabisa kwa sababu madarasa yote yapo chini. Sasa nauliza, ni lini Serikali itasaidia ujenzi upya wa shule hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imetenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa shule zetu hizi za msingi. Nimhakikishe Mheshimiwa

Mbunge tutamtazama kwa jicho la kipekee kabisa kwa kuzingatia mazingira ya shule zilizopo katika jimbo lake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ulisimama wewe mwanzo au jirani yako? Wewe ndiyo ulisimama? Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa spika, nashukuru, kwa kweli changamoto ni kubwa sana kwa shule kongwe.

Mheshimiwa Spika, ninataka kujua ni lini Serikali itakarabati Shule ya Msingi Mkombozi iliyopo katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma hasa ukizingatia ni shule ya muda mrefu na imechakaa sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Serikali imetenga fedha mahususi kabisa kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaitazama shule hii ya Mkombozi ili na yenyewe iweze kupatiwa fedha kwa ajili ya ukarabati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mvua za *El-Nino* na kimbunga Hidaya zimeleta uharibifu wenye thamani ya shilingi milioni 457 katika Wilaya ya Kilwa, je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati miundombinu hiyo iliyoharibiwa na mvua hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, bila shaka miundombinu hiyo anayoizungumzia ni ya shule. Serikali tayari imeshafanya tathmini kubaini uharibifu uliotokea kutokana na mvua kwenye miundombinu ya shule na Serikali itahakikisha

inaleta fedha kwa ajili ya kuhakikisha inarudisha au inarekebisha miundombinu ambayo imeharibika kutokana na mvua na hasa miundombinu ya shule zetu hizi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, Shule za Dung'unyi na Kinyang'wanjo katika Jimbo la Singida Mashariki ni shule kongwe na zimechakaa sana. Ni lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya kuzikarabati shule hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa imekuwa ikifanya ukarabati wa miundombinu chakavu katika shule zetu hizi za msingi na tayari imeanza kuhudumia maeneo mbalimbali ya nchi.

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wewe katika jimbo lako kwa sababu kuna shule hizi chakavu na Serikali inatambua, fedha italetwa kwa ajili ya kuhakikisha miundombinu inaboreshwa na shule zako zinakarabatiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mbunge wa Ilemela, sasa aulize swali lake.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa Serikali itoe majibu ya swali langu.

**SPIKA:** Swali lako ni namba 721.

Na. 721

**Miundombinu ya Kukaushia Samaki na Dagaa kwenye Mialo Ziwa Victoria**

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaweka miundombinu rafiki ya kukaushia samaki na dagaa kwenye mialo ya Ziwa Victoria – Mwanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mbunge wa Ilemela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali itaanza utaratibu wa kuweka miundombinu ya kukaushia samaki na dagaa ya mahema yaani *solar tents* na vichanja katika mwalo wa *New Igombe* uliopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Mkoani Mwanza.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali kwa kushirikiana na *Lake Victoria Fisheries Organization* yaani *LVFO* inatarajia kuweka mahema na vichanja katika mialo ya Chinfumfu (Kijiweni) katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema na Kasalazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa, Mkoani Mwanza ambapo wadau watakaohusika na miundombinu hiyo ni Vikundi vya Ulinzi Shrikishi yaani *BMUs* na wameshapatiwa mafunzo ya kuongeza thamani kwenye zao hilo la dagaa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza, niishukuru Serikali kwa majibu mazuri ambayo

yanaleta matumaini kwa wavuvi wa Ilemela na Kanda ya Ziwa kwa ujumla na nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na wafanyabiashara wa samaki wanaokuja kutoka nchi za nje badala ya kutumia masoko ambayo yameandaliwa na Serikali kwa ajili ya kununua mazao ya samaki, wanaenda moja kwa moja visiwani kununua samaki na kuwafanya wale wafanyabiashara wa maeneo hayo waweze kukosa bidhaa hiyo na wanapitiliza bila kulipa ushuru wa Serikali kama inavyotakiwa.

Je, Serikali ina mpango gani katika kuzuia wavuvi hawa wasiende visiwani bali watumie masoko yaliyoandaliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tunaishukuru sana Serikali imewawezesha wavuvi kwa kuwapa vifaa vya uvuvi katika Ziwa Victoria na Bahari ya Hindi pia, lakini changamoto iliyopo katika Ziwa Victoria baadhi ya vifaa walivyopewa na wamepewa kwa mkopo havifadhilii uvuvi ndani ya Ziwa Victoria inaonekana jinsi vilivyotengenezwa vinafaa katika maji marefu kwa maana ya bahari.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuwasaidia wavuvi hawa waweze kupata vifaa vinavyoendana sambamba na Ziwa Victoria ili waweze kulipa pia mikopo yao kwa sababu sasa hivi hawafanyi biashara wamevi-*park*? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nashukuru kwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Angeline Lubala Mabula, nitayajibu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru sana kwa maswali haya makini kabisa kutoka kwake yanayowakilisha wavuvi mbalimbali, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni hili la wafanyabiashara wageni. Kwa mujibu wa sheria yetu ipo wazi, wafanyabiashara wageni tumekwisha kuwatengea masoko yale ya kimataifa ikiwemo soko la Kirumba pale Mwanza. Kwa hiyo, ni maelekezo yetu sasa Serikali, kuhakikisha kwamba wenzetu waliopo katika wilaya na mikoa ambapo wana wataalamu, Kamati za Ulinzi na Usalama zina Maafisa wa Uhamiaji wenye uwezo wa kuwatambua wale wageni wakishirikiana na zile za vijiji na kata, washirikiane na Maafisa wa Uvuvi ili kusudi kuwapa maelekezo wanaofanya biashara. Sisi hatuna tatizo juu ya kufanya biashara, lakini kwa wageni ni muhimu wanunue bidhaa hizo wanazozikusudia katika masoko ya kimataifa yaliyotengwa kwa kazi hiyo na hili tutakwenda kulisimamia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni juu ya wale walikopeshwa boti lakini hazifanyi vizuri katika maeneo ya Ziwa Victoria. Ninashukuru sana kwa jambo hili na ninashukuru pia vilevile kwa pongezi ni kwamba tumeanza na wakati wote wakati tunaanza ni lazima zitokee changamoto za namna hii.

Mheshimiwa spika, walio wengi katika boti tulizozikopesha wanashukuru na wanafurahi na wanaendelea na shughuli zao, lakini wachache ambao wamekutana na hiyo changamoto, Serikali tayari tumeshakaa nao tumekubaliana na benki yetu ya kilimo tunakwenda kufanya marekebisho ya yale makosa yaliyoonekana ili kusudi tuweze kusonga mbele na lile azimio zuri kabisa la utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE SHABANI NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, wavuvi katika Ziwa Tanganyika wamefunga uvuvi kwa mpango wa Serikali na watafungua tarehe 15 Agosti, 2024 na ahadi ya Mheshimiwa Waziri ambayo ni ahadi ya Serikali ilikuwa ni kuongeza vizimba na kuwasaidia vifaa

vya uhifadhi wa samaki. Nataka Mheshimiwa Waziri atupe *commitment* kwenye Bunge hili kwamba jambo hilo litatekelezwa kabla ya wao kufungua? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba nijibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini na kwa niaba ya Wabunge wengine wote wa Ziwa Tanganyika ambao wameunga mkono jambo hili vizuri na sasa linaleta matokeo mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali tumejipanga, tunakwenda kuwakabidhi wavuvi hususani makundi ya wakinamama *cool boxes* ambazo zitakwenda kuwasaidia kwa sababu tunajua kwamba mazao yatakayopatikana ni mengi. Kwa hivyo, kabla ya tarehe 15 Agosti tutafanya utaratibu wa kwenda kugawa katika vikundi vya wakinamama wachakataji na wafanyabiashara ya samaki kwenye mialo ya Kibirizi, Kagunga na kwingineko ili kusudi waweze kufanya biashara zao vizuri na samaki wataokaowapata wasiharibike.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel.

Na. 722

**Bei Elekezi kwa Kilo ya Nyama na Mazao ya Mifugo**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL K.n.y. MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kupanga bei elekezi kwa kilo ya nyama na mazao mengine ya mifugo kama ilivyo kwa mazao ya kilimo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa haipangi bei elekezi ya kilo ya nyama na mazao mengine ya mifugo bali bei hupangwa na nguvu ya soko ambayo huamua bei ya kilo ya nyama katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea na mikakati ya kurasimisha biashara ya mifugo na mazao yake ikiwemo kusimika mizani katika minada ya mifugo ya awali na upili ili mifugo iweze kuuzwa kwa uzito ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya mizani 82 ilinunuliwa. Mkakati mwingine ni ujenzi wa vituo vya kukusanya maziwa maeneo mbalimbali nchini ili kuongeza vituo rasmi vya kukusanya na kuuza maziwa.

Mheshimiwa Spika, urasimishaji wa biashara ya mifugo na mazao yake utawezesha Serikali kubaini gharama halisi katika mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo hivyo kusaidia kutoa mwongozo ikiwemo bei ya mazao ya mifugo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wafugaji wa Wilaya ya Longido wanapeleka ng'ombe kuuza kwenye kiwanda na mwenye kuamua bei ni mwenye kiwanda, wakati mwingine hahesabu maeneo mengine ya nyama kama utumbo na ngozi. Je, nini kauli ya Serikali kuhusu jambo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Jimbo la Arumeru Magharibi kuna wafugaji wa ng'ombe wa maziwa wanapeleka maziwa kwenye viwanda vidogo vidogo na kuuza maziwa hayo kwa bei ya chini sana, kiasi cha shilingi 500 mpaka 700 kwa lita. Je,

nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wafugaji hawa wanaongezwa bei ili waweze kuinua maisha yao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Noah, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza juu ya jambo la nyama katika Kiwanda cha *Eliya Food* kilichopo pale Longido, wafugaji huwa wanauza kulingana na bei ya soko, kama nilivyosema katika jibu la msingi, tulikwenda na kuwasilikiza wafugaji tukiwa pamoja na watu wa kiwanda na jambo hili tumekwishalimaliza kwamba mfugo unauzwa kwa bei ya mfugo hai kwa kilo na sasa tumeweka utaratibu ambao ni wa wazi, mfugaji anapopeleka mbuzi au ng'ombe au kondoo wake anaona kilo zinazosoma pale katika mzani, anazidisha mara bei iliyopangwa. Kwa msingi huo, anapata chote ikiwa ni pamoja na utumbo, mkia, kwato, kila kilicho katika mfugo ule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimtoe hofu na sisi Serikali tunaendelea kulifuatilia kwa karibu jambo hili ili kulinda maslahi mapana ya wafugaji wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei ya maziwa kuwa ni ndogo pale Arumeru, namshukuru kwa swali hili. Serikali imekwisha kufanya *study* na kugundua kwamba tatizo kubwa linalopelekea bei ya maziwa ya mfugaji kuonekana kuwa ni ndogo ni gharama za uzalishaji kwa lita moja ya maziwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali imejipanga na inakuja na mradi mkubwa na kimsingi mradi huu ni wa kuongeza uzalishaji wa maziwa, lakini pili ni kupunguza gharama ya uzalishaji hasa katika eneo la upatikanaji wa chakula kitu ambacho ndiyo kinapelekea kufanya bei ya maziwa iwe kubwa, ambapo mradi utagawa mashine za kusaidia kuchakata vyakula vya ng'ombe hususani wa maziwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Noah na Wabunge wengine mradi huu tunakuja nao, ashsante.

**SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, sasa aulize swlai lake.

Na. 723

**Muswada wa Sheria Utakaokidhi Haki Nane za Kimataifa za Kumlinda Mtumiaji**

**MHE.DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italeta muswada wa sheria utakaokidhi haki nane za kimataifa za kumlinda mtumiaji/mlaji kama zilivyopitishwa na Azimio la Umoja wa Mataifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika Azimio la 39/248 la tarehe 16 Aprili, 1985 ulipitisha miongozo ya kuwalinda watumiaji au walaji na kuzitambua haki nane za mtumiaji au mlaji. Miongozo hiyo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2015 na toleo lililorekebishwa la miongozo hiyo lilipitishwa katika Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika Azimio la 70/186 la tarehe 22 Desemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa sheria kuu inayolinda haki za watumiaji au walaji ni Sheria ya Ushindani Na. 8 ya mwaka 2003. Sheria hiyo inatambua na kuheshimu haki za Kimataifa za mtumiaji au mlaji. Haki hizo nane zimezingatiwa ipasavyo katika Sheria ya Ushindani.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Ushindani Na. 8 ya mwaka 2003 ambao utasaidia utatuzi wa malalamiko ya watumiaji kwa njia ya usuluhishi, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kujua kama marekebisho yatazingatia kutenganisha Sheria ya Ushindani na kutunga sheria mahsusi ya kumlinda mtumiaji.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Tume ya Ushindani imelemewa na majukumu mengi na hivyo kusababisha kutowalinda watumiaji ipasavyo.

Je, Serikali haioni kuna uharaka wa kuleta sheria hii hapa Bungeni, tukatenganisha ushindani na tukatunga sheria mahsusi ya kuwalinda walaji iweze kuwahudumia Watanzania kwa ujumla? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu amekuwa mdau mkubwa wa kufatilia suala la kuwalinda walaji hapa nchini na mara nyingi amekuwa akiuliza suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza, tujue haki hizi za walaji zina historia yake, zilianza mwaka 1962 ambapo Mheshimiwa Rais wa Marekani John F. Kennedy alianzisha na kulikuwa na haki nne, aliasisi haki nne.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na malalamiko mengi kwamba bado hatujawalinda walaji ipasavyo na ndiyo maana tumesema sasa tunataka tufanye mapitio na

marekebisho ya sheria yetu ya ushindani. Sasa suala la kwanza katika marekebisho hayo tutapata maoni na hay ani maoni ambayo ametoa Mheshimiwa Mbunge kuona kama tunaweza kutunga sheria mpya ambayo itajitegemea ya kumlinda mlaji.

Mheshimiwa Spika, utafiti na uzoefu uliopo katika nchi nyingi ikiwemo Marekani yenyewe ambayo iliasisi hizi haki za kumlinda mlaji, bado wanatumia taasisi moja ambayo ndiyo inakuwa na sheria ya kumlinda na kumtetea mlaji, lakini kwa sababu ya hoja hiyo, Waheshimiwa Wabunge watatoa maoni ili tuone kama tutakuja na sheria mpya badala ya hii ya ushindani.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, siyo kweli kwamba Tume ya Ushindani imezidiwa, lakini nadhani ni changamoto ambazo kila wakati tutaendelea kuzitatua kwa sababu kadiri unavyofanya kazi changamoto nyingine zinajitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *FCC* inaendelea kutekeleza majukumu yake vizuri ipasavyo, lakini changamoto zinajitokeza kila siku na hizi tutaendelea kuzifanyia kazi kama ambavyo nimesema, mojawapo ni kuona namna gani tutapitia marekebisho ya sheria hizi ili ziendane na hali ya sasa ya ushindani na tumtetee vizuri mlaji, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 724

**Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Kukusanya na Kutumia *Passenger Service Charge***

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza: -

Je, lini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itaruhusiwa kukusanya na kutumia *passenger service charge* kuboresha viwanja vya ndege? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2017 Serikali ilifuta utaratibu wa *retention* kwa Taasisi za Umma kupitia hotuba ya Waziri wa Fedha kwa mujibu wa kifungu na. 58 (a) mpaka (c) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo ndio ulikuwa ukitumika kuipatia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* mapato yatokanayo na *passenger service charges.* Tangu kipindi hicho, Serikali imeendelea kuipatia *TAA* ruzuku kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida ikiwemo mishahara na matumizi mengineyo ili kuhakikisha kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania inaendelea kutoa huduma stahiki.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na maoni ya wadau mbalimbali wakiwemo Wabunge, Serikali imepokea maoni hayo na inayafanyia kazi ili kuona namna nzuri ya kutekeleza suala hilo bila kuathiri uendeshaji wa shughuli za Kitaifa zinazofanyika kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba leo Muswada Mpya wa Sheria ya Viwanja vya Ndege utasomwa kwa mara ya kwanza hapa Bungeni. Je, Serikali imezingatia matakwa ya kimataifa ya

kuiwezesha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kukusanya na kuiacha *passenger service charges* kwa ajili ya kuendesha viwanja vyake na shughuli za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, tunatambua ni kiasi gani *Royal Tour* imelifanya Taifa letu kukusanya fedha nyingi kupitia watalii.

Je, haioni haja ya kuboresha viwanja vyetu vya ndege kwa kutumia *passenger service charges* kutawezesha na kitakuwa ni kigezo muhimu cha kuwafanya watalii waichague Tanzania kama *the best tourism destination in the world?* *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa *Engineer* Ulenge kwa kazi kubwa aliyoifanya kimsingi katika kufuatilia jambo hili ili Serikali ilitazame kwa kina zaidi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda kujibu swali lake, pia naliarifu Bunge lako Tukufu ili tuungane kwa pamoja kutambua kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika uboreshaji wa viwanja jambo ambalo limepelekea mpaka Mheshimiwa Rais wetu kutunukiwa shahada maalum kwenye sekta ya anga na Chuo Kikuu cha Sayansi cha Korea mapema mwezi huu. Hii inatokana na mchango mkubwa ambao dunia inatambua na inathamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye swali lake, moja ni kwamba *passenger service charges* imetajwa kama chanzo cha mapato katika muswada utakaowasilishwa leo Bungeni, lakini pili, tunaona umuhimu mkubwa sana wa namna ambayo pengine *TAA* ikiachiwa kukusanya mapato hayo na ndiyo maana kwenye jibu letu la msingi kama Serikali tumesema tunaendelea na hatua mbalimbali za ndani ili kuona namna bora ya kutekeleza takwa hili ambalo Wabunge wengi wamekuwa wakilizungumza pasipo

kuathiri uendeshaji wa shughuli za Serikali na za nchi ambazo zinategemea Mfuko Mkuu wa Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, sasa aulize swali lake.

Na. 725

**Kuzalisha Mbegu za Mti wa Mninga kwa Ajili ya Zao la Biashara**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itazalisha mbegu za mti wa mninga ili kufanya mti huo kuwa zao la biashara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa niaba ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Ama? Mheshimiwa Waziri si yuko hapa?

Hapana, Mheshimiwa Waziri, njoo ujibu swali. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kunakuwapo na vyanzo endelevu vya uzalishaji wa mbegu bora za miti sambamba na ulimaji miti hiyo kibiashara, Serikali kupitia *TFS* imeanzisha upandaji wa miti jamii ya mninga katika mashamba yake.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa miti hiyo imepandwa katika shamba la Miti Ruvu lililoko Kibaha – Pwani, katika shamba letu la Miti la Mpepo lililoko Nyasa – Ruvuma, pamoja na Shamba la Mbegu za miti lililoko Kising'a katika Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo, Serikali imejizatiti kuongeza ukusanyaji wa mbegu, kuotesha na kusambaza mbegu bora na miche ya mninga kwa wadau mbalimbali kupitia vituo vyake vya uzalishaji mbegu za miti.

Mheshimiwa Spika, mathalani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia *TFS* ilikusanya jumla ya kilo 237 za mbegu za mninga kutoka katika vyanzo mbalimbali. Vilevile kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2024 Serikali ilifanikiwa kuzalisha na kugawa kwa wadau mbalimbali jumla ya miche ya mninga 5,115.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, Sikonge sisi tuna kilometa za mraba 26,000 ambazo tumezihifadhi kwenye misitu ya vijiji, halmashauri na Serikali Kuu na tuna ofisi kubwa sana ya *TFS* katika Wilaya yetu. Sasa la kwanza, ilikuwaje vitalu vikapandwa Ruvu, Iringa na Nyasa kule Ruvuma badala ya kupanda Sikonge hata kama tungepata vitalu vitatu au vinne? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, huu mninga ambao ni mti muhimu sana duniani, ni lini sasa Serikali itafanya maamuzi ya kuhakikisha kwamba wananchi wanaipanda kibiashara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kakunda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kama tulivyoeleza katika jibu la msingi tumeanza katika Mkoa wetu wa Pwani, pamoja Iringa na Mkoa wa Ruvuma kupitia wilaya yetu ya Nyasa. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba lengo la Serikali sasa hivi ni kuendelea kupata vyanzo vingi zaidi vya miti yetu ya asili

ikiwemo mninga, mivule pamoja na mingine ili iweze kutumika kibiashara, lakin tumeanza katika mikoa hiyo minne kupitia mradi wetu wa Panda Miti Kibiashara, Mkoa wa Iringa, Morogoro, Ruvuma na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa namhakikishia kuwa Mkoa wa Tabora ni moja ya mkoa ambo tunaenda kuongeza mashamba na tutaenda kuongeza mashamba pia katika Mkoa wa Katavi, Lindi, Kigoma, Mbeya pamoja na Iringa.

Mheshimiwa Spika, la pili, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa tutaendelea kuhamasisha taasisi za sekta binafsi pamoja na muungano wa wananchi kupitia vyama mbalimbali vya wakulima wa miti ili na wenyewe waweze kupanda miti hii ambayo imeanza kuwa adimu na imeanza kutoweka badala ya kupoteza fedha kuagiza mbegu za miche hii bora kutoka katika nchi jirani ikiwemo Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa sasa tumeendelea kupanda kupanda katika mashamba yetu mbalimbali 28 ambayo yana miti ya asili na miti hii ya kigeni. Sasa tumeona nchi za jirani pia wakija kujifunza kutoka kwetu na tunaamini tutajitosheleza katika mbegu hizi za miti bora ambayo imeanza kupotea kwa ajili ya mahitaji ya ndani pamoja na kuweza kuuza nje na kupata fedha za kigeni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhifadhi miti ya mpingo ili kusudi nayo isiweze kupotea? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Toufiq kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli miti hii imeanza kupotea kama nilivyoeleza katika jibu la msingi na tulichokifanya hivi sasa tumekusanya zaidi ya hizo kilo 257 na tunaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na chanzo cha uhakika cha mbegu hizo za asili ikiwemo mpingo na miti mingine, lakini pia tumeanza kuipanda katika hifadhi zetu za miti mbalimbali ya mbegu bora ili kuwa na uhakika pamoja na kuweza kuwagawia wananchi ili nao waweze kuipanda katika mashamba yao ya miti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa kuna miti ya mninga ambayo ni ya asili kwenye mashamba ya wakulima mbalimbali kwenye Mikoa ya Morogoro na Pwani, je, kuna mkakati gani wa kuhifadhi hii miti ambayo ipo mpaka sasa hivi kwenye mashamba hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ambaye ninamfahamu kama mbobezi katika masuala mazima ya upandaji wa miti na tunampongeza.

Mheshimiwa Spika, nikienda katika swali lake, ambacho tunakifanya sasa, tunaendelea kufanya *stocktaking* ili kuweza kujua kwanza wakulima wetu wa mbegu za aina mbalimbali, lakini pili, tunachokifanya, tunaendelea kuhakikisha kwamba tunawapatia mafunzo na huduma bora ili waweze kujua waandae vipi vitalu vyao, wavihudumie kwa namna gani na pia wajue jinsi ya kuviendeleza.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea kuwasaidia katika huduma mbalimbali za ugani na kuweza kuwagawia mbegu hizi za miti ili waweze kupanda katika mashamba yao ili kuweza kuwa na ziada katika mbegu za miche iliyo bora.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, yuko Sheikh mmoja anaitwa Sheikh Mohamed wa Msikiti wa Tanangozi, amekuwa akiotesha hizi mbegu za miti ya asili ukiwemo mninga. Je, mpo tayari kushirikiana naye kwa ukaribu kwa kuwa amekuwa akijitolea na kugawa kwa wananchi bure ili mmuwezeshe aweze kugawa kwa watu wengi zaidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba kujibu swali la Mheshimiwa Msambatavangu, kwanza, nampongeza huyo Sheikh wa Tanangozi kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na vyanzo vya uhakika vya mbegu za miti hii bora.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia kwamba tutashirikiana naye, tunao Mfuko wetu wa Misitu wa *TaFF* na tumekuwa tukitoa ruzuku mbalimbali kwa mtu mmoja mmoja, lakini vilevile kwa taasisi na mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali. Nitamtafuta na nitaomba *data* zake ili tuweze kuwasiliana nae kwa ajili ya kuweza kumwezesha ili aweze kusaidia zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya hili lililotokea, nitoe maelezo kidogo kwa sababu Mheshimiwa Kitila Mkumbo amewahi kuwepo hapa Bungeni na maswali yake yakajibiwa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kigahe na ni kwa sababu wakati huo Mheshimiwa Profesa Kitila hakuwa na Naibu Waziri.

Kwa hiyo, hakuna mazingira ambayo Mheshimiwa Waziri atakuwepo, halafu Naibu Waziri mwingine aje ajibu swali wakati wizara ina Naibu Waziri.

Kwa hiyo, nimeona niliweke hili sawa ili isije ikaonekana, mbona Mheshimiwa Kigahe alikuwa anaenda kujibu wakati Mheshimiwa Kitila yupo, hiyo ni kwa sababu Profesa Kitila wakati huo hakuwa na Naibu Waziri. *(Makofi)*

Kazi ya kujibu maswali ni ya, ikitokea Serikali kweli amepewa mtu halafu Mheshimiwa Waziri hayupo na Naibu, hayo yataendelea. Nayo kwa kipindi hiki tumejitahidi sana kupanga maswali ambayo Mawaziri wapo ama Naibu Waziri yupo. Ni machache sana ambayo yametokea anajibu mtu wa Wizara nyingine.

Kwa hiyo, mazingira ni hayo, maana lazima niliweke sawa ili mfahamu. Mimi huwa napenda kutenda haki na haki ndiyo imesimama kwa sura hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya ufafanuzi huo, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 726

### Serikali Kutoa Mashine kwa Vikundi vya Wanawake vya Ubanguaji Korosho

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kupitia *SIDO* kutoa mashine ndogo na rahisi kwa vikundi vya wanawake vya ubanguaji korosho Mkoani Mtwara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024 kupitia Shirika la Viwanda Vidogo *(SIDO)* imeendelea kushirikiana na wadau wengine katika tasnia ya korosho kuwezesha utengenezaji na usambazaji wa mashine ndogo za kubangulia korosho kwa vikundi vya vijana na wanawake.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 jumla ya mashine 100 zenye uwezo wa kubangua kilo nane mpaka 12 kwa siku zimenunuliwa na kusambazwa kwenye vikundi vya ubanguaji katika mikoa inayozalisha korosho. Kati ya hizo, mashine 71 zimesambazwa kwenye vikundi 15 vya vijana na wanawake wanaojishughulisha na ubanguaji wa korosho Mkoani Mtwara.

Mheshiwa Spika, Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na *NMB Foundation* wametoa mafunzo kwa wabanguaji wa korosho 537 wakiwemo wanaume 160 na wanawake 377 kutoka Wilaya za Newala, Tandahimba, Nachingwea na Ruangwa. Aidha, zoezi la kutoa mafunzo kwa wabanguaji linaendelea kwa Wilaya zote zinazozalisha zao la korosho hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, natambua mashine 100 zilitolewa na Bodi ya Korosho kwa fedha za *Korosho Marathon* zilizotengenezwa na fundi Mbwana.

(a) Je, *SIDO* yenyewe haiwezi kutengeneza mashine rahisi ikawauzia wabanguaji wadogo wa korosho kwa bei nafuu? *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuongeza mnyororo wa thamani katika zao la korosho, je, Serikali haioni haja ya kuwekeza kwa viwanda vidogo vinavyoweza kutengeneza pombe inayotokana na mabibo makavu *almaarufu* kama kochoko ili kupunguza pia msuguano wa *ethanol* ambao tumeujadili kwenye siku ya jana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kwamba *SIDO* wanaweza hilo jukumu ndiyo maana wanashirikiana na wadau na nimthibitishie tu kwamba sisi tutaendelea kushirikiana na *SIDO* kuhakikisha kwamba tunapunguza gharama za hizi mashine ili hata wale wananchi wa kawaida wanaotaka waweze kununua wao wenyewe binafsi kutoka *SIDO*. Kwa hiyo, niseme tumelipokea kwa uzito mkubwa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongeza thamani ikiwemo kutengeneza viwanda vidogo vya kuzalisha pombe ususani pombe ya *ethanol* na lenyewe tumelipokea kwa sababu ni sehemu ya mipango ya Serikali kuhakikisha kwamba zao la korosho likiwemo lile bibo linatumika kwa ajili ya biashara yaani kwa kuongeza thamani na kuweka biashara kwa wananchi wetu wa kawaida, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Mbunge ni swali namba 727.

Na. 727

**Viongozi wa Vyama vya Msingi Waliodhulumu Wakulima wa Kahawa - Mbozi**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawachukulia hatua viongozi wa Vyama vya Msingi waliodhulumu fedha za wakulima wa kahawa - Mbozi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya uchunguzi kwa Vyama vya Ushirika 20 vilivyopo Wilayani Mbozi ambapo kati ya hivyo,

vyama nane vimekutwa na changamoto mbalimbali ikiwemo wakulima kupunjwa malipo ya mauzo ya kahawa, vyama kutowasilisha makato ya ushuru kwa halmashauri na watoa huduma na baadhi ya kampuni za ununuzi wa kahawa kushindwa kulipa fedha za mauzo ya kahawa kwa Chama cha Ushirika.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchunguzi, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imekamilisha mapitio ya taarifa hizo na kuanza kuchukua hatua stahiki kwa viongozi na watendaji waliobainika kuhusika na ubadhilifu uliojitokeza.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na viongozi wa vyama vya ushirika kuondolewa kwenye uongozi na kufunguliwa kesi katika Mahakama ya Hakimu Mfawidhi wa Mkoa wa Songwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimsahihishe Mheshimiwa Waziri ni miaka miwili imepita sasa hakuna hata mmoja ambaye amefikishwa Mahakamani, hiyo kesi ipo tu kwa Mwendesha Mashtaka lakini bado haijapelekwa Mahakamani, sasa ni lini hawa watuhumiwa ambao wameiba hizi fedha za wakulima watafikishwa Mahakamani?

Mheshimiwa Spika, kingine ni kwamba vyama vilivyofanyiwa ukaguzi ni vyama 20 kati ya vyama zaidi ya 100 sasa ni lini ukaguzi wa vyama vingine vilivyobaki utafanyika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, taarifa ambayo tuliipata mpaka jana ni kwamba

wametuthibitishia kwamba wameshapeleka Mahakamani, lakini mimi nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge Mbozi ni Jirani kwetu na mimi baada ya Bunge hili nitapita pale na kushuhudia yote ambayo kama Mheshimiwa Mbunge anayasema. Nitakwenda mimi mwenyewe, lakini taarifa za jana tulizo *confirm* ni kwamba wameshawapeleka Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyama 20 ni kwamba ni kweli vyama 20 tulivyofanyia uchunguzi ni vile ambavyo vilikuwa na changamoto kubwa katika vile vyama 100 kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge anachotaka ni kwamba tupitie sasa vyama vyote kuliko vile 20 ambavyo vilikuwa na changamoto.

Kwa hiyo, sisi tutaendelea kupokea na kuangalia vyama vile ambavyo vina changamoto kubwa kwa wananchi. Niseme tu kwamba hili aliloleta Mheshimiwa Mbunge ni kama ombi na sisi tunaendelea kulifanyia kazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako mazuri kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

Na. 728

**Hitaji la Vitambulisho vya *NIDA* Karagwe na Kyerwa**

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo la vitambulisho vya *NIDA* kwa kuwapatia namba za *NIDA* wananchi wa Wilaya Karagwe na Kyerwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mhandisi Masauni, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalaum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Karagwe na Kyerwa jumla ya namba za utambulisho 102,440 zimezalishwa na kugaiwa kwa wananchi ambapo katika Wilaya ya Karagwe ni 64,833 na Wilaya ya Kyerwa 37,607. Aidha, katika Wilaya ya Karagwe vitambulisho 57,148 sawa na 90.9% ya vitambulisho 62,820 vimechukuliwa na wananchi na katika Wilaya ya Kyerwa jumla ya vitambulisho 26,870 ambayo ni sawa na 75.6% ya vitambulisho 35,501 vimechukuliwa na wananchi kupitia Ofisi za Serikali za Mitaa na Vijiji. Zoezi la uzalishaji wa namba za utambulisho, uzalishaji, usambazaji na ugawaji vitambulisho bado linaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe rai kwa wananchi wote ambao bado hawajachukua vitambulisho vyao kufika katika Ofisi za Serikali za Mitaa na Vijiji walipojiandikishia katika wilaya hizo kwa ajili ya kuvichukua vitambulisho vyao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya ya Kyerwa tangu mwaka 2018 zaidi ya wananchi 120,000 waliweza kujaza fomu na kuomba vitambulisho vya *NIDA,* lakini Mheshimiwa Waziri anasema hapa vilivyotolewa ambavyo vipo tayari ni 64,000 vimebaki 56,000.

Sasa ni kwa nini Serikali isione umuhimu wa kupeleka mashine kila kata kule Kyerwa kama tatizo ni mashine ili wananchi hawa 56,000 waweze kupatiwa haki yao kupata vitambulisho?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kumekuwa na ucheleweshaji sana wa kutolewa vitambulisho hivi au haki kwa Mtanzania hasa kwa maeneo ya mpakani vikihusishwana sana na *vetting* ambazo zinafanywa na maafisa husika kama kule kwetu Rorya na Tarime. Serikali haioni kwamba kuna haja kuja na mkakati mpya wa

kuepeleka maafisa wenye uelewa mpana na wananchi wanaoishi kule mpakani ili wananchi hawa wa mpakani waweze kupatiwa haki yao kuliko hivi sasa wanazungushwa kutokupewa haki yao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri juu ya changamoto za upatikanaji wa vitambulisho hususani kwa wananchi ambao wanaishi maeneo yaliyo karibu na mipaka ya nchi. Changamoto hii inasababishwa zaidi kutokana na muingiliano mkubwa uliopo baina ya wananchi wanaoishi katika maeneo hayo na raia wengine wasiokuwa wananchi wa Tanzania ambao wamekuwa wakiingia kupitia mipaka, hivyo inailazimu Serikali Serikali kuwa makini sana katika kuhakikisha kwamba inafanya uhakiki wa kina kujiridhisha juu ya uhalali wa mtu ambaye anapaswa kupata kitambulisho hicho kama anakidhi vigezo na sifa. Hilo ndiyo jambo ambalo limesababisha kuwa changamoto ambazohata katika wilaya hizi zilizotajwa hapa imekabiliana nazo.

Mheshimiwa Spika, nini Serikali inafanya kudhibiti hatua hiyo. Serikali imechukua hatua nyingi na hatua hizi zimechukuliwa kwa dhamira ya kuhakikisha kwamba Watanzania wenye sifa na vigezo wanaoishi katika maeneo yao wanapata haki stahiki na kwamba kuishi kwao au kuzaliwa kwao mipakani kusiwe sababu ya kuona wananyanyasika katika kupata haki zao za msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuna haja na umuhimu wa kuhakikisha kwamba Serikali inafanya kila linalowezekana kudhibiti hali ya usalama wa nchi yetu hasa unaosababishwa na uingiaji wa watu kilingana na hali ya mipaka yetu ilivyo. Kwa hatua ambazo kwa upande wa *NIDA* zimechukuliwa, kwanza ni kuja na mkakati kabambe ambao umeanzishwa katika maeneo ya mpakani.

Mheshimiwa Spika, katika kulithibitisha hilo mimi mwenyewe nilizindua mkakati huo kwa kuanzia na Mkoa wa Mara katika maeneo ya mpakani pale ambapo baada ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kutoa fedha zote zaidi ya shilingi bilioni 42.5 zilizopelekea kuzalisha *almost* kadi zote kwa watu wote ambao wana namba za utambulisho tukaanza uzinduzi wa zoezi hilo katika mikoa ya mipakani kuhakikisha kwamba tunakwenda kupeleka kadi zote kwa wananchi na kuwashirikisha Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapa utagundua kuna kadi nyingi sana ambazo bado wananchi hawajazichukua kwa mfano kwa Kyerwa na Karagwe kwa takribani vitambulisho 14,303 ambavyo bado havijachukuliwa na wananchi. Kwa hiyo kazi hii imeleta tija kiasi fulani, hata hivyo nichukue changamoto ambazo amezieleza Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuchukua maoni ya Waheshimiwa Wabunge na kufanyia kazi yale mapungufu mengine ambayo yanajitokeza hatua kwa hatua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la upatikanaji wa Vitambulisho vya *NIDA* Wilayani Kyerwa limeuwa ni kero ya miaka mingi unakuta baba ana kitambulisho, mama ana kitambulisho, lakini mtoto hana kitambulisho. Je, upo tayari kuja Wilayani Kyerwa kufanya mkutano wa hadhara ili kusikiliza kero hizi muone ni namna gani mtakavyozitatua kuwapatia wananchi wa Kyerwa vitambulisho vya *NIDA? (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bilakwate kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimuahidi Mheshimiwa Bilakwate kwamba mimi na yeye tutapanga ratiba hiyo mara baada ya kukamilika kwa Bunge hili tuweze kwenda tukasikilize wananchi kuhusiana na changamoto ambazo amezieleza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali lla nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbogwe ina changamoto ya vitambulisho wananchi walishajiandikisha muda mrefu lakini hawajapata vitambulisho hivi, ni lini wananchi wa Mbogwe watapata vitambulisho hivyo vya *NIDA*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwamba kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa vitambulisho sasa siyo changamoto tena, lakini kama kuna changamoto kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anaiuzungumza katika jimbo lake nadhani labda mimi na yeye tukae ili tuweze kupata orodha ya watu hawa ambao wamekosa hivyo vitambulisho tuweze kuchukua hatua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 729

**Maslahi ya Askari wa Uhamiaji**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaboresha maslahi ya askari wa Idara ya Uhamiaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha maslahi ya Maafisa, Wakaguzi na Askari wa Idara ya Uhamiaji kadiri hali ya kifedha inavyoruhusu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali iliridhia posho mbalimbali ambazo ni posho ya chakula, nyumba, ujuzi na utaalamu na katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imeongeza posho ya upelelezi, madaraka, intelijensia na ukufunzi. Aidha, Idara ya Uhamiaji imeendelea kuongeza nyumba za makazi za watumishi ambapo hadi sasa ina majengo 465 yanayokaliwa na familia 465.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza, je, Serikali ina mkakati wa kuwaongezea posho ya mazingira magumu ya kazi ukizingatia wanafanya kazi katika mazingira magumu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inajenga ofisi kwa ajili ya idara hii hasa wilayani kwa sababu kwa hali iliyopo sasa Idara hii ya Uhamiaji inakuwa inapewa chumba au vyumba katika Ofisi za Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa kufanya majukumu yake ambayo ni makubwa sana kwa nchi yetu? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Malapo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hoja ya kuongezwa posho ya mazingira magumu, kwanza nataka nimhakikishie kwamba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya kazi kubwa sana kuhakikisha inaongeza na kuimarisha maslahi ya askari wa vyombo vyote ikiwemo Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, katika kulithibitisha hilo, katika hii posho ya mazingira magumu ambayo Mheshimiwa Tunza Malapo amependekeza iongezwe, posho hii kwa muda mrefu ilikuwa hailipwi, lakini imeanza kulipwa mwaka jana wakati wa uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na katika mwaka huu wa fedha kama nilivyosoma katika bajeti tumetenga fedha za kutosha kwa ajili ya kulipa posho hii ambayo ilikuwa ni kero ya muda mrefu kwa askari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwanza hiyo ni hatua moja kubwa, hatua ya kulipa posho hii ambayo haikuwa inalipwa, kwa hiyo hatua ya pili ambayo Mheshimiwa Mbunge ameizungumza ya kuongeza kiwango ni wazo zuri, tutalichukua, tutalifanyia kazi pale ambapo hali itaruhusu basi nadhani itafikiria kuongezwa.

Mheshimiwa Spika, kazi ya uongezaji wa maslahi na stahiki tunaendelea nayo vizuri kupitia Tume Haki Jinai ambayo Mheshimiwa Rais ameunda imeitoa mapendekezo mbalimbali na apendekezo hayo yapo katika hatua nzuri za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la pili la kujengewa nyumba katika maeneo ya wilaya, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kupitia mkakati ambao tumeuzindua mwaka juzi wa ujenzi wa nyumba za askari pamoja na ofisi wa vyombo vyote vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Jeshi la Uhamiaji ni moja kati ya vyombo ambavyo vitaenda kufaidika na mpango huo na mpango huo tumeshaanza kuutekeleza hatua kwa hatua na unalenga katika kuhakikisha kwamba

maeneo yote ya wilaya za nchi hii yanapata ofisi za uhamiaji kwa kadiri hali ya ajeti itakaporuhusu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na askari wa uhamiaji katika Mkoa wetu wa Iringa, lakini hawajawahi kujengewa nyumba za kuishi. Je, ni lini sasa utawakumbuka askari wa uhamiaji Iringa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Iringa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua jitihada ambazo Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati amekuwa akichukua za kukabiliana na changamoto za askari wetu katika Mkoa wa Iringa kwa muda mrefu amekuwa ni mpambanaji mzuri. Nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwamba hoja yake hii tunaichukua na tutaufanya Mkoa wa Iringa ni miongoni wa mikoa ya kipaumbele pale ambapo mkakati wetu ambao nimeueleza unaendelea na utekelezaji wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako mazuri kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Toufik Salim Turky, Mbunge wa Mpendae swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Toufiq, naomba swali lake namba 730 lipatiwe majibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, kwa sababu humu ndani pia kuna Mheshimiwa Toufiq mwingine tutajie majina yake, Mheshimiwa Toufiq Salim Turky.

Na. 730

**Utitiri wa Kodi kwa Wawekezaji**

**MHE. TOUFIQ SALIM TURKY K.n.y. MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kunakuwa na muunganiko wa kodi ili kupunguza utitiri wa kodi usio wa lazima kwa wawekezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017 Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa biashara ilitoa mwongozo wa pamoja wenye dhima ya kuunganisha tozo na kodi mbalimbali kwa nia ya kupunguza utitiri wa tozo na kodi ili kuimarisha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, mpango huu umekuwa ukitekelezwa kwa ufanisi mkubwa kupitia marekebisho mbalimbali ya Sheria ya Fedha kuanzia mwaka 2018 hadi 2023 kwa kupunguza na kuondoa kodi na tozo mbalimbali. Hivyo, Serikali itaendelea kuhakikisha makubaliano yaliyofikiwa na wadau yanakamilishwa kama yalivyopangwa ili kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara nchini, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, swali la nyongeza.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini ili kuepusha changamoto ambazo zinawapata wafanyabiashara mbalimbali je, Serikali haioni umuhimu sasa ku-*centralize* mifumo hii ili kupunguza usumbufu kwa walipa kodi? La kwanza.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa sababu mifumo tunatengeza sisi na siyo *rocket science* je, ni lini Serikali inatuahidi italeta mifumo hii kwa haraka? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kabla ya kuanza kujibu nimpongeze sana Mheshimiwa Zahor kwa namna anavyofatilia suala hili.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza Mheshimiwa Zahor huko ndipo Serikali inapoelekea. Mwelekeo wa Serikali ni ku-*centralize,* kuifanya mifumo yote iwe kwa pamoja ili kupunguza utitiri lakini la usumbufu kwa wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Spika, nimtoe shaka Mheshimiwa Zahor kwamba huko tunapokwenda mifumo ikishaimarika basi *centralization* itapatikana.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, muda tu utakapokamilika mifumo yetu ambayo unaimarisha nchini basi tutatoa taarifa hiyo kwa wananchi wote na itafanyiwa kazi kadri ilivyopangwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako mazuri kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, Hoja ya dharura.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu, lakini pia majibu kutoka upande wa Serikali na sasa nilete matangazo niliyonayo hapa mbele kabla hatuajendelea na ratiba yetu.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na tangazo la wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, kwanza wageni waliopo Jukwaa la Spika na haw ani wageni wangu 28 ambao ni *Uyole Jogging Club* kutoka Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Mwenyekiti wa Umoja

wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Mbeya Mjini ambaye ni Ndugu Clemence Mwandemba, karibu sana. *(Makofi)*

Sasa hawa wote watasimama kwa pamoja, lakini yupo Ndugu Athumani Likomile ambaye ni Mwenyekiti wa *Uyole Jogging Club* ameongozana na Ndugu Sabela Kapufi ambaye ni Katibu wa Chama cha *Jogging* Mkoa wa Mbeya na yupo Ndugu Tulinave Chanimbaga ambaye ni Katibu *Uyole Jogging Club*. *(Makofi)*

Wageni wote 28 simameni kwa pamoja na karibuni sana Bungeni, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mbunge uliyeenda kumtembelea Mheshimiwa Waziri Mkuu nazungumza.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni Dkt. Jim Yonazi ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. *(Makofi)*

Wapo wageni mbalimbali wa kwenu Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo - Waziri wa Nchi, Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira hawa ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni Yussuf ambaye ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hawa ni Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Kikwajuni, Zanzibar. *(Makofi)*

Wapo wageni kumi wa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta ambao ni viongozi wa Vituo vya Huduma ya *Mtoto Cluster* ya Urambo, Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile ambao ni wafanyabiashara wa suti na viatu *Alfredo*

*Store* kutoka Masaki, Jijini Dar es Salaam na Medeli Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Taska Mbogo ambaye ni Mwenyekiti Mstaafu wa Jumuiya ya Vijana Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, mdau wa maendeleo kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu ambaye ni ndugu yake kutoka Arusha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo ambao ni watumishi wa Mungu kutoka Arumeru, Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete na Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara ambao ni Makatibu wa Waheshimiwa Wabunge kutoka Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ambao ni wapiga kura wake kutoka Bahi, Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni sita wa Mheshimiwa Stella Simon Fiyao ambaye ni mtoto wake pamoja na wadogo zake kutoka Mkoa wa Songwe, karibuni sana. Mtoto wa Mheshimiwa Mbunge ndiye yupi ama ni wale watoto wa nanii, kuna mwanao pale juu au ni mtoto wa sifa. Haya jamani, ahsante sana, karibu sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni mtoto wake jamani maana kuna watoto wa kulea, kuna watoto wanakuwa watu wazima zaidi, haya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni saba wa Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza ambao ni watoto wake kutoka Bukoba, Mkoa wa Kagera, haya, ahsante sana. *(Makofi)*

Sasa wote hawa ni watoto, wake kwa hiyo wa kulea wa kuzaa wote kwa pamoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni 18 wa Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda ambayo ni Timu ya Mpira wa Kikapu kutoka Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Wageni 26 wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ambao ni Madiwani kutoka Geita Mjini wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni 13 wa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar ambao ni wanafunzi wa Udaktari wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Francis kutoka Ifakara, Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wageni 50 wa Mheshimiwa Minza Simon Mjika ambao ni waimbaji wa Kwaya ya Waadventista Wasabato kutoka Kanisa la Kana, Mkoa wa Tanga, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, yupo Sheikh Ahmed Kandauma ambaye ni Mkurugenzi wa *Irshaad Foundation* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo linatoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu inawaalika kuhudhuria Maadhimisho ya Siku ya Kumbukumbu ya Mashujaa tarehe 25 Julai, 2024 katika Uwanja wa Mashujaa uliopo Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma. Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waheshimiwa Wabunge, wote mnakaribishwa kwa ajili ya kuwakumbuka mashujaa wetu hawa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya tunaendelea na ratiba yetu.

Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau.

## JAMBO LA DHARURA

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi na kwa mujibu wa Kanuni ya 54 ya Kanuni za Bunge, lipo suala la dharura.

Mheshimiwa Spika, Jimboni kwangu kule Kiteto, linahusu Kijiji changu kinaitwa cha Ilkiushbor, hiki kijiji kimeanzishwa mwaka 1989 na tuna mgogoro wa muda mrefu sasa na pori linaloitwa la Mkungunero. Pori la Mkungunero kwa mujibu wa *GN* limeanzishwa mwaka 1996 lakini kwa muda mrefu sasa kumekuwa na *harassment* zinazoendelea kwa wananchi wangu kwa muda mrefu kidogo sasa.

Mheshimiwa Spika, timu ya Mawaziri nane ambayo inatembea nchi nzima, ripoti yao ni ya tarehe 23 Septemba, 2019, lakini tarehe 29 Septemba, 2020 Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuja kunitafutia mimi kura kwenye hiki kijiji akiwa Makamu wa Rais na wananchi wakatoa malalamiko yao kuhusu *harassment* na mgogoro huu wa Pori la Akiba la Mkungunero. Kwa hiyo, kwa lugha nyepesi Mheshimiwa Rais ndiye wa mwisho kufika pale hata kabla ya wale Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kuja Bungeni nilizungumza hapa mara kadhaa kuhusu Serikali kutatua ule mgogoro. Timu ya Mawaziri nane tarehe 9 Oktoba, 2021 waliteremka na helikopta pale kijijini kwa wakati huo ilikuwa inaongozwa na Mzee Lukuvi na akawaambia wananchi Mheshimiwa Rais amesema kijiji hiki hakina shida na kitabaki na nitakutumia *clip* zake. Tuka-*celebrate* na tukaondoka.

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Novemba, 2022 Mheshimiwa Rais alikuja Manyara, aliyekuwa Waziri wa Ardhi wa kipindi hicho Mheshimiwa Mabula mbele ya Rais alirudia maneno hayo hayo ya Mheshimiwa Lukuvi kwamba vijiji vya Kiteto haviondoki. Tukajua mgogoro umeisha, lakini mwaka 2023 kuna timu nyingine sijui imetoka wapi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia TAMISEMI na Wizara ya Ardhi na Ofisi ya Takwimu walikuja Kiteto kupima vijiji na wakatengeneza ripoti inayoitwa ya kuhakiki vijiji na wakatengeneza ramani ya vijiji ikiwemo Kijiji hiki cha Ilkiushbor na ramani zake ziko hapa na wanakijiji wameambiwa njooni tumeshahakiki hii ni ramani yenu, lakini sasa mwezi Julai, 2023 wametengeneza ramani nyingine na tunaambiwa wanakubali Mkungunero haiko Manyara. Sasa *dispute* iliyopo ni mpaka kati ya Manyara na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kwa wiki nzima sasa wapo Polisi wanaotoka Kondoa, Dodoma wamepiga kambi kwenye hiki kijiji na kuongeza *harassments* ambazo hazina maana.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu huu mgogoro ni wa muda mrefu na nimezungumza kwenye hotuba ya Wizara ya Ardhi hapa, nimezungumza wakati wa hotuba ya Maliasili.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hotuba ya Wizara ya Maliasili ukurasa wa 37, huu mgogoro unaozungumzwa hapa inasema hivi na nanukuu; "Mamlaka imelipa fidia ya shilingi milioni 348 kwa Vijiji vya Ndaja, Keikei na Kitongoji cha Kagera, Msumbiji, Kisondoko" zote ziko Kondoa, lakini sasa *harassment* inayoendelea, kinachosemwa na uhalisia hakuna kinachoendelea, lakini wana-*harass* wananchi wangu na vitongoji.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa *GN* ya TAMISEMI, hiki Kijiji ninachosema cha Ilkiushbor vitongoji vyake viko hapa. Ina vitongoji vya Lombenek, Imbopom, Oslei, Durah, Armame kwa mujibu wa Tangazo la Serikali, lakini *harassment* inayoendelea ni *as if* hivyo sio vitongoji, kama walikuwa na *intention* ya ku-*convert* ardhi ya kijiji kwenda kwenye hifadhi, *process* ni nyingine kabisa, sasa *harassments* zinazoendelea *they are hurting me big time*.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa nimeshazungumza hapa mara kadhaa na karibu nimeshaenda kwa kila mtu, ninaomba sasa uingilie kati kama Mheshimiwa Spika, utupe tutoe hoja tuanze kuzungumza hii hapa, kwa sababu leo ni siku ya mwisho

wa Bunge na tunapoelekea sasa hizo *harassments* sitaki ziendelee.

Mheshimiwa Spika, kama ni suala la uhifadhi tangu mwaka 2006, sisi tumeanzisha *WMA* ya Makami kwa hiyo kama ni mambo ya hifadhi ni Makami, kama ni mambo ya uwekezaji Wizara hii ya Maliasili na Utalii ambayo ndiyo inapanga vitalu vya watalii walitengeneza ramani na kuipa mamlaka *WMA* kuanzisha vitalu na kuwapa wawekezaji. Kwa hiyo kama ni uhifadhi tumeanzisha, kama ni mwekezaji yupo wa *WMA*. Sasa inaonekana wao wamepata mwekezaji wao mwingine huko Mkungunero ambalo ni pori lao, lakini sasa isiwe sababu ya kufanya na ku-*harass* wananchi wangu na mwekezaji ambaye pia yuko huko. Hii nchi tunataka watalii wafike milioni tano, mwekezaji aliyepo *WMA* na aliyepo kwenye mapori ya Serikali ni *the same*. Tutakuwa tunajidanganya sana kama tunafikiri ukiwa-*harass* wawekezaji na wananchi walioko huku basi utakuwa unajenga wa kwako.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa haya na mbali na haya, mimi hiki kijiji mwaka 1998 miaka 26 iliyopita nimechunga kwenye hivi vitongoji ambao wao wanafikiri kwamba vimeanza jana tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakuomba kwa heshima kubwa sana, uniruhusu nitoe hoja ili Waheshimiwa Wabunge tuzungumze kuhusu suala hili, tupate suluhu kwa wananchi wasiwe *harassed all the time. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hoja bado haijatolewa. Mheshimiwa Olelekaita, umesema umeshawaona viongozi ama sijasikia vizuri, umesema umeshaenda sehemu nyingi.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nimesema wakati nachangia bajeti zote mbili za Wizara ya Maliasili na Utalii nimezungumza habari ya hii hoja. *In fact,* nimepata pia mazungumzo *one on one* na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Mheshimiwa Waziri Angellah Kairuki wakati akiwa na mpango wa kukutana na Wabunge wa Mikoa nanime-*raise the same thing…*

**SPIKA:** Na halijafanyiwa kazi?

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, halifanyiwi kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, kwanza.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Edward Olelekaita kwa jambo alililoliwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba upo mgogoro wa mpaka baina ya Wilaya ya Kondoa na Wilaya ya Kiteto nani mpaka wa Mkoa baina ya Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Manyara na katika maazimio ya Baraza la Mawaziri ya Vijiji 975 ambao sasa imefika 1004, mgogoro huu ulikuwa ni mmoja kati ya migogoro kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Kamati ya Mawaziri nane wa Kisekta ikiongozwa na Wizara ya Ardhi ilifika na utaratibu, utekelezaji wa kazi ile ya kuhakiki mpaka hufanywa na timu ya wataalam inayosimamiwa na Kamati za Usalama za Mikoa. Taarifa tulizonazo ambazo na Mheshimiwa Mbunge tulimwasilishia ni kwamba mpaka kufikia mwezi Julai, 2023 Kamati za Usalama za Mikoa hii miwili zilikwisha kuketi. Kamati za Usalama za Wilaya ya Kondoa na Kiteto zilikaa na mwezi Agosti, 2023 waliweka vigingi vya kuhakiki mpaka. Kijiji cha Ilkiushbor kipo, lakini sehemu yake imeingia kwenye Pori la Mkungunero ambalo lipo kwenye Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, kwa kauli aliyoongea Mheshimiwa Mbunge, nikuombe tukutane na Mheshimiwa Mbunge, lakini kwa kuwa tunayo maelekezo ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuondosha taharuki kwenye mambo yote yanayohusu wananchi, nikuombe tupate muda tuangalie hicho kinachotekelezwa huko kwenye Kijiji cha Ilkiushbor kama kinaendana na yale maelekezo ya Kamati ya Mawaziri nane, halafu naamini tutapata suluhu ya tatizo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kijiji kimeanzishwa mwaka 1989, Pori la Mkungunero limeanzishwa mwaka 1996. Katika maelezo yako unasema sehemu ya kijiji imeingia kwenye pori, sasa kimeingiaje wakati kijiji kilitangulia kabla ya pori? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yaani nani ameingia kwa mwezie kwa sababu kama ni Serikali inahitaji hiyo sehemu ya kijiji haiwezi kusema kimeingia ni kwamba ifuate utaratibu inahitaji hilo eneo labda ni muhimu kwa ikolojia, kwa nini si mambo hayo yanafanyika? Yaani kwa nini hii hoja kijiji kimetangulia, hili Pori la Mkungunero limefuata, sasa kidogo sijaelewa kwenye hilo eneo tu. Kwa maana ya ninyi kupewa muda Mheshimiwa Mbunge amesema ameshaonana nanyi. Kwa hiyo, mnahitaji muda gani ili wananchi kule, Mheshimiwa Rais alishaenda kule, Mawaziri nane walishaenda kule na ninyi wawili ameshawaona?

Mheshimiwa Waziri ukisema kijiji kimeingia unakusudia kusema pori linahitaji sehemu ya hicho kijiji maana kilichotangulia kwa takwimu zilizooneshwa hapa ni kwamba kijiji kilianzishwa kabla ya pori.

Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, karibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, hakuna ubishi kwamba Kijiji cha Ilkiushbor kimeanzishwa mwaka 1989 na hakuna ubishani kwamba Pori la Mkungunero limeanzishwa mwaka 1996, lakini ndio maana unaitwa mgogoro. Hata kwenye makazi yetu tunayoishi majirani wawili wanaweza wakawa na mgogoro wa mpaka baina ya *plot* moja na *plot* nyingine na zote zipo.

Mheshimiwa Spika, *issue* iliyopo ambayo na wewe umeielezea kwa namna yake ni kwamba uhakiki wa mpaka wa hiki Kijiji cha Ilkiushbor kilichoanzishwa mwaka 1989 ni upi na hili Pori la Mkungunero lililoanzishwa mwaka 1996 ni upi kwa sababu yako maeneo mengi kijiji kipo, lakini kutokana na shughuli za kiuchumi na kijamii na ongezeko la watu kijiji kimejikuta kimeingia kwenye hifadhi na ndio msingi mzima wa migogoro 975 ambavyo

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amemega zaidi ya hekari milioni 2.4 kwenye hifadhi, mapori ya hifadhi, mapori tengefu na kurejesha kwa wananchi.

Kwa hiyo, hoja iliyoko hapa ni hoja ya Kijiji cha Ilkiushbor kinakomea wapi na hoja ya Pori la Mkungunero linaishia wapi na ndio jambo ambalo tumeomba muda wa kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ukiwa bado uko hapo, Mheshimiwa vigingi vilivyotajwa vimewekwa nje au ndani ya kijiji?

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nje kabisa, unajua…

**SPIKA:** Ni nje ya kijiji?

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, hapana, yaani ndani kabisa, yaani *in fact* mgogoro…

**SPIKA:** Ngoja, vigingi vimeingizwa ndani ya kijiji kwa hiyo vimeondoa eneo la kijiji…

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ndani yaani ambayo inaweza ikachukua vitongoji viwili, inachukua shule ya wananchi, inachukua visima karibu 20.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana, umeeleweka. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, sijui kama nimemsikia vizuri, nilitamani sana kujua hilo jina la Kijiji ni Ilkiushbor au ni tofauti.

**SPIKA:** Orkush..., hebu…

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, sasa unajua lafudhi tutapishana hapa, nikitamka Kimasai kabisa kwa sababu ni jina la Kimasai kinaitwa Ilkiushbor, lakini kama ni Kiswahili

anielewe wakili hapa ni Ilkiushbor ndio mnachosema ninyi huko. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nilitaka ili ninavyojibu nijue kama ndio ninachokijua kiko sawa au laa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulikaa na Mheshimiwa Mbunge nilivyokuwa nafanya vikao na Wabunge wa Mikoa mbalimbali na baada ya kumsikiliza kuanzia tarehe 4 Aprili tulianza vikao na uongozi wa Wilaya za Kondoa, Kiteto na kwingineko na kama nitakuwa nimemuelewa vizuri, pia atakuwa labda anamaanisha mwekezaji ni *Sunset*, ni sahihi?

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumza sasa hivi na wenyewe tuna kesi tumemfungulia *Sunset* Mahakamani kwa sababu kuna eneo pia alikuwa ameingia kidogo katika eneo la hifadhi ambalo pia sasa hivi yupo mwekezaji kupitia uwekezaji wa *SWIECA*, kupitia mwekezaji Mark Ellan lakini tayari mashauriano yalishafanyika kuanzia mwezi wa tano na hata mwezi huu wa sita mpaka tarehe 11 Juni kulikuwa na mashauriano na tayari alishaelekezwa ahamishe baadhi ya miundombinu na uwekezaji alioufanya katika kambi zake mbalimbali katika hifadhi yetu na kuna kesi Mahakamani tumemfungulia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, mwekezaji sio sehemu ya huu mgogoro tunaojadili kwa sasa, sio sehemu. *(Makofi)*

Mgogoro uliopo ni mpaka wa hilo Pori la Mkungunero unaishia wapi wakati mipaka ya kijiji inaonekana ipo mpaka mahali. Sasa pori limeanzishwa limechukua na eneo la kijiji wakati kijiji kina ramani yake, ndiyo hoja. Hii ya mwekezaji nadhani itakuwa ngazi nyingine ila kwa ngazi hii ya sasa ni hii ya mpaka.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye hilo mpaka ni kama alivyoeleza Mheshimiwa Jerry Silaa, kwa sababu kwenye Kamati ya Mawaziri nane tunafanya wote kwa pamoja na hata kupitia uongozi wa mkoa kama alivyoeleza tangu mwezi wa nane tayari vigingi vilishawekwa na mpaka

ulishahakikiwa ili kuonesha wapi ni mpaka wa hifadhi na wapi inatakiwa vijiji viweze kuishia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Sasa Serikali mwaka 2022 Mawaziri nane mmekwenda Novemba mkasema kijiji kinabaki. Mmekwenda baadaye mwaka 2023 timu nyingine mmeunda, ramani mmetengeneza mpya na mnasema tena vitongoji vinaondoka. Sasa mwaka 2022 Rais alikuwepo pale, sasa saa hizi inabidi aende nani ili usemwe ukweli yaani kwamba mpaka utakuwa wapi? Maana wanakijiji wameambiwa mbele ya Rais. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi amesema wanaomba muda na wewe sababu umekwishalileta hapa Bungeni, kwa kawaida Waheshimiwa Wabunge tukilijadili hili kama suala la dharura ni kwamba limeshindikana katika njia zile za kawaida na kwa kweli alipofikia Mbunge ni kwamba amefuata hizo hatua zote na bado wananchi wananyanyaswa. *(Makofi)*

Sasa ili na sisi tuweze kulijadili vizuri ni pamoja na kuipa Serikali muda, kwa namna alivyoelezea Mbunge vilevile na wao wajielekeze hivyo hivyo kwamba, Serikali imekwenda ikakipa usajili kijiji mwaka 1989, ikaja mwaka 1999 ikaanzisha pori kijiji bado kipo. Baadaye mwaka 2020 na ngapi migogoro ikaanza. Mwaka 2022 Serikali yenyewe na Mawaziri nane imesema kijiji kinabaki, baadaye imekuja kusema mbele ya Rais akiwa Manyara kwamba kijiji kinabaki. Sasa hayo yote mkishajiridhisha na pale mahali ambapo mmeweka vigingi, mwezi wa tisa *In sha Allah* Mwenyezi Mungu atakapotuleta hapa Bungeni taarifa hii muwe nayo tayari ili Bunge sasa liweze kufanya maamuzi hapa, ikiwa hilo jambo litakuwa bado limeshindikana mpaka hapo, Bunge litaazimia nini Serikali sasa ikafanye, lakini kwa sasa maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Mbunge yanajitosheleza. Serikali kaangalieni mfuatano wa hayo mambo mjione na ninyi mko sehemu gani. Pia mmesema vizuri kwamba Mheshimiwa Rais migogoro ya ardhi hataki na amewapa maelekezo maalumu kuhusu hilo eneo. Hakuna sababu ya kuanzisha mgogoro ambao ulikuwa haupo. Kama eneo linahitajika fuateni tu utaratibu kwa sababu sheria za

nchi hii ziko wazi. Kama mnalihitaji fuateni utaratibu wa kulihitaji na msitengeneze mgogoro mahali ambapo hapapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge naona umesimama.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa jinsi ulivyo *approach*. Sasa kwa sababu ya kuondoa taharuki ambayo Mheshimiwa Rais haitaki, walazimishe watoe mapolisi waondoke ili maisha yaendelee wakati wanafanya hiyo kazi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kweli, sasa kwa sababu hawa walioitwa mapolisi nataka kuamini ni wale wa uhifadhi. Ni mapolisi wale wa kawaida au wale wa uhifadhi?

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, *in fact* wamechanganyikana wale wa hifadhi eti na wa Kondoa wanaotoka Dodoma. Wanasema eti lile ni eneo letu, sasa wanaleta taharuki ambayo haina maana. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mbunge hapa ametoa maelezo ambayo sote tumemuelewa na mimi nimetoa maelezo ambayo Serikali inapaswa kwenda kuyafanyia kazi ili Bunge kama kutakuwa na ulazima tutalishughulikia jambo hili Bunge lijalo ili kuipa nafasi Serikali kwa ajili ya kufanya mambo haya Kiserikali, lakini sasa kwa hili alilolisema hapa mwisho alikuwa amelisema mwanzo lakini sasa limesemwa kwa sura ambayo kwa kweli itakuwa haipendezi kama tumesikia kwamba kuna wananchi wananyanyaswa halafu bado wakaendelea kunyanyaswa.

Sasa kwa sababu Serikali tumewapa muda wa kulifanyia kazi hili jambo na ninyi maana yake mpaka sasa bado hakuna maamuzi ndiyo maana neno mgogoro limejitokeza. Kwa sababu hili eneo bado liko katika huo mgogoro, basi hao polisi wapishe kipindi hiki ambacho tunasubiri mwezi wa tisa mpaka Bunge litakapokuwa limejadili jambo hili kwa kina ili tuwe tumeelewana ni maamuzi gani ambayo mtakwenda nayo upande wa Serikali, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea baada ya kusikiliza hilo. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria zinazohusu Ulinzi wa Watoto *(The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa *(The Prevention and Combating of Corruption (Amendments) Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, miswada minne imekwisha somwa kwa mara ya kwanza. Baada ya hatua hiyo Kanuni ya 97(1) inanipa mamlaka ya kuelekeza miswada hii kwenye Kamati na sasa Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa mwaka 2024 utakwenda Kamati ya Miundombinu; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 2, Bill 2024)* utapelekwa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Zinazohusu Ulinzi wa Watoto *(The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill 2024)* utapelekwa Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa *(The Prevention and Combuting of Corruption (Amendments) Bill 2024)* utapelekwa kwenye Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024**
***(The Finance Bill 2024)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana tulikuwa tumemaliza kwa sehemu kwa maana uchangiaji kutoka kwenu na ilikuwa

Mheshimiwa Waziri bado kuhitimisha, kwa maelezo niliyoyatoa jana nisiyarejee leo, lakini katika maelezo yale nilisema ninaweza kumpa nafasi Mwenyekiti wa Kamati kama kutakuwa na sababu ama kuna mambo ambayo pengine Mheshimiwa Waziri ameyapeleka na Mheshimiwa Mwenyekiti angependa kulijulisha Bunge, nitoe nafasi hiyo na kama yote mmekubaliana ama kuna ambayo hamjakubaliana na Waziri atayasema yote basi nakupa nafasi hiyo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Oran Manase Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na jana tulikaa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na tulipitia maeneo yote. Napenda kulifahamisha Bunge kuwa yote ambayo tulikuwa tumeelekezwa kuyafanyia kazi tulikubaliana na yale machache ambayo hatukukubaliana ambayo ni machache sana yako kwenye *schedule of amendments.*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo hayo aliyoyatoa Mheshimiwa Mwenyekiti maana yake yale marekebisho ambayo yatakuwa yameletwa na Serikali wamekubaliana na upande wa Kamati.

Sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Fedha aje ahitimishe hoja inayohusu muswada huu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema na kutujalia rehema za kukutana tena kwenye hoja hii.

Mheshimiwa Spika, pili, nikushukuru wewe mwenyewe kwa moyo wangu wa dhati kwa kuwezesha majadiliano kuhusu

Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2024/2025 kufanyika vizuri na tatu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa maoni na ushauri wao walioutoa katika majadiliano ya muswada huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutambua michango yote ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala wa muswada huu. Naahidi kwa niaba ya Serikali kwamba tutafanyia kazi yale maelekezo ambayo Bunge lako Tukufu limetoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijafafanua hoja napenda nitumie Bunge lako hili Tukufu kuwahakikishia Watanzania kwamba wana Serikali makini sana inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambayo inajali sana maslahi ya Watanzania na ndiyo maana umeona tumekuwa na mjadala wa kina sana kuhusu sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imesikiliza kwa kiwango kikubwa sana ushauri wa Wabunge na imesikiliza kwa kina sana ushauri wa wadau wa shughuli za maendeleo ambao walifika katika Kamati na katika majadiliano Kamati ime-*share* na sisi na Kamati inafanya kazi kwa niaba ya Bunge zima, kwa hiyo, wadau wamesikilizwa kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, niseme sambamba pia na kuwafahamisha Watanzania kuwa wana Bunge moja makini sana ambalo linajali sana maslahi mapana ya Watanzania. Unaweza kuona jinsi ambavyo Wabunge wanafuatilia kwa umakini sana masuala yote ya utungaji wa sheria na hiyo yote ni kwa ajili ya kuwatendea haki Watanzania ambao wamewatuma kuja hapa.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo nianze kwa kuelezea hoja ambazo zilichukua nafasi kubwa sana katika mjadala.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ambalo limechukua nafasi kubwa na pamoja na kwamba limelezewa kwenye Wizara za Kisekta, napenda na mimi kuongezea ni lile lililokuwa linahusu mabadiliko kwenye masuala ya sukari.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya ya Sheria ya Sukari tunayoyaleta yanalenga kujenga msingi imara wa kulinda Uchumi wetu dhidi ya mitikisiko katika Uchumi kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Spika, mimi niliwahi kupata bahati ya kuwa Waziri wa Kilimo, natambua hili jambo ambalo tumekuwa tukilijadili hapa. Tumewahi kujaribu mbinu mbalimbali za kushughulikia jambo hili, tumewahi kuwaamini wafanyabiashara, tukawapa wafanye shughuli hii, yalijitokeza matatizo na sote tunajua. Tuliwahi pia kuwaamini wazalishaji tukawapa shughuli hii ya kuagiza sukari, wote na wenyewe pia matatizo yalijitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa Taifa ambalo limeshafikisha zaidi ya miaka 60 yaani umri wa mtu mzima kuwa tunafika wakati tunakuwa na sukari inayotosha wiki moja, wiki mbili ni mambo ambayo hayakubaliki kwa Taifa lenye heshima kama Tanzania, kwa maana hiyo, Serikali inachukua jukumu hili la kuhakikisha upatikanaji wa sukari kwa Watanzania wakati wa upungufu linafanywa ipasavyo na Serikali na litafanywa hivyo wakati wa upungufu na litafanywa hivyo wakati wa muda wote kama tunavyofanya katika bidhaa nyingine na jambo hili tunaamini kwamba litakwenda kuiondoa nchi yetu kuwa kwenye mashaka na hii tumefanya katika mazao mengine na tumeweza.

Mheshimiwa Spika, sheria hii itasimamia vizuri bei za mlaji kuanzia kutoka kwa mzalishaji na kwenda kwa mlaji na hii itafanywa kwa wazalishaji kukokotoa gharama zao vizuri. Hivi tunavyoongea Bodi ya Sukari imekuwa ikifanya utafiti wa aina hii, imekuwa ikikokotoa bei za sukari na imekwishakokotoa kwa mfano katika muda huu ambapo masuala haya yalikuwa yananendelea sisi Serikali tumejiridhisha sana kutaka kujua undani wa masuala haya.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano bei ya jumla kama bodi ilivyokokotoa kutoka kiwandani bila *VAT* ni kama shilingi 95,000. Ukiweka *VAT* tunatarajia 18% iwe kama shilingi 112,000 na hii ni bei ya jumla ambayo ingeweza kufikisha kama shilingi 115,000 kwa mfuko moja wa kilo 50, lakini utaona katika mazingira tuliyokuwa nayo kwa *calculation* kwa upande wa wazalishaji tulikuwa

tunaona kwamba wanaweka bei ambayo ilikuwa inatoka kwenye shilingi 122,000 na shilingi 125,000 mpaka shilingi 130,000.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya kazi hizi zote sambamba na Serikali ya Awamu ya Sita imefanya jukumu hili kikamilifu sana. Jukumu la kwanza la kuhakikisha tunaendeleza uzalishaji ili tuweze kujitegemea. Jukumu hili Serikali imelifanya kikamilifu na hata wazalishaji wenyewe wakiulizwa watakuwa mashahidi kwamba kuna *incentives* ambazo wamezifukuzia kwa zaidi ya miaka kumi walikuwa hawajazipata, lakini Rais amefanya ziara kwenye maeneo haya na akaelekeza jambo hili likamilike. Wamepata *incentives* zote zile ambazo kwa nchi hizi za Afrika Mashariki na Kati na ukanda wa *SADC* hamna *incentives* kama hizo zimetolewa kwa wazlishaji wa sekta hii.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, Serikali inajali sana wazalishaji na imetoa *incentives* ambazo ni kubwa mno na hamna mtu ambaye anaweza akatoa *excuse* yoyote ya kutokuzalisha.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali ina wajibu wa kuwalinda wananchi wake na kuwalinda walaji, wajibu huo ni lazima ufanywe na Serikali na hicho ndicho ambacho imekuwa ikifanya na nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Sekta Ndugu yangu Hussein Bashe kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapokwenda tutashirikiana na sekta zote za Serikali ambazo zinaguswa na jambo hili, tutaweka *ETS* kuweza kujua kwamba hadi inafika kwenye uzalishaji ni kiasi gani kimezalishwa na kimezalishwa kwa gharama gani.

Mheshimiwa Spika, tumefanya uwekezaji ambao unatosheleza kuwa Taifa makini ambalo linalenga kuhakikisha kwamba uzalishaji wa bidhaa hii muhimu tunajitosheleza.

Mheshimiwa Spika, siyo jambo jema sana kubishana kuhusu na ulaji, *trading*, tunatakiwa tujadiliane na tutumie muda mwingi kuhusu kuzalisha ili tujitosheleze. Hii habari ya watu kugombania

faida na kila mtu anataka kwa manufaa yake yeye mwenyewe aagize, afanye biashara, apate faida, bila kumjali mlaji, hili siyo jambo ambalo Serikali inatakiwa kulifumbia macho. Tutawekeza kama ambavyo tumeshafanya na tutalinda walaji/watumiaji wa bidhaa hii ambao ni Watanzania ili waweze kupata bidhaa hii kwa upatikanaji ambao hauna mashaka, lakini pia kwa bei ambayo wanaweza wakaimudu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limeongelewa ni kuhusu jambo la *ethanol*. Tofauti na ambavyo imejadiliwa kwamba tumepandisha bei, hatujapandisha bei badala yake tumebadilisha utozaji, ilivyokuwa mwanzo bidhaa hii kwa Tanzania hapa kwenye upande wa *ethanol* tulikuwa hatutozi, tulikuwa tunatoza kwenye *spirit*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tulikuwa hatutozi kwenye *ethanol* tumegundua pana mianya mingi baada ya kuwa tumetoka kwenye *ethanol* imekwenda kwenye *spirit* ambapo tunapokwenda kutoza kwenye *spirit* tunakuwa tumepata upotevu wa mapato huku mwanzo kwa sabau bidhaa yenyewe kwanza ina matumizi mengi, lakini pia mtiririko wake haujanyooka sana kwa sababu mnajua matumizi haya na namna ambavyo inakwenda kubadilishwa kwenda kwenye *spirit*.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo la kwanza ambalo tumefanya, tumeoanisha utozaji wa kodi hii sambamba na nchi nyingine za jirani, kwa mfano ukifanya kwa *conversion* ambayo inapeleka kodi ambayo inatolewa kwa fedha za Kitanzania, wakati sisi hatutozi Kenya walikuwa wanatoza 5,000 ukibadilisha ikawa kwenye shilingi ya Kitanzania. Wakati Tanzania ikiwa *zero* Kenya ilikuwa 5,000 na Uganda ilikuwa 5,000, sisi tulikuwa tunatoza tu kwenye *spirit (final product)*.

Mheshimiwa Spika, uzoefu umeonesha hapa katikati kunakuwa na upotevu mkubwa sana na ndiyo maana tumeona tufanye kama *advance tax,* ije mwanzoni hapa na kwa wale ambao watakwenda kutengenezea zile *spirit* maana yake wata-*account* kwanza ile *advance tax* ambayo ilishatolewa, kwa maana hiyo hakutakuwepo na *burden* kwa yule ambaya anauza

ile *raw material.* Kwa hiyo, hii tumeitengeneza na wenzetu ndivyo wanavyofanya.

Kwa hiyo, kwa ile ambayo inatozwa ndani ya nchi inayotokana ndani ya nchi tumeiwekea ushuru unaolingana na nchi nyingine majirani wa Afrika Mashariki lakini kwa ile ambayo inatoka nje ndio ambayo tumeiongezea kidogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali tumekubaliana na Kamati kwenye mizigo ambayo imeshaagizwa kabla ya sheria hii mpya kutungwa itatozwa kwa utaratibu wa zamani ambao waliagiza mizigo kabla hawajajua kwamba kutakuwepo na sheria hii. Kwa hiyo, mizigo yote ile itakuwa na *bill of landing,* itakuwa na taarifa ambazo zinaonesha imeagizwa lini tutafanya utaratibu wa kiutawala kuweza kuhakikisha kwamba hatuwakwamishi vijana wale ambao wanafanya shughuli hiyo na jambo la aina hii liliwahi kufanyika kwenye masuala ya vitenge, tulivyobadilisha sheria, mizigo ambayo ilikuwa imeshaagzwa tulitumia utaratibu ambao ulikuwa unatumika kabla ya sheria mpya kupitishwa ili kuweza kuhakikisha kwamba hatuwasababishii hasara wale ambao walikuwa wameshaagiza.

Mheshimiwa Spika, nikuombe pamoja na Bunge lako Tukufu kwenye jambo hili tukubaliane na Serikali kwa sababu tunalenga tu kutenda haki ya kuhakikisha kwamba mapato hayapotei kwa sababu wale ambao wamekuwa wakitozwa kodi hii na wengine wakiwa hawajatozwa hii ilikuwa inatengeneza *imbalance* kwenye *field* ya pamoja ya kufanyia biashara.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo lilikuwa limependekezwa na Waheshimiwa Wabunge aliisemea Ndugu yetu Kandege ni kuhusu fedha zinazotokana na tozo ya maendeleo ya viwanda, ushauri huo umepokelewa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililetwa na Kamati ya Bunge ambalo lilikuwa linaongelea kuongeza huduma ya zenye sura ya taasisi hisani kama vile huduma za kisheria na kuongeza upatikanaji wa huduma hizo kwa wingi kwa mujibu wa kifungu cha sheria cha 64(8) cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura Namba

332 vigezo vya taasisi kutambuliwa kuwa ni taasisi hisani vimejumuisha shughuli zenye malengo ya kuondoa umaskini na tumezingatia ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, upande wa Kamati pia waliongelea kuhusu kutoa ufafanuzi wa *low interest rate,* tumeisemea ile kwa kirefu tulipokuwa kwenye Kamati ya bajeti. Pia Kamati ya Bajeti pamoja na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha waliongelea kuhusu Serikali kuondoa kodi kwenye vifaa vya vinavyotumika kuunganisha mifumo ya gesi, ushauri huo umepokelewa na tumeweza kujibu wakati tunashauriana na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Bajeti pamoja na Wabunge wengine wote ambao wameongelea masuala haya ya gesi, natambua Mheshimiwa Profesa Manya, Mheshimiwa Esther Matiko pamoja na Wabunge wengine wote ambao tumeliongelea hilo tumelipokea na ninadhani mmeona kwamba, tumeweza kufanya ule uamuzi. Kamati ya Bajeti pia, imesema Serikali ifanye tathmini ya hatua za kikodi zitakazotekelezwa katika kila Mwaka wa Fedha, ili kujua athari hasi pamoja na chanya na kubaini malengo yaliyokuwa yamekusudiwa. Huu ni ushauri mzuri, tumeupokea na tumesema tutaufanyia kazi kama ambavyo imekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Charles Kimei, Abbas Tarimba, Nusrat Hanje na wengine wameongelea kuhusu Serikali, iangalie uwezekano wa kuwasilisha Bungeni Sheria ya Fedha mapema, ili kutoa muda kwa kamati kufanyia kazi vya kutosha uchambuzi na mapendekezo; ushauri huu umepokelewa. Tutaendelea ku-*engage* na kamati, ili kuona njia bora zaidi ya kuweza kutekeleza ushauri huo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ameongelea kuhusu kufuta pendekezo la kutekeleza asilimia mbili pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wengi ambao wameongelea jambo hili; jambo hili limepokelewa. Pendekezo hili limepokelewa na Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali sikivu ambayo inatambua mchango

wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge, kama wawakilishi wa wananchi, imepokea pendekezo hilo na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Reuben Kwagilwa ameelezea kuhusu Serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza ushuru wa forodha kwenye chumvi ghafi inayotambuliwa kwa *Heading* 25(01); ushauri umepokelewa na jambo hili limefanyiwa kazi. Tumekubaliana na maoni ambayo ameyatoa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Priscus Tarimo ameongelea kuhusu utaratibu wa ukadiriaji wa kodi kwenye magari utumike katika bidhaa zote; ushauri wa Mheshimiwa Mbunge umepolewa na utafanyiwa tathmini kwa kina. Tutakapoendelea kufanya *engagement* na Waheshimiwa Wabunge tutakuwa tunaelezea utekelezaji wake umefikia hatua gani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi amesemea kuhusu Serikali ifute pendekezo la kutoza shilingi 382 kwa kilo kwenye gesi, nimesema na Wabunge wengine wengi ambao wameisemea hii hapa; ushauri umepokelewa na umefanyiwa kazi. Nakumbuka Wabunge wengi, orodha yao ni ndefu naomba iingie kwenye kumbukumbu ya *Hansard*, wote wameongelea masuala haya ambayo yanawatetea wananchi. Serikali imezingatia na imeweka jedwali la mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Timotheo Mnzava pamoja na Mheshimiwa Ahmed Juma wameongea kuhusu suala la Wizara ya Ardhi ipewe jukumu la kukusanya kodi ya ardhi; Wizara ya Ardhi inakasimiwa jukumu la kukusanya kodi ya ardhi kwa mujibu wa Sheria. Aidha, marekebisho yaliyofanyika katika Kifungu cha 33(a) cha Sheria ya Ardhi, Sura Namba 113, kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2003, imeruhusu makusanyo hayo yaende kwenye Mfuko Mkuu na vilevile pendekezo la kurekebisha Kifungu cha 33(a) cha Sheria hiyo kupitia Muswada wa Fedha wa Mwaka 2024 inaruhusu mgawanyo wa mapato na 20% isalie.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba, kwenye eneo hili bado tuna kazi ya kufanya. Tumeongea na Waziri wa kisekta

pamoja na Naibu wake kwamba, tuna kazi ya kufanya. Tutaendelea kulifanyia kazi jambo hili na kama tutakuwa hatujalikamilisha kimamilifu kwa wakati huu tunaomba Waheshimiwa Wabunge mridhie kwamba, tutalifanyia kazi pamoja na wizara ya kisekta, ili kuweza kuhakikisha kwamba kule tunakokwenda tunakuwa na *consensus*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Musukuma amesema Serikali iangalie na ihakikishe kiasi cha madini ya dhahabu kinachonunuliwa na Benki Kuu ya Tanzania, kwa ajili ya kuongeza akiba ya fedha za kigeni, kinasafishwa na viwanda vya kusafisha dhahabu hapa nchini; ushauri umepokelewa. Mheshimiwa Waziri wa kisekta jana aliliongelea vizuri jambo hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nusrat Hanje pia, ameongelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji na kitengo cha tafiti kwa masuala ya kikodi; Mheshimiwa Nusrat jambo hili limepokelewa, ushauri umepokelewa na Serikali inaendelea na utaratibu wa kujenga mifumo ya kodi. Tunajenga mifumo ya kodi za ndani, tunajenga mifumo ya kodi za forodha pamoja na haya mengine yote ambayo yatalenga ku-*harmonize* masuala yanayohusiana na makusanyo, ili kuondoa usumbufu ambao unatokana na masuala ya utawala wa kikodi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika ameongelea Serikali iongeze ushuru wa forodha kwenye bidhaa ya *liquid glucose* kwa lengo la kulinda wazalishaji; ushauri umepokelewa. Tathmini ya kina ya kujiridhisha uwezo wa uzalishaji pamoja na mahitaji utaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohamed Said Issa alimesema Serikali iangalie uzoefu wa nchi nyingine kuhusu utaratibu unaotumika katika kuhamasisha wananchi na wafanyabiashara kudai na kutoa risiti; Mheshimiwa Mbunge tumepokea ushauri huu. Tunaamini baada ya hoja hii ambayo imejadiliwa kwa kina sana na Waheshimiwa Wabunge, ya kwenda kwenye *cashless economy,* tukifika huko tukaanza kutumia masuala ya kidigitali tunaamini pia, masuala haya ya utoaji wa risiti yatafanyika kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunakokwenda tunapanga kuangalia *incentives* za kuweza ku-*motivate* wale ambao wanafanya malipo ya kidigitali tuweze kuwatofautisha na wale ambao wanafanya malipo kwa *cash* yote hii inalenga kurahisisha utaratibu huu. Nchi zote ambazo zimeemdelea zilishavuka habari ya kujadiliana kuhusu kutoa risiti ama kutokutoa risiti. *Transaction* zote zinazofanyika wanatoa risiti za kielektroniki kwa hiyo, na sisi tunaelekea huko tutaendelea kutoa hiyo elimu tunaendelea kutoa hiyo hamasa.

Mheshimiwa Spika, nawakumbusha tu Watanzania, pale unapolipia bidhaa unalipa na kodi, lakini usipodai risiti kodi yako inakwenda kwa mtu binafsi. Kodi hii inapoenda kwa mtu binafsi ndio tunatengeneza pengo la walionacho na wasia nacho kwa sababu, panatokea mtu katikati hapa anakusanya kodi kwa niaba ya Serikali kwa fedha ambayo haitumii kwa kurejesha jambo lolote la maendeleo kwa wananchi ambao amechukua fedha yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natoa rai kwa Watanzania wote wawe na wivu na fedha wanayoitoa kwamba, ni lazima iende kufanya shughuli za maendeleo. Usiachilie tu kwamba, bora limeenda ukamuachia mtu binafsi ambaye hatahusika kujenga madarasa, hatahusika kujenga kukuletea barabara iliyo njema, hatahusika kuleta maji na wala hatahusika kufanya shughuli nyingine za maendeleo. Ni bora fedha ambayo imetoka kwako, kama kodi, hakikisha inakwenda Serikalini, ili uidai Serikali maendeleo na uiwajibishe Serikali kuhakikisha kwamba, inakupatia maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tunaona hii huwa inatokea. Mtu anakuwa hauhusiki kabisa na masuala haya, yuko mbele ya duka ama yuko sokoni, hahusiki kabisa na masuala ya kutoa ama hakudai risiti ambayo hiyo ndiyo inatakiwa ifanye shughuli za maendeleo, lakini pia, anashiriki kulalamika kwamba, hapa hakuna lami wala zege, mbele ya eneo lile analohusika. Kwa hiyo, ni lazima tuhusianishe maendeleo na kodi unayolipa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge amesema Serikali ihakikishe upatikanaji wa chanzo cha uhakika, kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara; ushauri huu umepokelewa. Ndio maana tumeleta pendekezo lile la kuhakikisha tunakuwa na mfuko ambao utashughulikia matengenezo ya barabara kwa dharura.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na hoja ambazo zimekuwa zinatolewa kwamba, kwa nini fedha ile isiende kwenye Mfuko wa Barabara moja kwa moja?

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Barabara una chanzo chake. Katika baadhi ya miaka ambayo haina *maintenance* kubwa fedha zile bajeti yake, ilikuwa, inakuwa chini ya fedha zile ambazo zimekusanywa. Mfuko huu tunaosema ni wa dharura *experience* ya majanga haya ambayo yamejitokeza imetupa somo kwamba, tunatakiwa tuwe na fedha ambazo ziko *standby* pale ambapo majanga haya yanajitokeza na barabara zinaharibika.

Mheshimiwa Spika, tukiweka kwenye mfuko wa kawaida upo uwezekano zikatumika kutengeneza barabara, kama ambavyo huwa zinafanyika na pale ambapo panatokea majanga, ikatokea fedha hizo hazipo, tutaingia kwenye matatizo ya kukosekana fedha kama ambavyo imekuwa ikijitokeza. Kwa hiyo, tumeona tuwe na Mfuko wa Dharura kwa maana halisi ya Mfuko wa Dharura wa Barabara kwa sababu, mambo haya yamekuwa yakijitokeza na yanajirudia ndio maana tumeona tufanye namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia, zimekuwepo hoja ambazo nadhani zimetolewa na Mheshimiwa George Mwenisongole kwamba, kwa nini tunawapa *exemption* wazalishaji wa mbolea wa ndani ilihali tunatoa *exemption* na tunatoa tena ruzuku kwenye mbolea?

Mheshimiwa Spika, ili tuwatendee haki wanaowekeza kwenye uzalishaji ndani ya nchi ni lazima na wenyewe tuwapatie *incentives.* Kwa hiyo, tunachofanya si kwamba, mbolea tu, pale tunapotoa unafuu kwenye uingizaji wa mafuta ya kula, tumekuwa pia, tukiwapa motisha wale wanaozalisha mafuta ya kula ndani.

Kwa sababu, tukiwapa nafuu wale wanaoagiza tu kutoka nje tutajenga nchi inayojivunia watu wanaoagiza bidhaa kutoka nje. Tunataka tuwatengenezee mazingira wale waliojitoa wakaamua kujenga kiwanda hapa ndani ya nchi, ni lazima na wenyewe wapate *incentives* za kuwafanya wakamilishe ujenzi wao, wawekeze na waongeze uzalishaji, ili tujitosheleze.

Mheshimiwa Spika, kuagiza bidhaa nje siyo sifa kwa hiyo, hatupaswi kujivunia sana kuwapa *incentives* watu wanaoagiza bidhaa kutoka nje. Tunatakiwa tuwape *incentives* watu wanaojenga kiwanda hapa, wanatengeneza ajira kwa watoto wa Kitanzania hapa, wanapambana kuhakikisha kama ni mbolea inayozalishwa ndani ya nchi inajitosheleza na ikiwezekana iuzwe nje ya nchi. Kwa hiyo, ndio maana tunawapa *incentives* wale wanaozalisha mbolea hapa, tunawapa *incentive* pia, wanaozalisha mafuta ya kula hapa, tunawapa *incentive* pia, wanaozalisha bidhaa nyingine zinazozalishwa hapa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hiyo ndio mantiki na lengo letu. ufike wakati mbolea izalishwe ndani ya nchi na tujitosheleze, ufike wakati mafuta ya kula yazalishwe ndani ya nchi na tujitosheleze, ufike wakati sukari izalishwe ndani ya nchi na tujitosheleze, ufike wakati na bidhaa nyingine ambazo tunaweza kuzizalisha ndani ya nchi tufanye hivyo na tuweze kuhakikisha kwamba, tunajitegemea.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia baadhi ya hizi bidhaa ambazo tumehangaika sana wakati wa *Covid* pamoja na mzozo wa Russia na Ukraine kimsingi sisi, kama Tanzania na nchi nyingi za ukanda huu wa Afrika, tulitakiwa tuilishe Dunia. Ni aibu kwa nchi zetu hizi za Afrika kupata shida ya mafuta ya kula kwa sababu, kuna mzozo wa Russia na Ukraine, wale ndio wanatakiwa watutegemee sisi huku kwa mazingira ambayo tukonayo. Kwa maana hiyo ndio maana Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweka utaratibu wa *export guarantee scheme* ambao unalenga pia, kushughulikia suala la *import substitution,* ili tuweze kuhakikisha kwamba, bidhaa nyingi tunazoweza kuzizalisha hapa tunazizalisha hapa, tunajitosheleza na tunapeleka katika mataifa

mengine; hiyo na yenyewe ni njia ya kuweza kuhakikisha kwamba, tunapata fedha za kigeni na kujitosheleza.

Mheshimiwa Spika, kwenye mabadiliko madogo tuliyofanya pia, tumeweka jambo moja ambalo Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete, ameliongelea sana mwaka jana, linalohusisha masuala ya *unclaimed assets.* Tumeweka kwenye marekebisho na jambo hilo litaenda kujitokeza kwenye na tunatarajia lianze kutumika mara moja katika mwaka huu wa fedha tunaoanza.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa pia, tunajadiliana kwa kirefu na kamati kuhusu *language* ya masuala haya ya utararibu wa matumizi ya dola. Lugha imetusumbuasumbua, lakini tunacholenga ni tutaweka mwongozo ambao Mtanzania hatahangaika wala hatashurutishwa kutafuta dola kulipia bidhaa ndani ya nchi yake, atatumia fedha ya Kitanzania kulipia bidhaa ama huduma anazozipata ndani ya Tanzania lakini hatutaweka masharti ya kuzuia *transaction* ambazo teknolojia imeshakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mtu anaweza akalipa kwa kutumia fedha ya kigeni kama ana *VISA Card*. *Provided* anatumia *VISA Card* au anatumia *Credit Card* haya huwa yanafanyika hata wewe ukienda na Shilingi ya Kitanzania kwenye *bank account* yako ukiwa umesafiri na kadi unaweza ukafanya malipo ukiwa nchi yoyote ile. Kwa hiyo, haya mambo ya kukua kwa teknolojia yote kwenye mwongozo yatazingatiwa, lakini pia, na mazingra mengine ambayo yanaipa nchi faida. Kwa kufanya hivyo, yatazingatiwa katika kanuni na mwongozo utakaotolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, nimeshaona kengele ya kwanza imegongwa, natumia fursa hii tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi kubwa ambayo wameifanya, wamewatendea haki wapigakura wao. Nawatakia safari njema tutakapokuwa tumemaliza shughuli hii kubwa ambayo iliwaweka hapa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya nawaomba Waheshimiwa Wabunge tena waridhie, kama walivyofanya juzi, wapitishe Muswada huu kwa kishindo, kwa kihistoria kwa sababu, tunatunga Sheria ya kuwawezesha Watanzania kuweza kufanya kazi vizuri na kujenga nchi yao. Kwa hiyo, Muswada huu upite, ili uweze kuiwezesha Serikali kuingia kazini kukusanya mapato, kwa ajili ya kuwahudumia Watanzania na kutekeleza miradi ya maendeleo. Baada ya kusema maelezo haya naomba sasa kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri ahsante sana, sasa tunaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Bunge Zima.

**SPIKA:** Kamati ya Bunge Zima.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024**
***(Finance Bill 2024)***

**MWENYEKITI:** Sasa tuanze.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

**MWENYEKITI:** Kifungu cha Nne kina marekebisho ya Serikali, Mheshimiwa Waziri ameleta marekebisho kwenye Kifungu hiki lakini kuna Waheshimiwa Wabunge wawili wanataka ufafanuzi. Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha ni Kifungu hiki unataka ufafanuzi?

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha Tano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kamonga ni Kifungu hiki au ni Kifungu kinachofuata?

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Mheshimiwa Waziri ametoa ufafanuzi kuhusiana na ile biashara ya dola, ila atakapofikia lile neno ku-*transact* ndiyo lina utata. Je, mtu akiwa amehifadhi fedha zake nayo inazuiwa? Pia, huo mwongozo utatolewa na kutoa nafasi kwa watu waweze kuweka mambo yao vizuri? *Otherwise,* nampongeza sana kwa uzalendo wa kutetea shilingi yetu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa ndiyo tuko hapo, unasema ikifikia kwenye maneno ku-*transact; "A person who transact using any other currencies other than the legal tender issued by the bank commits an offence*." Hii inashida gani?

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, neno *transaction,* kwa mfano unaweza kuta kuna mtumishi wa shirika la kimataifa mkataba wake uko kwenye kulipwa fedha kwa dola au mtoto yuko hapa na mzazi yuko nje amemfungulia *account* anamhifadhia fedha hizo. Sasa nimeshaona Mheshimiwa Waziri amesema kule anatoa *regulation.* Sasa nikawa nauliza, yaani hiyo ni kwenye *trading* tu, *buying and selling* au kwenye shughuli zote itazuiwa au maelezo mengine yatakaa kwenye *regulation*? Ni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna watu kwa mfano labda ananunua kahawa kwa fedha hiyo nyingine, je haiwezi kuleta *disturbance* kwenye dola? Lakini kwa ufafanuzi alioutoa nilianza kumuelewa, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Waziri, japo ameelewa lakini nimeona unataka kuzungumza.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni kweli kama nilivyosema, tulihangaika hangaika kuweka *wording* inayofaa ili isiathiri zile *routine and norms* lakini tunachokilenga ambacho tuta-*prohibit* ni ile Mtanzania kushurutishwa kutafuta dola ili aweze kupata huduma. Kwa hiyo, masuala ya kunukuu bei kwa dola kwamba Mtanzania ashurutishwe kupanga nyumba, kwamba lazima ulete dola kulipa kodi, lazima ulete dola kulipa ada na lazima ulete dola kupewa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni *daily trading* ambazo tunazizuia lakini mtu kama ana *account* yake na anapokea malipo ya dola, kama nilivyosema ana *credit* kadi ama kadi nyingine za kidijiti za kuweza kutumia *routine* na *re-exchange* ambayo inafanyika kwa njia ya mfumo, nadhani hivyo ni vitu ambavyo ni kama wanavyofanya wenzetu. Kwa hiyo, tumewa-*task* wataalamu tutakapotoa huo mwongozo utakuwa umezingatia *experience* ya wenzetu ambao wamelinda *currency* zao za ndani bila kuathiri *connection* na Mataifa mengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa ufafanuzi huo. Waheshimiwa Wabunge…

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, …

**MWENYEKITI:** Nani amesema Spika?

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwambe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe, samahani kuna Mwambe wawili humu Bungeni.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Geoffrey Mwambe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nilikuwa na mchango kidogo hapo. Ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Kamonga pale, ukitumia neno ku-*transact* lina-*limit* kidogo yale mawanda yake. Neno zuri zaidi ambalo ni pana ni *to deal with, anyone who deals with*. Maana yeke hiyo ni *transaction, saving* na *any kind of facilitation*. Yaani *transaction* ambayo itakuwa *facilitated* na *currency* ambayo siyo *other than Tanzanian currency*. Hii nasema hivi kwa sababu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe, ngoja twende tuelewane vizuri. Kwa hiyo, kwa maelezo yako mtu akiwa na *account* ya dola anakuwa amefanya kosa?

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes* ni *part of dollarization* na hii nilitaka…

**MWENYEKITI:** Aaah! *come on. (Kicheko)*

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitolee mfano, kama mtakumbuka nafikiri Gavana alishawahi kutoa mwongozo baada ya benki moja kutoa matangazo kabisa kwamba, je una imani na Shilingi ya Tanzania?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** …je, una imani na Shilingi ya Kitanzania? Na kama huna Imani nayo njoo fungua *account* ya dola.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wako.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Walikuwa wanasema kabisa hivyo, *which was not good*. Kwa hiyo, *Dollarization* ina-*include transaction* lakini pia na…

**MWENYEKITI:** Sasa hiyo kwa ngazi hii naona itatuchanganya kwa sababu Kifungu kinazungumzia *who transacts,* halafu hapa baadaye inasema; *"Than the legal tender",* ambayo inajulikana kwa hapa kwetu nchini. Sasa tukiipeleka huko kwingine kidogo ndiyo tutakuwa na changamoto aliyokuwa anaitaja Mheshimiwa pale kwa sababu mtu yuko hapa nchini anatumia kadi yake. Hiyo kadi yake kafungua *account* huko kwao, ina pesa ya kigeni ya huko kwao, hapa kwetu akitumia kadi hatuna shida kwa sababu benki zile zinaelewana.

Sasa tukiweka mazingira hayo unayoeleza, huyu ndio itakuwa tumemuweka mazingira magumu kwamba lazima hapa nchini afungue *account,* kwa sababu hata sisi huko tunakoenda hatufungui *account* tunatumia zilezile za kwetu za huku, Mheshimiwa Halima Mdee.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mwongozo kwa yaliyotokea mapema hapa sasa hivi. Utaratibu wa kutunga sheria inabidi mtu alete *schedule of amendments* ili uweze kumpa ruhusa ya kuongea. Sasa naona watu wanajiachia tu, *schedule* hawajaleta. Sasa tukiruhusu haya mambo yatatupotezea muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, uko sahihi lakini sasa hii sheria tunayotunga ndiyo maana hata jana ilibidi tuipe nafasi Serikali kwa sababu safari hii, hii sheria ni tofauti kidogo kwa sababu ya mazingira ambayo yametokea. Ndiyo maana hata jana hatukuweza kuhitimisha hoja tuliipa nafasi Serikali ikalete *further and further amendments.* Kwa hiyo, Mheshimiwa Halima usiwe na wasiwasi kiti kiko vizuri kwa sababu kinaongoza. Utaratibu ndiyo unaishia hapa.

Hata hao Waheshimiwa wawili niliowapa nafasi wameniandikia hapa mbele lakini wanataka ufafanuzi na siyo kwamba labda wameleta marekebisho. Kwa hiyo, Mheshimiwa Halima, tusiwe na wasiwasi tuko vizuri, Mheshimiwa Nahodha.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Nimemsikiliza Waziri kwa makini sana. Kama maelezo yale aliyoyaeleza kwa ufasaha kwa Kiswahili ndiyo atakayoweka kwenye kanuni, kwa sababu kanuni hatutaziona lakini kama taweka kama alivyoeleza nafikiri ule wasiwasi wangu haupo. Isipokuwa kuhusu suala la mgeni, kama mgeni anatumia *credit card* au *visa card* ameweka dola za Kimarekani hatakuwa amevunja sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Uingereza mwaka jana Machi, natumia *Visa Card* ya *CRDB* nimeweka fedha za Tanzania, wanaka *sterling pound* wala huvunji sheria, inakubalika. Kwa hiyo, nafikiri hiyo siyo kuvunja sheria. Ni utaratibu ambao ulitumika katika medani ya Kimataifa, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Imeeleweka. Waheshimiwa tunaenda huku na huku kwa sababu tumeshasema *amendments* ziko hapa inabidi zote tuzipitie. Kwa hiyo, kuna vifungu vitakuwa vimekaa kwa sura hiyo lakini **mwishowe** tutaelewana wote kwamba sheria inakuwa imekaaje. Sasa hicho kilikuwa ni Kifungu cha 4. Sasa katika uandishi wa hizi *amendments* katika kuangalia huku na kule tumejikuta kwamba mjadala ulikuwa kwenye Kifungu cha Tano lakini hakuna shida. Haya tuendelee.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 4

**MWENYEKITI:** Kifungu cha Nne kina marekebisho ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Taarifa za Kamati walizotoa wamekubaliana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 10 kina marekebisho ya Serikali. Mheshimiwa Waziri hapa kwenye Kifungu cha 10(1)(b) kwenye, "*Windfall fuel toll charged pursuant to the road and fuel tolls act*", sasa kwa Waheshimiwa Wabunge wale watakaoweza kukumbuka, nadhani bajeti ya mwaka kama siyo uliopita ni ule mwingine, ilikuwa hii *toll* ikiwa *charged* pia fedha hizi zitumike mafuta yakiwa yamepanda, kwa sababu hapa maana yake mafuta yakiwa yameshuka bei, bei itabaki pale. Hii ya kiasi cha hapa ndiyo mnayotoza. Si ndiyo kinachomaanishwa hapa? Sasa hii ikitozwa je yale mafuta yatakapopanda zaidi hii fedha inaweza ikatumika kuyafanya mafuta yabaki pale kwenye ile bei?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizingatia hilo kwamba katika kipindi kilichopita tuliwaza hivyo lakini hatukwenda kwenye utekelezaji lakini tulijikuta tunakata fedha kutoka kwenye mafungu mengine kutoa ruzuku. Tulikuwa tunatoa shilingi bilioni 100 kwa kila mwezi, ambapo fedha ile tulienda ku-*re-organize* kutoka kwenye Mafungu mengine. Kwa hiyo, kwa sasa hivi tulisema tupeleke kwenye dharura. *Of course,* kwa mwaka huu wa fedha dharura ambayo imetupiga sana na Waheshimiwa Wabunge wameelezea ukubwa wake ni barabara. Kwa hiyo, barabara imekuwa eneo kubwa sana na inatakiwa takribani shilingi trilioni moja mpaka shilingi trilioni 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tulikuwa tumepanga fedha za *windfall* ziende kwenye *contingency* zikiwa zinalenga maeneo ya aina hiyo lakini kwa mwaka huu tumelenga kwenye barabara, ndiyo maana tumepeleka kwenye mfuko wa *contingency*. Kwa hiyo, kwa kile ulichokisema kwenye *broad perspective* tulikuwa tunawaza hivyo kwamba zikitokea dharura kama za aina hiyo maana yake hatuendi kukata miradi ya maendeleo tunakuwa na fedha kwenye *contingency*. Kwa hiyo fedha hii itakuwa *ring fenced* na yenyewe, kwa maana ya ikishamaliza kazi ya dharura tunataka iwe ina-*pile up* kama wazo lilivyokuwa mwanzo, kama hivyo ulivyosema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ni muhimu upande wa Serikali kuwa nalo hilo, ili hata kama kwa sasa hivi fedha zinaelekezwa huko lakini zitakapokuwa zina-*be charged* hizi fedha, huko baadaye ni muhimu kuweka Kifungu vizuri ili mafuta yakiwa yameshuka inapo-*be charged* ile mafuta yakipanda basi yasipande kwa mwananchi yabaki pale kwa sababu Serikali inakuwa imekusanya zile fedha.

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 11

Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14
Ibara ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 25
Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 29

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 30

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34

Ibara ya 35
Ibara ya 36

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 37

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nilileta jedwali hapo na nilikuwa nime-*propose* kufuta *the proposed section 83(d)* ambacho kimefutwa na Serikali na nashukuru kwa hilo maana yake wamesikiliza tulichokuwa tumependekeza, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 42

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kifungu cha 47 Serikali inaleta Marekebisho yake kwa kuongeza sehemu mpya ya 12 yenye Kifungu 47(A) na Kifungu 47(B).

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hii sehemu inayopendekezwa kuongezwa na Serikali ina Kifungu cha 47(A) na 47(B).

Sehemu Mpya ya 12
Ibara ya 47A
Ibara ya 47B

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 48
Ibara ya 49
Ibara ya 50

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 51

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 52

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 53

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 54
Ibara ya 55
Ibara ya 56

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 57

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 58
Ibara ya 59

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kifungu cha 59 Serikali inafanya marekebisho kwa kuongeza

Sehemu Mpya ya 16A
Ibara ya 59*A*
Ibara ya 59*B*.

Sehemu ya 16C
Ibara ya 59C
Ibara ya 59D

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Serikali inaongeza Sehemu Mpya, ambayo itakuwa inasomeka kama 16A na inahusu Mabadiliko ya Sheria, *Amendment of the National Parks Act*. Wanaongeza Kifungu 59A na 59B.

Haya, mabadiliko yaliyopo hapa ni ya Sehemu ya 16A ambayo ina Kifungu cha 59A na 59B. Pia, inaongezwa sehemu ya 16B ambayo inahusu *Amendment of the* Ngorongoro *Conservation Area Act* ambayo inaongeza 59C na 59D. Kwa hiyo, sehemu hizi mbili zinaongezwa kabla ya hii ambayo tunayo hapa ambayo inasomeka kama Sehemu ya 27. Kwa hiyo, Sehemu Mpya ya 26A na 26B.

Narudia tena, Sehemu ya 16A yenye vifungu 59A na 59B na Sehemu ya 16B yenye vifungu vya 59C na 59B vinaafikiwa?

*(Sehemu Mpya iliyotajwa hapo juu na Ibara zake zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 60

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 61

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 62
Ibara ya 63
Ibara ya 64
Ibara ya 65
Ibara ya 66

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 67

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Prof. Shukrani Manya.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ambayo nilikuwa nimependekeza kuanzia Kifungu 67, 68 na 69 na kile cha 71, vyote vilikuwa vinazungumzia kuondoa kodi katika gesi asilia inayotumika katika magari. Vifungu hivyo vimeafikiwa na Serikali kwa hiyo tuwapongeze kwa kukubali maoni hayo, pia Kamati yetu ya Bajeti imekubali kwa hiyo ninafurahi kwamba Serikali imechukua maoni yetu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 68

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 69

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nilikuwa nimeleta marekebisho ya kufuta Kifungu hicho chote, kwa maana ya *A*, *B*, *B* iki-*include ile compressed natural gas* ambayo ni *D* na *E*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya Serikali kwenye kipengele *E* nakubaliana na maelezo ya Serikali kufuta 69*A*, *B* ambayo inahusiana na *D* lakini *E* ikibaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tulikuwa tunatamani hii kodi sasa hivi tumeiondoa lakini kwa *future* ningependa kuishauri Serikali kwamba huko mbeleni tunakoenda tuweze kuangalia kuwavutia Watanzania wengi waweze kuweka magari gesi kwa kuondoa kodi ya vipuli ambavyo wanaingiza,

kujenga vituo vingi na kuhamasisha magari ya Serikali kuonesha mfano kwa kuwekewa gesi na kuingiza magari ambayo yana mfumo wa gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo na kuhakikisha magari ya *diesel* pia yanawekwa gesi ili kwa baadaye hata tukiwa na magari zaidi ya 30% tuweze kuweka sasa hizi kodi ambazo tunazitamani leo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hii sehemu ya 69A hapa mwishoni kabisa, *the amount derived from the collection of the windfall fuel toll shall be remitted to the account of the contingency fund established under the Budget Act to be used solely for road infrastructure maintenance*. Nadhani hiyo sehemu ndiyo ile nilitoa maelezo kule mwanzo. Pengine barabara na mafuta yakipanda bei lakini siyo kwa ajili ya leo, Serikali huko baadaye lazima ifikiri hivyo ili mafuta yanavyopanda beo inatumika fedha hii, yanaposhuka bei, inaenda kwenye barabara, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Kifungu cha 69 pamoja na marekebisho, tuvumiliane marekebisho yamekuwa mengi kwa hivyo lazima tuyapitie.

Waheshimiwa Wabunge, marekebisho yaliyoletwa na Serikali, hapa nilikuwa nimeshawahoji Kifungu cha 67 tulikuwa tumeenda kifungu 68 sasa tulielekea 69. Sasa Kifungu cha 67 marekebisho ya Serikali mliyohojiwa na 68 marekebisho ya Serikali mliyohojiwa ni kuvifuta vifungu hivi. Kwa hiyo, vifungu viwili vya 67 na 68 vimefutwa na Serikali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 70

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 71

**MWENYEKITI:** Ibara ya 71 Serikali inakifuta kwa sababu ya yale marekebisho ambayo yamefanyika huku mwanzo na vile vifungu vilivyofutwa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Ibara ya 72

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 73

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 74
Ibara ya 75

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 76

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake ya Serikali)*

Ibara ya 77

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 78

**MWENYEKITI:** Ibara ya 78 pamoja na marekebisho ya Serikali, Mheshimiwa Waziri hebu tufafanulie haya mabadiliko yaliyokuja

kwenye hiki Kifungu cha 78. Kifungu cha 78 kinafuta kifungu kidogo cha 3 na 4 kinaweka cha 3 kimoja, tuko wote hapo?

Haya, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majadiliano na Kamati ya Bajeti kwenye Kifungu 78 tuliondoa *subsection 3* na tukaongeza kifungu kidogo cha 4*A* na *B*. Ambapo *A* tunasema *as determined by technical team advisory committee established by the Minister under regulations*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ile *process* ya ku-*establish sugar gap* tumeiondoa tunaileta hapa kwenye sheria badala ya kubaki kule kwenye *regulations.* Halafu, *technical advisory committee in consultation with the board, by considering among other things, sugar gap between local productions and consumption including sugar that is needed to maintain a buffer stock in the country*, tume-*add* hiki ili hata pale tuna uzalishaji lakini *National Food Reserve Agency* iwe na haki ya ku-*maintain a buffer stock* ndani ya hifadhi yetu wakati wowote na pale tutakapohitaji kuweza kuitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa tume-*add* hii *technical process* yaku-*determine* naku-*establish buffer stock* ambayo *National Food Reserve* itakuwa inahifadhi muda wote wa mwaka mzima.

**MWENYEKITI:** Sasa, hii 4 na 3 ukizisoma kwa pamoja mbona kama hii 3 inakuwa ime-*defeat* hii 4? Kwa sababu hii 3 hamjaifuta, hii 3 inaendelea kuwepo na sasa mmeongeza 4. 3 inasema hivi, *the board shall not issue sugar import license under subsection 1 unless it is satisfied that the local sugar production is below the level of sugar requirement at a particular time*.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. 3 *essence* yake ni kwamba *the country is full sufficient in terms of production,* haturuhusu *importation*. Lakini, *reserve it can be acquired even from the local producers* sisi tukahifadhi kama Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumei-*maintain* 3 lakini 4 na hizi *subsection* ndiyo zinatengeneza ile *concept* ya kuwa na *buffer stock at any particular time na determination* inafanywa na *technical team*. Kwa hiyo, tumezalisha, tumefikia kiwango tunachohitaji kama nchi, hakuna *importation*, sheria inasema wazi kabisa. Halafu, *National Food Reserve* haitakiwi kutokuwa na *buffer stock* wakati wowote ule ili kuweza ku-*control* bei inayokuwepo sokoni.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna kitu kidogo hapa. Mwanasheria Mkuu wa Serikali uko nazo hizo nyaraka? Hebu zitazame vizuri kwa sababu ikitokea soko linayo sukari ya kutosha lakini *stock* haipo, ile inayoitwa *buffer*, Serikali itaitoa wapi hiyo sukari ya kuweka kule? Yaani kwa vifungu hivi ukivisoma vyote viwili kwa pamoja, kwa sababu umeshasema kama sukari soko limejitosheleza, hakutakuwa na utafutaji wa sukari lakini kama hii inaitwa *reserve*, si maana yake lazima iwepo?

Sasa, tutaipata wapi ile ya kuwepo wakati huku sokoni tuko vizuri lakini likaanguka jambo hapa la mabadiliko ya tabianchi na sukari haipo na haturuhusiwi kwa vifungu hivi ukivisoma pamoja. Hebu tusaidiane maana inawezekana mimi, nadhani kuna neno mahali linapaswa kukaa vizuri.

Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwa pamoja kuanzia tulipotoka, *clause* ya *76* halafu tunapofika kwenye 78 ninaona umuhimu kama anavyosema Mheshimiwa Waziri ile *subsection 3* kubaki kuweka msingi lakini baadaye kuongeza yale mabadiliko yanayoongezwa ili *technical team* sasa kwa kuongozwa na ufundi na tafiti ndiyo itoe *criteria* kwa bodi kuona kama kuna ile *gap* ambayo inakuwa *established* na hatua za kuchukuliwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *the board shall not issue sugar import license under subsection (1) unless it is satisfied that the local sugar production is below the level of sugar requirement at a particular time.* Hii *below level*

haipo, yaani tuko vizuri lakini ile *reserve* haipo, tutapitia mlango gani? *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaweza kuwa jambo *technical* lakini mimi nachukulia hii *technical team* lazima itakuwa na mawanda mapana ya kuangalia maeneo mengine zaidi ya yale ya kawaida.

**MWENYEKITI:** Sasa ndiyo tunataka kurekebisha hayo mawanda yanayowapa wasiwasi wale wa viwanda, yanampa wasiwasi mlaji wa kawaida, ndiyo tunataka hapa tuyaweke sawa ili wote twende na uelewa sawa. *National Food Reserve Agency* itunze sukari, huku nje na kwenyewe viwanda vyetu vizalishe, tujitosheleze, tuwe sawa. Lakini hiyo hoja sasa hapo kwenye kutunza wakati soko linayo unatunzaje? Yaani unakuwa umepita wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa msingi wa hoja yako, lakini inajibiwa *sub-section 4* kile kipengele ambacho kinasema, ukikisoma mwisho kinasema *including sugar that is needed to maintain a buffer stock*. Kwa hiyo, jukumu la *technical team* inapofanya *evaluation*, kwamba tuna-*demand* ni tani 650,000 mfano, *buffer stock* ni x *quantity* kwa hiyo, *production* imetimiza mahitaji yetu lakini tuna *buffer stock* hii ambayo tunaihitaji. Kwa hiyo, kwa kutumia hiki kipengele, *the buffer stock* itakuwa *determined* na *technical team* na hiyo ndiyo itakayokuwa inahifadhiwa kila wakati na *National Food Reserve Agency*. *(Makofi)*

**MWENYEKIT:** Ikitokea unapaswa kuagiza ndiyo swali langu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *technical team* inayokaa ndiyo ita-*determine* na hapo ndiyo itakayoshauri kwamba kuna uhitaji wa uagiziaji ama hakuna uhitaji wa uagizaji.

**MWENYEKITI:** Kwa nini hapa kwenye 3? Mheshimiwa Mbunge nimekuona lakini tusikilizane kidogo, hii namba 3, kwa namna

ilivyoandikwa, hapa hiki Kifungu cha 4 *actually* kinachofanya ni jambo moja tu ku-*define* ni nini maana ya *low level of sugar production*, ndiyo kinachofanya. Lakini hiki Kifungu cha 3 kimeweka katazo, hii inakueleza tu maana ya *low level* kwamba ile kamati ndiyo atakayoteua Mheshimiwa Waziri, ndiyo itakayosema.

Mheshimiwa Manyinyi naona unaweza ukatusaidia hapo kidogo.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilichotaka tu kupata tu *comfort* ya Serikali kwa yale maneno ambayo wameyasema kwamba lazima wawe na *buffer stock* kwa ajili ya dharura. Kama hivyo ndivyo, ndiyo maana tunasema hivi sasa wanacho tayari kianzio cha tani 70,000 ambacho hakijafika lakini kitafika wakati wowote na kwa sababu uzalishaji upo wa kutosha, sasa wapo tayari kuanza na hiyo kama *buffer stock* wakati huo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba sukari haiishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi hata jana ulisema, una shida gani na hii tani 70,000 ikija hapa ikapunguza bei ya sukari? Kama itatupunguzia bei ya sukari, una shida nayo hiyo tani 70,000?

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umesema vizur, wala mimi sina shida na hiyo…

**MWENYEKITI:** Aaah! Haya, ahsante sana, basi ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri ili tuweze kuwa wote tumeelewana vizuri kwenye hoja hii, nafikiri, hivi Mkurugenzi wetu wa Sheria yuko humu ndani? Hayupo, eeh! Haya, Mwanasheria Mkuu labda umepata neno ambalo litatutoa hapa? Hii namba 3 kuna neno litakuwa linahitajika kuwekwa ili kuweka msingi huo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, njia moja ya kuondoka mkinzano huo ni kuanza na neno *Subject to provisions of Section 14(a)* ili sasa ikisomeka kwa pamoja,

ionekane hilo katazo. Vilevile litatolewa baada ya kuzingatia yale yote ambayo yatakuwa yametokana na *technical assessment* itakayofanya na *team* lakini pamoja na *mandate* ambazo zinahusiana na uagizaji.

**SPIKA:** Sawa, Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane. Kifungu hiki, Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka labda Mheshimiwa Waziri atusaidie ili tuweze kupata picha ya pamoja. Kuna hoja ya msingi ambayo ni kulinda viwanda vya ndani, ndiyo msingi, sawa? Lakini kuna hoja ya pili ya kuwa na akiba *(reserve)*, kuna hoja ya tatu, yametokea kama yaliyotokea mwaka huu, uwezo wa kuagiza nani anao? Na kwa sababu gani? Na kuna hoja ya nne, uhai wa sukari, sasa, hapa tunataka tujue haya maswali ambayo yatatupa majibu, yamekuwa *translated* vipi kwenye hivyo vifungu mnavyovizungumza kwenye Sheria? Msitupe mambo ya *technical* sijui *technical*, kwenye Sheria kwa sababu Sheria ikitupa msingi mzuri, huko *technicalities* zitaenda kwenye Kanuni, sasa mtuambie amejibu vipi hizo hoja nne? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, sasa kuna maneno hapa, hiki kifungu kidogo cha 3 yanapaswa yaongezwe ili kuweza kujua kwamba hii *importation* haitazuiwa tu na jambo moja la *low level*. Ni kwamba nchi lazima iwe na *reserve*, sasa *whether reserve* itatoa kwa wale wazalishaji wa hapa nchini wakizalisha *in excess* ama itatoa huko nje lakini lazima nchi iwe na *reserve*. Sasa, tukizuia wakati ndiyo tunajaribu kurekebisha hilo tatizo ambalo tumelipata tena hapa, italeta changamoto.

Sasa, niwaombe kwa tangazo hili nadhani Mkurugenzi wa Sheria atakuwa ananisikia huko aliko, lakini pia namuomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kama nimemuona hapa Mwanasheria Mbobezi. Enhee! Hebu nyinyi kwa sababu haya inabidi tubaki nayo humu ndani, tunaendelea na marekebisho mengine. Nyinyi Waheshimiwa Mawaziri wawili, yule Mkurugenzi wetu wa Sheria na huyu wa *AG* hebu kutaneni pale nje, mtengeneze kitu ambacho hiki Kifungu

cha 3 kikae sawa kuweka msingi wa hiki cha 4 mlichoweka hapa na mwanasheria mwingine atakayejitolea anaweza kwenda, Mheshimiwa Halima Mdee hebu kaungane pale ukasaidie ama mkutane hapo nyuma, kutaneni hapo kwenye *lounge* yangu hapa nyuma. *(Makofi)*

Kutaneni hapo Mheshimiwa, kitengenezeni hicho vizuri halafu mje nacho hapa tufanye mambo, tutengeneze Sheria ikae sawasawa ili kuondokana na hii changamoto ambayo wametusumbua hapa. Niongeze na Mheshimiwa Tadayo, unapigiwa kura huku, Mheshimiwa Olelekaita unapigiwa kura huku, haya, hebu elekeeni hapa *lounge* mara moja mfanye hayo mambo yakae sawa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Olelekaita na yeye anaitwa huku kwa hiyo aende, ahsante sana, nadhani hao wanatosha kwa sababu wakiwa wengi sana pia tena mjadala utakuwa hauishi, ahsante sana. Kwa hiyo, Kifungu cha 78 na haya marekebisho yaliyopendekezwa tutakirejea wakishamaliza hawa ndugu zetu wakija hapa ili hii changamoto tuliyonayo tuweze kuiweka sawa, sasa, tuendelee Waheshimiwa Wabunge. Haya, tuendelee Waheshimiwa Wabunge.

Ibara ya 79

**SPIKA:** Kifungu cha 79, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, haya maneno yanayoongezeka hapo kwenye 79 14(a)(2) yanayoongezeka; "*and in the manner provided in the regulations after the word board,*" hebu yapitie mbona kama yanakuwa *superflow?*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri, *recraft* inayofanyika iangalie na Kifungu hiki.

**SPIKA:** Tutakuwa tumewapa sasa mawanda mapana sana.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana kwa sababu inahitaji kusomwa kwa pamoja.

**SPIKA:** Aahaha! Kwa pamoja lakini na sisi tumekipitia hapa mbele tunafikiri hiki kinaweza tu kusimama pekeyake hata bila hiki kingine. Hapa sasa tunaongeza haya maneno kwa ajili gani? "*The Minister shall in consultation with the Board determine the mode of importing sugar to cover sugar gap*" wakati huohuo tunasema tunataka kuongeza maneno *The Minister shall in consultation with the Board and in the manner provided in the regulations*", *regulations* ambazo anatengeneza yeye mwenyewe *Minister*? *Like*, hii iko sawa kwenye *drafting*? Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *regulations* zinatengenezwa ili kumuongoza…

**SPIKA:** Samahani endelea Mheshimiwa, sijakusikia. Samahani.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema *regulations* zinapotengenezwa, inakuwa ni sehemu ya Sheria za kumuongoza Mheshimiwa Waziri kutokutenda kinyume na matakwa ya Sheria. Kwa hiyo, nafikiri ile uwajibikaji wake kama Waziri lazima ufuate *regulations* ambazo zitaandaliwa.

**SPIKA:** Haaaaa! *Wallah! A minister shall*… haya, tusonge, maneno yanakuwa mengi lakini hayana madhara kwa sababu *regulations* zenyewe pia anatengeneza mwenyewe *Minister* kwa hiyo atazitengeneza kwa sura anayoona haitaleta mkanganyiko.

Ibara ya 79

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 80

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 81

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 82
Ibara ya 83
Ibara ya 84
Ibara ya 85

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 86
Ibara ya 87

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 88

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 89
Ibara ya 90
Ibara ya 91

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 92
Ibara ya 93
Ibara ya 94
Ibara ya 95

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 96

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 97
Ibara ya 98
Ibara ya 99

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 100

*(Ibara iiliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 101

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kifungu Na. 101, nikiwa nimeleta marekebisho ya kuondoa neno siku 30 na kuweka siku 90. Lakini nashukuru Serikali imekiondoa Kifungu hiki kabisa kwa hiyo, nakubaliana na marekebisho ya Serikali, lakini lazima tuangalie *the cause of this*, sasa hivi ni *90 days* lakini bado kunakuwa na *backlog* nyingi sana watu hawalipwi *on time* hizi *VAT refund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tumeirudisha, Serikali iendelee kuweka *90 days*, ni wakati sasa wa Serikali kujenga mifumo imara ya kisasa yaani TEHAMA, kupitia TEHAMA ili iweze kufanya *compilation* ya *applications* za hawa watu wanaokuja kudai *VAT refund on time* na kuhakikisha kwamba baadaye tunarudi kwenye *at least 60 or 30 days* kuliko kuwa na *90 days*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi nilikuwa nimekiondoa kwa sababu najua uhalisia, kulikuwa bado kuna

*backlog* nyingi sana ambayo unakuta mafaili ya haya wanaoomba *VAT refund* hawapewi *on time*, hata *90 days* zenyewe bado kulikuwa tunabaki na mafaili mengi sana. Kwa hiyo, nashukuru kwa haya marekebisho ambayo wameleta lakini *going forward*, lazima muimarishe mifumo yenu kuhakikisha kwamba *applications* zinafanyika *on time*. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo ilifutwa)*

Ibara ya 102

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 103

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, pole nimesikia umegonga meza lakini tumeshahoji Kifungu, sema hoja yako, Mheshimiwa Waziri ataichukua Kifungu kitakuwa kimeshapita.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nilijitahidi kuandaa jedwali lakini bahati mbaya lilikuja kwa kuchelewa. Hoja yangu hapa ni moja, kwanza tunaishukuru Serikali kwa hii *flexibility* kukubali kuwa-*exempt VAT* kwenye chai. Lakini kwa hali ya Sekta ya Chai ilivyo sasa hivi, ukifanya *VAT exemption*, hauwezi kuja baadaye ku-*claim refund*. Ni ombi kwamba Serikali tuiangalie, huko mbele ya safari, ili kuiinua Sekta ya Chai na kuirudisha kwenye uimara wake, ni vizuri tunai-*zero- rate* badala ya kufanya *VAT exemption*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni ushauri tu kwa sababu jedwali langu limechelewa, ili Serikali ione namna ya kutusaidia tui…

**SPIKA:** Kwenye marekebisho nadhani Serikali imefanya hiyo *zero*.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, kwenye marekebisho ni…

**SPIKA:** Marekebisho, Kamati ilikuwa imependekeza hivyo nadhani ndiyo mlivyokubaliana na Mheshimiwa Waziri, sivyo?

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, walifanya *VAT exemption*, hawajai-*zero-rate*.

**SPIKA:** Nadhani wamefanya *zero-rate*, hebu, ngoja tupitie hizi tulizonazo hapa mbele, ama Mwenyekiti wa Kamati tusaidie, mbona hayo ndiyo maelezo sijui yaliyokuwepo, ama? Ama tumepitiwa? Mwenyekiti.

**MHE. ORAN M. NJENZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumependekeza iwe *zero* badala ya *exempt*, lakini baada ya maelezo ya Serikali na kuifafanua, tumesema ibaki hiyohiyo kwa muda huu kuwa *exempt*. Kwa hiyo, tutaendelea kuiangalia kwa sababu kwenye kilimo, *input tax* mara nyingi zinakuwa siyo nyingi sana kwa hiyo tukasema iwe *exempt* badala ya kuwa *zero*.

**SPIKA:** Hoja anayosema Mheshimiwa Mbunge ya kwamba wakiweka *exempt* maana yake wale wa chai hawataweza kudai *refund*?

**MHE. ORAN M. NJENZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yeah*, na hiyo tulikuwa tumei-*consider* ndiyo sababu nikasema ya kwamba *input VAT* kwa kilimo mara nyingi siyo nyingi kiasi hicho. Kwa hiyo, tunasema, ikiwa *zero*, ina maana watahitaji *refund* na kutokana na *complications* ambazo ziko kwenye *refund* ya *VAT*, tukasema ni bora kwa kipindi hiki tuiache iwe *exempt* na isiwe *zero*, lakini hoja ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati nafikiri ni hoja ya msingi. Ila ni kwa vile Serikali nayo walitupa maelezo ya kuridhisha ya kwamba, kwa kipindi hiki tuiache iwe *exempt* badala ya kuwa *zero*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alichokieleza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ni sahihi. Moja ya maelezo tuliyoyatoa ni *administration complication* za utoaji wa *zero rating.* Kwa sababu ita-*invite claiming* ya *input* ya *refund* kwenye *input* zake. Na kwa aina ya bidhaa tuliona itaenda kukinzana tena na sheria. Kwa sababu Sheria ya Kodi inampa Mamlaka Waziri wa Fedha kufanya *exemptions,* kwa hiyo *administration* yake wakati wa utekelezaji kwa *exemption powers* zinakuwepo kwa Waziri wa Fedha, na kama itazidi *one billion powers* zinakuwepo kwa *cabinet.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa bidhaa ambayo *administration* yake haiko *intended* kwa *exporting* sheria inatuzuia kufanya *zero rating,* inatupa fursa ya kufanya *exemption* ambazo zinaweza zikawa *monitored during the time* ya utekelezaji wake. Kwa hiyo tulivyoshauriana na Kamati tulikubaliana kwamba kwa hali tete ya sekta inavyoenda sasa tuunganishe na yale mengine ambayo tumeyatoa lakini tuanze na *exemption;* na kadri tunavyokwenda tutaendelea kitu gani kingine kitaweza kufanyika.

**MWENYEKITI:** Sawa. Mheshimiwa Mbunge kama nilivyosema kwa sababu tayari Bunge lilikuwa limekwishafanya maamuzi ya kifungu hiki lakini nikakupa nafasi ili Mheshimiwa Waziri asikie hoja yako ili kama anaweza kuifanyia kazi kwa huko baadaye basi atafanya hivyo. Nadhani katika kipindi hiki kama walivyosema ndani ya mwaka huu ni kutazama namna ambavyo imeweza kufanya kazi halafu huko mbele tutaendelea kuishauri Serikali. Kama kuna mabadiliko yoyote ambayo watapaswa kufanya basi tukishaziona changamoto nadhani tumeona Serikali kwa kweli wakishauriwa wanasikiliza. Kwa hiyo ngoja tuone utekelezaji wa hiki ambacho Serikali imeleta tuone namna ambavyo inaweza kukwamua sekta hii.

Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa tumeisha hoji Kifungu hicho tunaendelea.

Ibara ya 103
Ibara ya 104

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 104A
Ibara ya 104B

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kifungu cha 104 Serikali inafanya marekebisho kwa kuongeza sehemu mpya ya 26A yenye Kifungu 104A na 104B.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Serikali inaongeza sehemu mpya ya 26A ambayo inazungumzia *amendment of the Wildlife Conservation Act,* kwa hivyo naongeza Kifungu kipya cha 104A na 104B.

Waheshimiwa Wabunge, tunaafiki sehemu hii mpya ambayo Serikali imeileta?

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko ya Serikali)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, haya tumeishavimaliza hivi vifungu vingine isipokuwa kile Kifungu ambacho wenzetu wamepewa kazi huko ya kwenda kukifanyia kazi; na ili tuweze kusema hapa mbele kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi lazima na kile kifungu tuwe nacho, kwa sababu la sivyo tutakuwa tumemaliza bila hivyo vifungu ambavyo wenzetu wamekwenda kuvitazama. Kwa hiyo tuwape dakika chache wamalize halafu watuletee. Lakini na sisi tulioko humu ndani tuendelee kuangalia namna ya kifungu kinavyoweza kukaa. Haya kuna Mbunge naona yeye anaweza kuwa na majibu. Mheshimiwa Mbunge wa Buchosa, Mheshimiwa Eric Shigongo.

Ibara ya 78

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina jibu ila nilitaka tu nitumie huu muda wakati tunasubiri wenzetu wanaokuja niseme nilivyoilewa sheria hii. Ninajua suala la sukari ni kubwa, na nikienda jimboni lazima nitalikuta kijijini kwangu. Sasa niseme nilichokifahamu halafu niambiwe kama ufahamu wangu uko sahihi au kuna upungufu, kwa ridhaa yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kwa kifupi nilichokielewa kwenye mjadala ulioendelea hapa ambao wenzetu wanaumalizia huko nyuma. Kwamba itakuwepo *technical team* na kazi ya *technical team* itakuwa ni ku-*establish gap;* na ikishajua *gap* ni kiasi gani, kwa mfano viwanda vinauwezo wa kuzalisha tani laki nne kwa mwaka lakini mahitaji ni tani laki sita kwa hiyo *gap* inakuwa ni laki mbili. Jukumu la kuiagiza hii *gap* wamepewa watu wa *NFRA,* ndiyo kazi yao kuiagiza. Wakishaziba hiyo *gap* wanatakiwa wawe na kiwango kingine cha sukari ambacho kitaitwa *buffer,* ambacho kitakuepo kama itatokea dharula nyingine. Kama ikitiokea sukari viwanda viwanda vimeweza kuzalisha laki sita kwa mwaka bado wa *NFRA* watakuwa na wajibu wa kununua hiyo *buffer* kama laki moja au laki mbili ili ikitokea tatizo wakati wote iweze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka tu nione kama uelewa wangu uko sawa sawa ili kesho kwenye mkutano wangu wa hadhara wananchi wakiniuliza niweze kuwaelezea vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naona nimepata wasaidizi huko nyuma wamekujibu kwamba umeelewa vizuri. Sasa ili wote tuwe tumeelewa vizuri hicho utakachokwenda kusema ngoja kije kwanza hiki walichokileta hawa ndugu zetu. Sasa sijui wamekubaliana huko mtoa mrejesho ni nani; ni wewe uliyetangulia au ni hawa waliobaki? Ni nani?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mimi.

**MWENYEKITI:** Umepewa wewe kazi ee.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kuondoa *contradictions* tumekubaliana chini ya Uongozi wa Wanasheria Wabobezi kwamba kipengele cha tatu ambacho kilikuwa kinasema "*the body shall not issue sugar import license under this sub section*" kinafanyiwa marekebisho madogo. Tunaongeza maneno *save for the mandate of National Food Reserve Agency to maintain the buffer stock, the board shall not issue sugar import license under sub section one unless it satisfied* mpaka mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tumeongeza kipengele kidogo ambacho kinaitafsiri hiyo *mandate* ya *NFRA what is that buffer stock*. Kwa hiyo, tumetafsiri *buffer stock. For the purpose of this section buffer stock means a sugar minimum reserve for the consumption of two months reserved by National Food Reserve Agency. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, vizuri, hebu niyapate haya maandishi hapa ili niweze kuunganisha na yaliyoko hapa, yale maandishi kule. Asogee hapa mbele, ngoja aniletee kwanza, niletee nisome mwenyewe kama sikuelewa sasa leo, leo itakuwa kazi hapa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sawa, hiki kifungu cha tatu maandishi yanasomeka hapa. Kwa hiyo, kitaongezwa maneno kabla ya neno *the board; "save for the mandate of National Food Reserve Agency to maintain the buffer stock, the board shall not issue sugar",* sawa. Sasa maana yake kile alichokuwa anakieleza Mheshimiwa Shigongo sasa ni kwamba lazima nchi iwe na *buffer stock* kwa maneno haya kuongezeka hapa. Kwa hiyo, itapatikanaje *buffer stock;* lazima iwepo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya sehemu inayofuata ni hii ya kusema kifungu kidogo cha nne sasa kilikuwa kimeishawekwa cha 4A na 4B sasa wanaongeza kifungu kidogo, wamependekeza kifungu kidogo ambacho kitakuwa kinasema kuhusu hii *buffer stock*. *For the purpose,* nadhani hii inaitwa *for the purposes.* Eti

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, huwa ni *for the purpose* au *purposes?* nadhani ni *purposes* siyo? Haya. *For the purposes of this section buffer means,* sasa hapa inabidi iwe neno *buffer stock* badala ya *buffer. Buffer stock means sugar a minimum* au *a minimum sugar reserve. A minimum sugar reserve,* haya *a minimum sugar reserve for consumption of two months.* Sawa.

Sasa Waheshimiwa Wabunge nadhani tumekubaliana kimsingi kitu ambacho kitawekwa hapa, na haya ndiyo maneno yatakayowekwa ili kuweka mazingira ambayo tutakuwa na sukari hiyo kwa hiyo miezi miwili.

*(Hapa Mhe. Charles J. P. Mwijage alizungumza bila kutumia kipaza sauti)*

**MWENYEKITI:** Ngoja nimalize haya maelezo halafu ulete hoja yako. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa sababu haya maandishi tunayoyapitisha hapa tumeishaelewa msingi ambao tunataka uingie. Sasa haya ya kuongeza S mahali kuongeza wapi lazima sheria yetu ikae vizuri. Sasa kwa sababu sheria inakuruhusu wewe kufanya vile utaenda ututengenezee hiyo vizuri hapa kwa kutumia haya maneno tuliyoyasema. *(Makofi)*

Haya, Mheshimiwa unasema hoja, hapo ndipo sijaelewa.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwenye Kingereza chao hicho.

**MWENYEKITI:** Ahaa! Kwenye Kingereza. Haya sema ili Mwanasheria Mkuu wa Serikali akichukue hicho.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kingereza kilichotumika kinapaswa kurekebishwa kidogo, kwa heshima na tahadhima Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hilo neno *minimum* linaleta tatizo; ni tatizo kubwa. Mtu anaweza akaleta *consumption* ya mwaka mzima hajavunja sheria, lakini kuweka *consumption* ya mwaka mzima hapa

ataweza kuwanyima *confidence* wawekezaji ili wasiweze kuwa na moyo wa kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani *it should be maximum,* yaani tuwe na *stock* ya kututosha miaka miezi miwili tu, isizidi; lakini unaposema isiyopungua miezi miwili; Aaa! Naomba kuwakilisha.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu nia ni kuweka mazingira ambayo hii changamoto inayojirudia rudia kila mwaka isiwepo. Mheshimiwa Waziri kwa hesabu za kawaida tukisema miezi miwili hii "a *minimum reserve for consumption of two months*" Tukisema hivi tunamanisha ni zile hesabu zitakuwa zimepigwa kwamba kwa matumizi ya mwezi kwa Watanzania wanahitaji kiasi gani, kwa hiyo inapigwa ya miezi miwili ndiyo nimeelewa sawa sawa?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba tutapiga hesabu ya matumizi ya Watanzania ya mwaka mzima, kwamba matumizi yetu ni tani laki sita. Sasa, kama hii ndiyo *consumption* ya mwaka mzima maana yake; kwa mfano kama hata kwenye mahindi sasa hivi hata *any particular time* tuna *reserve* mahindi *at least* yatakayotutosheleza mwezi mmoja ndani ya nchi kuweza kutumia. Kwa hiyo tunapopiga mahesabu ya mwaka mzima tunaweka *buffer stock* ya miezi miwili tunakuwanayo ghalani kwa sababu tunajua mahitaji yetu ya kila mwezi ni kiasi gani.

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa mimi nafikiri kwa ngazi hii Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ni jambo jipya, kwa hiyo nafikiri tunaweza kuanza na hii ya miezi miwili tuiwekee sura ambayo haitaifanya *NFRA* sasa maghala yote ijaze sukari, sindivyo? Ili tuweze kwenda vizuri. Kwa sababu kama nilivyosema jana pande zote ni zetu, lazima wawekezaji nao wawe sawa na wananchi pia wawe sawa. Kwa hiyo nafikiri kwa miezi miwili ndiyo changamoto ambayo wenzetu wanaipima huko; na madamu wameileta wao tunaondoa neno minimum ili *NFRA* isijikute ina sukari ya mwaka mzima kwa sababu viwanda sasa vinaweza kupata changamoto.

Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa sababu ni jambo jipya tukishaona hii ya miezi miwili ikitokea, na kwa kweli isitokee kama ya mwaka huu, lakini ikitokea kwamba tumepata changamoto na haikutosheleza basi Bunge bado lipo kwa ajili ya kazi hii. Kwa hiyo kwa sasa nadhani tupitishe hii miezi miwili ambayo itafanya kila upande uwe sawa. Mwanasheria Mkuu wa Serikali nadhani hilo pia umelisikia? Kwa hiyo tunaondoa neno *minimum* hapa. Kwa hiyo itakuwa; *buffer stock means, not a maximum,* hiyo hatutaweka, tunaweka neno *minimum,* labda *shall not exceed;* yaani ile sheria ndiyo inavyotaka; *sufficient for two months, not exceed.*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba tuondoe neno kama walivyoshauri *minimum* na neno *maximum* lisiwepo tuseme tu *buffer stock means sugar sufficient for consumption of two months reserve*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hasa unajua ndiyo maana nimesema *drafting* ya matumizi ya haya maneno ya *sufficient* na *adequacy* na nani yatatupa changamoto hapa. *Shall not be exceeding;* yaani kuna maneno huwa hayaingii kwenye sheria, kwa sababu kipimo chake hata wewe unavyosema miezi miwili huna hakika sana na hiyo miezi miwili hizo utakazosema tani laki mbili ndiyo kweli zinatosheleza. zinaweza kupungua ama kuongezeka kidogo.

Waheshimiwa Wabunge nadhani tukubaliane kwamba hoja ya msingi *AG* ameielewa na maneno ya kuanzia tumeishampa. Yale ya kuweka *comma* kufanya nini yeye atakwende kuyaweka kwa sababu sheria inamruhusu kufanya hivyo. Sawa, kwa hiyo tusonge hapo.

Sasa ninawahoji kwa maneno haya niliyowasomea. Kwanza ya kuongezeka pale kwenye kifungu cha tatu kilichokuwepo kwenye Muswada halafu maneno ya kuongezeka kwenye kifungu kidogo cha nne cha hii 78, kifungu kidogo cha nne ambacho

kitakwenda kuongeza maana ya neno *buffer stock*. Kwa hiyo, ndiyo nawahoji sasa hicho kifungu kikiwa kamili kwa sura hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, wanaoafiki Kifungu cha 78 pamoja na marekebisho ya Serikali na yale ambayo Bunge imeyafanya sasa na kumpa kazi Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kurekebisha lugha ya kisheria waseme ndiyo, ndiyoo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kutoa taaria kwamba Kamati ya Bunge zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Tuketi. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, namba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge zima imepitia Muswada wa Sheria ya Fedha 2024 *(The Finance Bill Act, 2024)* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi na Bunge zima.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA Serikali**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024**
***(The Finance Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu.

Hivi nimeshawahoji au bado?

Mlipaswa kuhojiwa kabla haujasomwa mara ya tatu, sasa ameshasoma mara ya tatu. Tunafuta hiyo kwanza ya kusomwa mara ya tatu, inabidi asome upya. Maana inabidi mhojiwe kwanza, halafu ndio asome mara ya tatu.

Waheshimiwa Wabunge, wanaoafiki kupitishwa kwa Muswada wa Sheria ya Serikali ambao ni Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024 *(The Finance Bill 2024),* waseme ndiyo. Wasioafiki waseme siyo.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote mmeafiki, ahsanteni sana. Sasa namuita Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024**
***(The Finance Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu. Baada ya kusomwa, Muswada wetu huo kwa mara ya tatu, natumia fursa hii kutangaza rasmi kwamba, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 *(The Finance Bill 2024)* umepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu wetu wa Kikatiba Muswada huu sasa utapelekwa kwa Mheshimiwa Rais, ili na yeye aweze kufanya kwa sehemu yake na uwe Sheria tayari kwa utekelezaji.

Waheshimiwa Wabunge natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu Waziri wa Fedha kwa hatua zote ambazo tumefikia. Pia, Katibu Mkuu na Watendaji wote chini ya Wizara hii kwa ushirikiano ambao wameutoa tangu tuanze safari hii ambayo leo tunaihitimisha hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, baada ya hayo yote tunaitakia kila la heri Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla kwa yale yote ambayo mmewaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba, mtayafanyia kazi. Pia, tunawatakia utekelezaji mwema wa yale yote ambayo mliyaleta kwetu na tumewapitishia hayo mafungu, ili muweze kwenda kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo na kuwatumikia Watanzania. Waheshimiwa Wabunge kwa kusema hivyo, tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. BARAKA KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Kanuni ya 35 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Naomba kutoa taarifa kwamba, shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, sasa zimemalizika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusikia hiyo Taarifa ya Katibu wa Bunge sasa tunaendelea.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

**SPIKA:** Hoja ya kuahirisha Bunge. Waheshimiwa Wabunge namuita sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, aje atoe hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na kutuwezesha kukutana katika siku hii muhimu. Nasema siku hii ya leo ni muhimu kwa sababu, tunakwenda kuhitimisha Shughuli za Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ulioanza Tarehe 2 Aprili, 2024.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kazi nzuri na weledi uliouonesha wakati wote wa mkutano huu ambao ni mahsusi, kwa ajili ya mawasilisho na Mjadala wa Hoja za Bajeti za Kisekta na Bajeti Kuu ya Serikali. Ninakupongeza sana kwa kuliongoza Bunge hili kwa hekima ya hali ya juu huku ukitanguliza maslahi ya Wananchi wa Tanzania katika kipindi chote cha mijadala ya hoja zinazowasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kukusaidia kuliongoza Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile natumia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, nikianza na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum. Vilevile,

nampongeza Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wenyeviti wetu kwa kuendesha mijadala ya Bunge kwa weledi mkubwa. Sina shaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana na mimi kuwa, Waheshimiwa Wenyeviti wameonesha hekima, umahiri, ukomavu na uwezo mkubwa wakati wote walipokuwa wakitekeleza majukumu yao ya kumsaidia Mheshimiwa Spika. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kuwasilisha na kutoa ufafanuzi wa Hoja za Bajeti za Kisekta na pia, kwa kujibu hoja zinazowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kushiriki kikamilifu katika mijadala ya hoja zilizowasilishwa katika hili Bunge la Bajeti. Wakati wote wa mijadala Waheshimiwa Wabunge wametoa maoni, mapendekezo na michango kwa lengo la kufanikisha Bajeti ya Serikali na kutimiza wajibu wetu wa kikatiba kwa kupitia, kujadili na kupitisha mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Ninawashukuru sana na nikiri kwamba, michango yote pamoja na ushauri imekuwa ikisaidia sana katika mipango ya utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii pia, kumpongeza Mheshimiwa Oran Manase Njenza, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwa kuongoza vyema vikao vyote vya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ya Mwaka 2024/2025. Uongozi wake makini umekuwa chachu ya mafanikio ya vikao vyote na kuiwezesha Serikali kupata michango maoni na mapendekezo wakati wa mchakato wote wa maandalizi ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Serikali imepokea ushauri, mapendekezo na michango yote iliyowasilishwa hapa Bungeni. Vilevile, itaendelea kuhakikisha kuwa inasimamia ipasavyo utekelezaji wa vipaumbele vya bajeti kama vilivyoainishwa katika bajeti hii. Licha ya hayo nitaimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato ya Serikali na matumizi ya Fedha za Umma kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Hamis Yusuph Mussa, Mbunge wa Jimbo la Kwahani kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo hilo kufuatia uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni wakati mkutano huu ukiendelea. Ushindi huo utadhihirisha kwamba, wananchi wana imani kubwa na Chama cha Mapinduzi kutokana na uongozi thabiti, sera makini pamoja na ilani ya uchaguzi inayotekelezeka. Natumia fursa hii kumkaribisha sana Mheshimiwa Hamis Yusuph Mussa na ninamuhakikishia kuwa, Waheshimiwa Wabunge wote tutampa ushirikiano mkubwa, ili aweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mijadala ya bajeti ikiendelea Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, kuwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Aidha, Mheshimiwa Rais alifanya mabadiliko ya baadhi ya Watendaji Wakuu wa Taasisi, Mabalozi na Viongozi wa Tawala za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na uteuzi wa viongozi wapya ambao pia, wameteuliwa. Natumia fursa hii kuwapa pongezi na kuwatakia kila la kheri wateule wote katika kutekeleza majukumu yao mapya. Mheshimiwa Rais amewaamini basi nendeni mkafanye kazi kwa bidii na kuhakikisha kwamba, mnashughulikia kero za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nawakumbusha wateuliwa wote kuhakikisha kwamba, wanasimamia kikamilifu utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinnduzi ya Mwaka 2020 pamoja na Ahadi za

Viongozi Wakuu wa Nchi. Kila mteule aweke kipaumbele katika kufuatilia utekelezaji wa miradi na kusimamia shughuli za mendeleo za Serikali pamoja na zile shughuli mbalimbali za Serikali kama ilivyoainishwa kwenye maandiko mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Salamu za Pole. Katika kipindi hiki cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge lako Tukufu, wapo Watanzania wenzetu waliopatwa na majanga mbalimbali yakiwemo mafuriko yaliyosababishwa na Mvua za *El Ninyo,* maporomoko ya udongo, kimbunga, ajali za barabarani na majanga mengine yaliyosababisha vifo, uharibifu wa miundombinu pamoja na mali. Natumia nafasi hii kutoa salamu za pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wote waliopoteza wapendwa wao. Vilevile, natumia nafasi hii kutoa pole kwa majeruhi wote, namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie uponyaji na kuwapa marehemu pumziko la amani, Amina.

Mheshimiwa Spika, katika huu Mkutano wa Bunge jumla ya Maswali 730 ya Msingi na mengine 2,276 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Pia, jumla ya Maswali 52 ya papo kwa papo yalielekezwa kwa Waziri Mkuu na kujibiwa. Kwa namna ya pekee nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuuliza maswali yaliyolenga kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizowakabili wananchi ambao mnawawakilisha. Aidha, maswali yaliyoulizwa yamewezesha Serikali kuongeza jitihada katika kushughulikia changamoto za wananchi na kuchukua hatua mahsusi kwa lengo la kujenga ustawi wa wananchi. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili pia, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kujadili Miswada mbalimbali iliyoletwa Bungeni na kusomwa kwa mara ya kwanza na mara ya pili na Bunge lako Tukufu kuchukua hatua kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Katika mkutano huu Bunge lako tukufu limepokea Miswada ya Sheria kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024 *(The Written Law Amendment No.2 Bill 2024)* kusomwa kwa mara ya kwanza;

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria zinazohusu Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024;

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2024;

(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 ya Mwaka 2024;

(v) Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 (*The Finance Bill 2024)* ambayo tumeikamilisha muda mfupi uliopita, pamoja na;

(vi) Muswada wa Sheria ya Fedha ya Matumizi ya Mwaka 2024 *(The Appropriation Bill 2024)* ambayo pia tumeikamilisha muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa la Miswada iliyowasilishwa Bungeni na kusomwa ni kuhakikisha tunaendelea kuboresha na kustawisha maisha ya Watanzania ambao wamejenga imani kubwa kwa Serikali na Bunge hili Tukufu, juu ya masuala yote yanayohusu mustakabali wa Taifa letu na kuwapatia ufumbuzi kupitia njia za Kisheria.

Mheshimiwa Spika, wakati wakati Bunge lako Tukufu likiendelea kulitokea matukio kadhaa ambayo kwa mujibu wa taratibu ililazimu Kiti chako kutoa Taarifa kwa umma kwa lengo la kutambua kuguswa na kuthamini mchango uliotokana na walengwa waliosababisha kuwepo kwa taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizotolewa ndani ya Bunge lako Tukufu wakati wa Mjadala wa Bunge hili ni kama ifuatavyo:-

(i) Taarifa kuhusu Kifo cha Mheshimiwa Ahmed Yahaya Abdul-Wakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani, ambaye alifariki ghafla kwa shinikizo la damu, Tarehe 8 Mwenzi wa Nne 2024 na kuzikwa Tarehe 9 Mwezi wa Nne 2024 Kijijini kwao Buyuni Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kutoa pole kwa familia, Wananchi wa Jimbo la Kwahani na Waheshimiwa Wabuge kufuatia msiba huu mzito.

(ii) Taarifa kuhusu kifo cha Mheshimiwa Dkt. Shogo Richard Mlozi aliyekuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Aliyefariki dunia Tarehe 13 Juni, 2024 na kuzikwa Tarehe 17 Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, hapa pia, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwa familia, Watanzania na Wanajumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuondokewa na kiongozi aliyekuwa mstari wa mbele katika kupigania Ustawi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema, Amina.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili Serikali imetoa jumla ya kauli tano kama ifuuatavyo:-

(i) Kauli ya Serikali kuhusu Mikopo ya Kaushadamu;

(ii) Kauli ya Serikali kuhusu Changamoto ya Wanyamapori Wakali na Waharibifu katika Wilaya za Mbarali na Maeneo Mengine Nchini;

(iii) Kauli ya Serikali kuhusu Kimbunga Hidaya kilichotokea Pwani ya Bahari ya Hindi;

(iv) Kauli ya Serikali kuhusu Changamoto za Hali ya Hewa Nchini; na

(v) Kauli ya Serikali kuhusu Kupinga Ukatili Dhidi ya Watu Wenye Ualbino.

Mheshimiwa Spika, tarehe 25 Mwezi wa Nne 2024 na tarehe 9 Mwezi wa Tano 2024, nilitumia Kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu kutoa Taarifa kwa Bunge lako Tukufu kuhusu mwenendo wa matukio ya hali ya hewa, athari zilizotokea kutokana na Kimbunga Hidaya na Mvua kubwa ya *El Ninyo* na

hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali. Hatua hizo ni pamoja na kurejesha miundombinu ya barabara na madaraja yaliyoharibiwa kwa kufanya matengenezo ya dharura, ili kuwezesha barabara kupitika. Aidha, Serikali ilifanya tathmini ya kubaini gharama ya kurejesha mioundombinu iliyoharibiwa.

Mheshimiwa Spika, tathmini hiyo ilionesha kuwa, gharama inayohitajika sasa ni shilingi trilioni 1.07. Kati ya hizo shilingi bilioni 728 ni, kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara na shilingi bilioni 158 ni, kwa ajili ya matengenezo ya dharura. Aidha, shilingi bilioni 184 ni, kwa ajili ya matenegenezo ya dharura na kurejesha miundombinu iliyoathirika kutokana na Kimbunga Hidaya. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali itaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu iliyoharibiwa, ili kuwezesha huduma za usafiri na usafirishaji wa bidhaa kurejea.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufanya Maboresho mbalimbali ya Utumishi wa Umma, ikiwa ni pamoja na kusimika Mifumo ya TEHAMA mahsusi, kwa ajili ya kurahisisha utoaji huduma kwa umma na kushughulikia masuala ya maslahi ya Watumishi wa Umma. Waheshimiwa Wabunge wenzangu sina shaka mtakubaliana na mimi kuwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka alama isiyofutika katika kushuhgulikia masuala ya Maslahi ya Watumishi wa Umma. Kupandisha vyeo watumishi na kubadili mishahara, kulipa malimbikizo ya mishahara, kubadilisha kada mbalimbali za utumishi na kutoa vibali vya ajira kwa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa upandishaji vyeo watumishi, Serikali ya Awamu ya Sita imeweza kupandisha vyeo, madaraja na kuwalipa mishahara jumla ya watumishi 440,316. Licha ya hayo, imebadilisha kada au muundo wa watumishi 6,042 na inaendelea na zoezi la kubadili kada watumishi wengine 7,912 waliosalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kipindi cha kuanzia Machi 2021 hadi Aprili 2024 imelipa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 164,075 ya thamani ya shilingi bilioni 271.07. Aidha, katika kipindi hicho hicho Serikali imetoa ajira mpya na ajira

mbadala kwa watumishi 247,968 pamoja na kutenga nafasi nyingine za ajira za watumishi 47,404. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala ya mafao ya wastaafu; katika kuhakikisha kuwa wastaafu wanalipwa kwa wakati, Sheria za Mifuko zinamtaka mwajiri kuwasilisha taarifa za maandishi kwenye mifuko ndani ya miezi sita kabla mtumishi kustaafu ili mfuko uweze kuanza taratibu za kuandaa mafao ya wanachama. Mifuko nayo inatakiwa ndani ya siku 60 baada ya mwanachama kustaafu iwe imeshamlipa mafao yake yote kama madai yake yalivyokuwa, yakiwa hayana kasoro na michango imewasilishwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2023/2024, 90% ya wadai wastaafu wamelipwa ndani ya muda wa siku 60 kwa Mfuko wa *NSSF* na 61% kwa Mfuko wa *PSSSF*. Sababu ya baadhi ya wastaafu kutolipwa kwa wakati ni pamoja na michango yao kucheleweshwa kuwasilishwa katika mifuko na baadhi ya wastaafu kubadilisha kumbukumbu za utumishi kama vile tarehe za kuzaliwa, majina na muda wa kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya ucheleweshaji wa michango kutoka kwa waajiri, Serikali imewasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mifuko inayolenga kuzipa nguvu Bodi za Wadhamini za Mifuko kupunguza au kusamehe kabisa tozo zinazotokana na ucheleweshaji wa michango. Marekebisho haya yatawezesha waajiri wenye malimbikizo makubwa ya michango kulipa madeni yao na kuhakikisha kuwa wastaafu wanalipwa kwa wakati na kulitumikia Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa waajiri wote kuhakikisha wanalipa michango ya watumishi wao kwa wakati na kuondoa usumbufu wa kucheleweshwa kulipwa kwa watumishi hao pindi wanapostaafu. Aidha, niitake pia Mifuko kuchukua hatua kwa waajiri wanaokiuka kwa makusudi wajibu wao wa kuwasilisha michango kwa wakati. Bodi za Menejimenti za Mifuko tumieni Vifungu vya Sheria katika kuhakikisha kuwa michango inawasilishwa kwa wakati ili kuwaondolea wastaafu changamoto ya kutolipwa mafao yao kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nijielekeze katika utekelezaji wa miradi mikubwa na nianze na miradi ya maji. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali ilipanga kutekeleza miradi 1,790 ya maji ambapo kati miradi hiyo, ya mijini ni 244 na ya vijijini ni 1,546. Hadi kufikia Mwezi Juni 2024, jumla ya miradi 773 ilikuwa imekamilika. Aidha, miradi 1,057 bado iko kwenye hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi hiyo, Serikali inatekeleza miradi mikubwa ya maji ikiwemo Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe. Mradi huo una uwezo wa kuhudumia wananchi 456,900 katika Miji ya Same na Mwanga na vijiji 38 vya vya Wilaya ya Same, Mwanga na Korogwe. Hadi kufikia Juni 2024 utekelezaji umefikia 95% ambapo wananchi wameshaanza kupata maji katika baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi mingine inayotekelezwa ni pamoja na mradi wa maji wa miji 28 wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 500. Utekelezaji wa mradi huo upo katika hatua mbalimbali na utakapokamilika utanufaisha wananchi wapatao milioni 5.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Serikali inaendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda kwa gharama ya shilingi bilioni 329.47. Hadi kufikia Juni 2024, utekelezaji wa mradi umefikia 20.92%. Katika kukabiliana na ulimbikizaji wa madeni ya Ankara za Maji pamoja na utoaji wa Ankara zilizo sahihi kwa wateja. Serikali imeamua kuanza kutumia Dira za Maji za Malipo ya Kabla. Mpaka kufikia Juni 2024, jumla ya dira 12,928 zilikuwa zimeshafungwa kwa wateja mbalimbali hapa nchini. Kwa sasa Serikali inaendelea na uandaaji wa mpango mkakati wa kufunga Dira za Maji za Malipo Kabla ili kufikia 50% ya maunganisho yote ifikapo Disemba 2025.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi wa Reli ya Kisasa *(SGR)*; katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024 Serikali iliendela kuboresha sekta ya uchukuzi kwa kusimamia na kuendeleza sekta ndogo ya reli ikiwemo ujenzi wa *SGR* na ukarabati wa reli iliyopo, *MGR*. Usafiri wa anga, usafiri wa majini,

ujenzi na ukarabati wa meli na uboreshaji wa bandari. Kwa upande wa Reli ya *SGR*, ujenzi wa reli hiyo kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza yenye urefu wa kilometa 1,596 uliogawanyika katika vipande vitano umeendelea kutekelezwa. Ninaomba kulitaarifa Bunge lako Tukufu kuwa, tayari uendeshaji wa treni hiyo kati ya Dar es Salaam na Morogoro umeanza. Aidha, safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma inatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Julai 2024.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwango vya nauli ya Treni ya *SGR*, Serikali imetangaza viwango vya nauli za treni ya abiria ya kawaida kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ambayo ni shilingi 69.1 kwa kilometa kwa treni itakayokuwa inasimama kila kituo. Hivyo, kwa treni hii kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro itakuwa ni shilingi 13,000 na kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ni shilingi 31,000. Aidha, viwango vya nauli kwa treni ambayo itakuwa inasimama vituo vichache takribani viwili vya Pugu na Morogoro *(Express Trein)*, nauli zitakuwa shilingi 112.6 kwa kilometa ambapo kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ni shilingi 22,000 na kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma itakuwa shilingi 50,000.

Mheshimiwa Spika, kipekee ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa msukumo wake wa kuweka kipaumbele katika kuhakikisha kuwa mradi huu unakamilika na kuanza kutoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa taarifa juu ya hali ya upatikanaji wa chakula na uhifadhi wa chakula. Uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo 2023/2024 unatarajiwa kuongezeka kutokana na kuongezeka kwa mvua katika maeneo mengi ya nchi na upatikanaji na matumizi ya mbolea nchini. Mafanikio haya yanatokana na jitihada za makusudi za Serikali kwa kuweka kipaumbele katika kilimo na kutoa ruzuku ya mbolea ili wakulima wapate pembejeo hiyo muhimu kwa bei nafuu. Hakika mchango wake umekuwa chachu katika maendeleo ya sekta ya kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula na upatikanaji wake hapa nchini umeendelea kuimarika. Katika msimu wa uzalishaji wa mwaka 2023/2024, nchi yetu inatarajia kuzalisha mazao ya chakula kiasi cha tani milioni 31.4 ambapo kiasi cha tani milioni 20.3 ni za mazao ya nafaka na kiasi cha tani milioni 11.1 ni cha mazao yasiyo ya nafaka. Hadi kufikia tarehe 24 Juni, 2024, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* umefikisha akiba ya chakula tani 339.995, zikijumuisha mahindi tani 332,772, mpunga tani 6,762 na mtama tani 461. Aidha, hadi kufikia tarehe hiyo, Wakala umetoa chakula cha msaada tani 639 kwa waathirika wa mafuriko yaliyotokana na mvua za *El Nino* katika halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha hifadhi ya chakula ili kuwa na akiba ya kutosha nchini. Nitumie fursa hii kutoa wito kwa wakulima kutumia vizuri mavuno wanayoyapata kuhifadhi kiasi cha mazao ya chakula na kuzingatia kanuni bora za uvunaji na uhifadhi mzuri wa mazao ya chakula ili kupunguza upotevu wa mazao hayo. Aidha, maafisa ugani wote waendelee kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi ya teknolojia za uhifadhi wa mazao ya chakula na matumizi sahihi ya chakula kwenye ngazi ya familia.

Mheshimiwa Spika, ninapozungumzia suala la upatikanaji wa chakula, ongezeko la uzalishaji wa chakula linawiana na mahitaji yetu ambayo ni tani milioni 16 kwa mwaka, mwaka 2023/2024 na tani milioni 17 kwa mwaka, mwaka 2024/2025. Ongezeko hili limejidhihirisha kwenye bidhaa muhimu pia ikiwemo na bidhaa ya sukari. Mahitaji ya sukari yameendelea kuongezeka kutoka tani 550,000 mwaka 2023/2024 na kufikia tani 640,000 mwaka 2024/2025, sawa na mahitaji ya tani 45,000 kwa mwezi. Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba kiasi hicho cha sukari kinakuwepo nchini na kuwa na *buffer stock* ya miezi miwili kila wakati ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa sukari kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuzalisha tani 700,000 ifikapo Mwaka wa Fedha 2025/2026 ili kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya sukari hapa nchini. Kwa msingi huo,

Serikali itaendelea kusimamia uzalishaji wa ndani ili kukidhi mahitaji ya sukari nchini. Aidha, katika kipindi hiki ambacho uzalishaji wa ndani hautosholezi mahitaji, Serikali itaendelea kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha kwamba upatikanaji wa bidhaa hii muhimu kwa wananchi unakuwa wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; Serikali imeendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ambapo Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, hadi kufikia Juni, 2024 jumla ya wanafunzi 224,056 wamepatiwa mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 743.2, sawa na 94.6% ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mikopo kwa ngazi ya Stashahada, Shahada ya Awali, Stashahada ya Juu ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo, Shahada za Umahiri na Uzamivu na Ufadhili wa *Samia Scholarship* katika masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bunge lako Tukufu limepitisha kiasi cha shilingi bilioni 787 kwa ajili ya kukopesha wanafunzi 250,000, ikijumuisha wanafunzi wapya wa shahada ya kwanza wapatao 80,000. Aidha, maandalizi ya awali yameanza ikiwa ni pamoja na kusambaza Mwongozo wa Upangaji na Utoaji Mikopo, kufungua dirisha la uombaji mikopo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa muda wa siku 90 kuanzia tarehe 01 Juni hadi 31 *August*, 2024. Pia tunaendelea na kutoa elimu kwa waombaji mikopo na wadau wengine vilevile.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa urejeshaji mikopo, Bodi ya Mikopo imeendelea kukusanya mikopo iliyoiva kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Serikali ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 230 ambapo hadi kufikia mwezi Mei 2024 jumla ya shilingi bilioni 161 zilikusanywa, sawa na 70% ya lengo.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba ukusanyaji wa mikopo hiyo, Serikali imeweka mikakati kadhaa ikiwemo kuwakumbusha waajiri kuwasilisha majina ya wanufaika ndani ya siku 28 baada ya kuwaajiri. Pia, kushirikiana na kuunganisha mifumo na wadau wa kimkakati kama vile *NIDA*, *TRA*, taasisi

binafsi za ndani na nje ya nchi, kufanya kampeni za kuwafichua wanufaika, kutoa elimu kupitia mitandao ya kijamii na kufanya kaguzi kila mwezi kwa waajiri wa sekta za umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa mikopo inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri; ikumbukwe kwenye mwezi Aprili 2023 Serikali ilisitisha utoaji wa mikopo wa 10% kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Hadi kufikia mwisho wa Mwaka huu wa Fedha 2023/2024, Serikali imekamilisha maandalizi ya uratibu na upelekaji wa fedha za mikopo ya 10% katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwenda kwenye Mfuko wa Mikopo ya Vikundi na kusimamia urejeshwaji wa mikopo iliyotolewa wa miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, Mwaka wa Fedha 2024/2025 Serikali imepanga kutoa mikopo takribani shilingi bilioni 228 ambapo shilingi bilioni 63.7 ni fedha za marejesho zitakazokuwa zikiendelea kukusanywa kutokana na mikopo iliyotolewa kabla ya kusimamishwa Mwezi Aprili 2023. Shilingi bilioni 63.2 ni fedha zilizokuwa zinatengwa kwa ajili ya mikopo na shilingi bilioni 101.1 ni fedha ambazo zimetengwa kutokana na makisio ya makusanyo ya mapato ya ndani kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga utaratibu wa kutumia benki kwa halmashauri 10 za majaribio ambazo ni Majiji ya Dar es Salaam na Dodoma, Manispaa za Kigoma Ujiji na Songea, Miji ya Newala na Mbulu, Wilaya za Siha, Nkasi, Itilima na Bumbuli. Aidha, halmashauri 174 zilizobaki zitatumia utaratibu ulioboreshwa, ikiwemo uanzishwaji wa kitengo cha usimamizi wa mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika Ofisi za Rais - TAMISEMI na uanzishwaji wa Kamati za Usimamizi wa mikopo hiyo katika ngazi za Ofisi za Wakuu wa Wilaya, halmashauri na kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe taarifa ya fidia ya ardhi maeneo yanayotwalia na Serikali kwa uwekezaji; Serikali imeendelea kutwaa maeneo kwa ajili ya miradi yenye manufaa ya umma kwa malengo ya uwekezaji na miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa

barabara, viwanja vya ndege, uchimbaji wa madini na maeneo mengine muhimu kwa uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kwa nyakati tofauti kumekuwepo malalamiko ya wananchi kucheleweshewa malipo ya fidia katika baadhi ya maeneo. Katika kuhakikisha kuwa malalamiko haya yanatatuliwa, ninazielekeza taasisi zote kuhakikisha kuwa zinatenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kulipa fidia kabla ya kuanza zoezi la utwaaji wa ardhi, kama inavyoelekezwa katika Waraka wa Uthamini wa Fidia Na. 1 wa mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi. Serikali yetu ilisaini mkataba na Benki ya Dunia kiasi cha shilingi bilioni 346, kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi siku ya tarehe 21 Februari, 2022. Malengo makuu ya mradi ni kuimarisha usalama wa milki za ardhi na kuwezesha miundombinu ya usimamizi wa ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mradi unatekelezwa kupitia vipengele vinne ambavyo ni kuongeza usalama wa milki za ardhi kwa kutoa hati milki 1,000,000 katika maeneo ya mijini kwa njia ya urasimishaji wa hati za milki za kilometa 500,000. Pia, kuimarisha mifumo ya taarifa za ardhi, kujenga miundombinu ya ardhi na usimaizi wa mradi. Mradi huu unatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano; mwaka wa fedha 2022/2023 – 2026/2027 katika halmashauri 67 na mikoa 26.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 15 Juni, 2024 kazi zilizotekelezwa kupitia mradi huu katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni pamoja na: urasimishaji wa vipande vya ardhi 62,200 katika halmashauri mbalimbali; usimikaji wa alama za msingi za upimaji 327 katika halmashauri 26; upimaji na uhakiki wa mipaka ya vijiji na uandaaji wa vyeti vya ardhi ya vijiji 843 katika halmashauri 21; pia uandaaji wa hati milki za kimila 381,509.

Mheshimiwa Spika, aidha mradi umewezesha kununuliwa magari 18 ambayo yanatumika sasa kutekeleza mradi maeneo

mbalimbali nchini na taratibu za ununuzi wa magari mengine 52 zinaendelea na yanatarajiwa kuwasili Septemba 2024. Hatua hii itapunguza changamoto kubwa ya usafiri iliyopo katika sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuendelea kuzisisitiza Mamlaka za Upangaji Miji chini ya uratibu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kuendeleza kasi ya utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi kwa ufanisi ili fedha zilizopangwa kutumika kwenye mradi ziwe na tija.

Mheshimiwa Spika, kadhalika kupunguza migogoro kupitia uhakiki wa upimaji wa mipaka ya vijijini, maandalizi ya mipango ya matumizi ya ardhi na vijiji, kuandaa mipango kazi ya vijiji na kuandaa hati za hati milki za kimila, kurasimisha vipande vya ardhi, kubadilisha nyaraka za ardhi kutoka analojia kwenda kidigiti na kusanifu na kusimika vituo vya kielektroniki vya upimaji. Nitoe wito kwa wananchi hususan wa maeneo ya vijijini kuchangamkia fursa za uwepo wa mradi huo kurasimisha maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, maboresho ya mazingira ya biashara hapa nchini; Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuhakikisha inaboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, imetekeleza afua mbalimbali za kikodi na kiutendaji. Hata hivyo kumekuwa na changamoto ambazo zimeendelea kujitokeza na hivyo kusababisha taharuki na sintofahamu nyingi hasa kwa wafanyabiashara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sintofahamu hizo kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge walivyochangia humu Bungeni katika siku za hivi karibuni ni pamoja na migomo ya wafanyabiashara wetu kutoka katika maeneo tofauti hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ifahamike kwamba sehemu kubwa ya madai ya wafanyabiashara wetu inatokana na hoja takribani 41 ambazo ziliwasilishwa na viongozi wa jumuiya ya wafanyabiashara Tanzania. Kati ya hizo hoja sita zilikuwa ni za

kisera na kisheria na zilizobaki 35 ni za kiutendaji. Serikali imeweza kufikia muafaka katika kutatua kero za wafanyabiashara nchini, Serikali ipo pamoja na uongozi wa jumuiya ya wafanyabiashara nchini, wameafikiana kusimamia maazimio kama yalivyowasilishwa na Msemaji Mkuu wa Serikali, baada ya kikao cha mwisho.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii mbele ya Bunge lako Tukufu kuziagiza mamlaka zote za Serikali kuhakikisha kuwa maazimio yote yaliyofikiwa yawezekutekelezwa kwa ufasaha na kwa wakati uliyokubalika na pande zote, yaani muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Kadhalika mamlaka husika ziendelee kushirikiana na uongozi wa jumuiya ya wafanyabiashara Tanzania katikakuhakikisha kwamba kero na changamoto mbalimbali za wafanyabiashara zinatatuliwa.

Mheshimiwa Spika, wito hapa kwa mamlaka zote zinazoshughulikia biashara, wafanyabiashara wasikilizwe na kuona namna bora ya utatuzi wa changamoto pale zinapojitokeza. Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati wote itaendelea kuwapokea, kuwasikiliza na kuthamini shughuli za biashara na mchango wao mkubwa katika kukuza uchumi wa Taifa letu. Niwahakikishie wafanyabiashara wote wadogo kabisa, wadogo na wa kati na wakubwa, kuwa Serikali hii inadhamira ya dhati ya kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wanafanya shughuli zao kwa mafanikio ili waweze kujipatia kipato na kuchangia katika uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kwa kifupi utekelezaji wa kampeni ya matumizi safi ya nishati safi, nitumie Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa wadau wote, ikiwemo Wizara za kisekta, taasisi za umma, idara za Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, asasi za kiraia, sekta binafsi, washirika wa maendeleo, waheshimiwa wabunge na watanzania wote kushiriki kikamilifu katika mkakati wa utekelezaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ili Taifa letu liweze kufikia malengo ya kuimarisha utunzaji wa mazingira pamoja na kuboresha afya na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, kampeni juu ya matumizi ya nishati safi inaendelea kote nchini, maelekezo thabiti yameshatolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais na Mazingira, miongozo yote inaendelea kusimamiwa na taarifa na elimu juu ya matumizi ya nishati safi yataendelea kutolewa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nikumbushe juu ya maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kama unavyofahamu kuwa mwaka huu nchi yetu itafanya zoezi la kidemokrasia la uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Serikali kwa kutambua umuhimu wa uchaguzi huo kwa maendeleo ya Taifa letu inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za maandalizi, hatua hizo ni pamoja na kukamilisha kazi zote muhimu zilizopaswa kutekelezwa kabla ya kutangazwa rasmi kwa kuanza mchakato wa uchaguzi huo. Hadi sasa kazi zinazotekelezwa ni pamoja na kuhakiki maeneo ya utawala na kufanya maandalizi ya kanuni za uchaguzi ambayo yapo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji.

Mheshimiwa Spika, maandalizi yanaendelea hivyo basi niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuhamasisha wananchi kushiriki zoezi la maboresho la daftari la mpigakura pamoja na kujiandikisha. Vile vile nielekeze viongozi wote kuanzia ngazi ya vijiji, mitaa, kata, wilaya na mikoa kuhakikisha wanasimamia zoezi la kuhamasisha na kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kujiandikisha na kufanya maboresho la daftari la mpigakura kwa wananchi ili kuwa na ufahamu na uelewa wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu naomba nisisitize masuala yafuatayo: -

(1) Itakumbukwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 26 Juni, 2024 Bunge lako Tukufu lilipitisha kwa kishindo Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Ni wahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba, Serikali itatekeleza bajeti hii kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano 2021/2022 hadi 2025/2026 wenye dhima ya kujenga uchumi

shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu pamoja na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi niwakumbushe viongozi wa wizara na taasisi zilizo chini yao kuzingatia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025: -

Kwanza, Maafisa Masuuli wazingatie waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma namba mbili wa mwaka 2021 kuhusu utaratibu wa kutumia magari aina stahiki za magari kwa viongozi katika utumishi wa umma kwa lengo la kupunguza matumizi Serikalini. *(Makofi)*

Mbili, katika kuhakikisha malengo ya ukusanyaji mapato ya Serikali yanafikiwa, nazielekezwe taasisi zilizopewa dhama ya kukusanya mapato ya Serikali, kuendelea kutumia mifumo rasimi na kuhakikisha kodi stahiki inalipwa kwa mujibu wa sheria kama alivyosisitiza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tatu, taasisi zote za Serikali kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma namba 10 ya mwaka 2023, inayoelekeza kutoa kipaumbele kwa bidhaa au huduma zinazotengenezwa au kuzalishwa ndani ya nchi katika mikataba inayotolewa kwa misingi ya ushindani wa zabuni za kitaifa na za kimataifa ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni na kukuza viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la michezo kidogo. Sina shaka waheshimiwa wabunge wenzangu mtakubaliana nami kuwa Sekta ya Michezo imeendelea kukua kwa kasi kubwa hapa nchini, hii inatokana na msukumo mkubwa wa Serikali Awamu ya Sita ambayo sote ni mashuhuda wa jitihada kubwa zinazofanywa ambazo zimekuwa chachu ya ukuaji wa maendeleo ya sekta ya michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, wakati wote amekuwa kinara katika kuhakikisha wanamichezo wetu wanapata motisha

pamoja na rasilimali muhimu ili waweze kuwakilisha vema Taifa letu katika mashindano ya kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imepata heshima ya kuwa wenyeji wa mashindano ya Kombe la Mataifa ya *AFCON* mwaka 2027, yanayotarajiwa kufanyika nchini kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda. Katika kufanikisha mashindano hayo kwa viwango vinavyotarajiwa, Serikali imekamilisha maandalizi ya mpango mkakati wa kitaifa wa *AFCON 2027*. Mpango mkakati huo umejumuisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu, uendelezaji wa masoko ya utalii, uandaaji wa timu yetu ya Taifa, ulinzi na usalama pamoja na mpango wa matangazo na hamasa kwa umma.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mkakati huo, Serikali imeandaa mpango kazi utakaowezesha utekelezaji wa malengo yote yaliyobainishwa katika mpango mkakati huo.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Serikali kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)* imeanza kuweka mikakati ya maandalizi ya timu yetu ya Taifa kuelekea mashindano haya ya *AFCON* 2027. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na kuanzisha programu za kuendeleza vipaji kwa kushirikisha timu za vijana waliyochini ya umri wa miaka 17, miaka 20 na miaka 23 pamoja na kutumia wachezaji wa *diaspora*.

Mheshimiwa Spika, mipango mingine ni pamoja na kuboresha mipango mikakati ya upatikanaji wa vifaa mbalimbali vya michezo, kuandaa mabenchi ya ufundi yaliyobora, kuandaa programu za lishe na kugharamia malipo ya kocha wa Timu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo ya *golf*, nataka nianze kwa kumpongeza mwanadada shupavu Madina Iddi, aliyepata ushindi wa kwanza wa jumla kwenye mashindano mawili ya *Ghana Ladies Open* kwenye *gross champion category* iliyofanyika Yaounde Cameroon, pamoja na mashindano ya Kenya *Coast Ladies Open tournament*, mchezaji huyu anayechezea timu ya Taifa ya *golf* wanawake kadhalika alipata

ushindi wa nafasi ya pili wa jumla katika mashindano mengine mawili ya Uganda *Ladies Open* yaliyofanyika nchini Uganda pamoja na mashindano ya *golf* wanawake Afrika Mashariki na kati yaliyofanyika Kigali nchini Rwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ilipata ushindi wa nafasi ya kwanza kwenye shindano la *golf* wanawake la nchi za Afrika Mashariki na Kati lililoshirikisha nchi saba, nawapongeza sana wanamichezo waliowakilisha ambao ni Neema Olomi, Hawa Manyeche, Madina Iddi na Vicky Eliasi. Nitumie nafasi hii kuzipongeza sana timu za mchezo wa *golf* za wanawake na nitoe rai kwa wadau wa michezo kuwapa ushirikiano wachezaji wetu hawa wanaouhitaji ili wazidi kupeperusha bendera ya Tanzania, kazi yao ni njema, Serikali na wadau wataungana pamoja kuwawezesha ili waendelee kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie mchezo wa ngumi, riadha na mchezo wa kuogelea pamoja na kareti. Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya ngumi kimataifa, ushindi huu umepatikana na mchezaji mmoja mmoja na kwa timu zilizoshiriki katika mashindano hayo, nianze kwa kuipongeza sana Timu ya Taifa ya ngumi za wazi kwa kufanikiwa kutwaa medali tatu za shaba katika mashindano ya *All African Games* yaliyofanyika nchini Ghana mwezi Machi mwaka huu 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia mwanamasumbwi Yusuph Lucas Changalawe, mcheza ngumi za ridhaa aliyeshinda kwa *knock out* baada ya kumtwanga Pereira Diego wa Venezuela katika pambano la kwanza la dunia la kufuzu *Olympic* ya Paris 2024. Natoa pongezi nyingi kwa mwanamasumbwi mwingine Hassani Mwakinyo mchezaji ngumi za kulipwa aliyeshinda ubingwa wa *WO Africa* katika pambano lililofanyika Januari 2024 hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza sana mwanariadha Josephat Joshua Gisemo, aliyeibuka kidedea kwa kushinda nafasi ya kwanza katika mbio za kilometa 10 zilizofanyika Januari 2024 huko nchini Brazil. Ninampongeza sana kwa ushindi

huo mkubwa ambao umeendelea kuipaisha nchi yetu katika medani za kimataifa. Vilevile nampongeza mwanariadha Gabrieli Geay, Alphonce Simbu, Magdalena Shauri na Jackline Sekilu ambao wamefuzu kushiriki mashindano ya *Olympic* yatakayofanyika Jijini Paris Ufaransa Julai 2024. Wanariadha hawa wameendelea kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali na wanazidi kung'ara katika mashindano mbalimbali ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mchezo wa kuogelea Timu ya Taifa ya mchezo wa kuogelea ilishinda nafasi ya pili kati ya nchi 13 zilizowania ubingwa katika mashindano ya *Aquatic Zone III Championship* yaliyofanyika Kigali nchini Rwanda. Nawapongeza sana kwa ushindi huo pia naipongeza Timu ya Taifa ya kuogelea ya vijana iliyoshinda na kufikia hatua ya fainali katika mashindano ya vijana ya Afrika, *Africa Aquatics Junior Championship,* yaliyofanyika nchini Mauritius.

Mheshimiwa Spika, Timu ya Taifa ya Kareti ilipata ushindi mnono na kunyakua jumla ya medali 45 zikiwemo medali mbili za dhahabu, medali saba za fedha na medali 36 za shaba baada ya kushika nafasi ya tatu katika mashindano ya kareti ya nchi za maziwa makuu yaliyofanyika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, nawapongeza sana washiriki wote kwa kupeperusha bendera ya Taifa letu na kuleta heshima kubwa katika mchezo wa kareti.

Mheshimiwa Spika, siachi kuipongeza pia *Bunge Sports Club* ambayo inashirikisha Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ninawapongeza kwa kushiriki kwenu kwenye michezo mbalimbali kupitia *Bunge Sports Club* lakini pia na *Bunge Marathon* ikiwa ni njia sahihi ya kujiimarisha kiafya, kuongeza vipaji lakini pia kuimarisha ushirikiano miongoni mwetu. Tunaendelea kutakia mema *Bunge Sports Club* ili iendelee kuratibu michezo mingi zaidi na tuweze pia kushiriki kwenye michezo ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie mpira wa miguu. Naomba nianze kwa kuipongeza Timu yetu ya Taifa maarufu kwa jina la Taifa Stars kwa kushinda mchezo wa kuwania kufuzu kombe la dunia mwaka 2026, ushindi huo ulipatikana baada ya kuichapa

kwa bao moja bila timu ya Taifa ya Zambia maarufu kama 'Chipolopolo' katika pambano lililofanyika hivi karibuni jijini Ndola. Ushindi huo unaipa Taifa Stars nafasi nzuri ya kufuzu mashindano ya kombe la dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuzipongeza klabu zetu za hapa ndani ya nchi Yanga na Simba kwa kushiriki na kufikia hatua ya robo fainali katika mashindano ya Klabu Bingwa Barani Afrika, sote tumeshuhudia timu hizo zikiendelea kuliheshimisha Taifa letu na kuzidi kuongeza umaarufu wake. Natoa pongezi nyingi kwa wachezaji, mabenchi ya ufundi, viongozi na wanachama wa vilabu hivyo, sina shaka umoja na mshikamono wa Taifa hili unaimarika zaidi kwa michezo hii kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe wito kwa wapenzi wa michezo na wanamichezo wote tuendelee kuimarisha michezo na hasa katika kuimarisha uongozi wa vilabu vyetu ili viweze kuwa chachu ya kufikia hatua kubwa zaidi ya timu zetu za Taifa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii basi nipongeze angalau klabu moja moja nikianza na Klabu ya Yanga kwa kufanikiwa kunyakua... *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie, basi na mimi nitumie nafasi hii kuzipongeza timu zetu za hapa ndani, nianze kwa kuipongeza Klabu ya Yanga kwa kufanikiwa kunyakua Kombe la Ligi Kuu, kwa kunyakua Kombe La Ligi Kuu ya *NBC* na Kombe la Shirikisho la *CRDB*, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuipongeza Timu ya *Simba Sports Club* kwa kunyakua Kombe la Muungano, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia matokeo haya niendelee kuzipongeza timu ya Yanga na Azam kwa kufanikiwa kufuzu kuiwakilisha nchi kwenye mashindano ya Klabu Bingwa Afrika msimu ujao lakini vile vile nichukue nafasi hii kuzipongeza timu za

Simba na *Coast Union* nazo kwa kufuzu kuwakilisha nchi yetu kwenye mashindano ya kombe la shirikisho msimu ujao, tunazitakia kila la heri kwenye mashindano hayo na tunahitaji kupata ushindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa na shukrani za dhati nimalizie hotuba yangu kwa kutoa shukrani na pongezi za pekee kwako wewe Mheshimiwa Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Spika wa Mabunge ya Dunia, kwa namna mlivyoweza kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi na maarifa na kutuwezesha kukamilisha mijadala yenye manufaa makubwa kwa nchi yetu, aidha niwapongeze na kuwashukuru waheshimiwa Naibu Spika na wenyeviti wa Bunge letu na uwongozi mahiri uliyouonesha katika kusaidia kuongoza vikao vya Bunge hili muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii pia kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kunisaidia kazi na kuhakikisha kwamba uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu unaimarika na kutoa miongozo katika nafasi zetu za wizara mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, ambaye pia ni msimamizi wa shughuli za ndani ya Bunge kwa upande wa mawaziri na kuratibu shughuli zote za uchangiaji hapa ndani ya Bunge letu. Vilevile nataka nitumie nafasi hii kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuhakikisha kuwa anatoa mwongozo wa kisheria na kuhakikisha kuwa uwasilishaji wa Miswada na shughuli nyingine za utungaji sheria zinaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, ambaye pia ameendelea kunisaidia kazi katika kuhakikisha kwamba tunaratibu maeneo haya yote ya uratibu wa Serikali hapa ndani ya Bunge. Niendelee kuwashukuru waheshimiwa mawaziri wote, Naibu mawaziri wote na watumishi

wa Ofisi ya Waziri Mkuu, wakiongozwa na Katibu Mkuu, bwana Jonath James ambaye pia ameungana na watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika kuandaa taratibu zote zinazotakiwa kuhakikisha kwamba Bunge letu linaendelea vizuri. Kwa heshimiwa kubwa nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano wenu wakati wote wa Bunge hili kuweza kutoa michango yenu ya thamani ambayo imewezesha Serikali yetu kujielekeza kuelekea kutekeleza bajeti ambayo mmeipitisha kwa nguvu moja ndani ya Bunge letu hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niendelee kuwashukuru Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, dada yetu Mheshimiwa Nenelwa na watumishi wote wa Bunge kwa kuhakikisha wanatupatia huduma nzuri iliyotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa muda wote tulipokuwa hapa Bungeni. Vilevile nitoe shukrani kwa mamlaka zote zilizopo Dodoma na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kuhakikisha kunakuwa na utulivu wakati wote kwa kipindi cha Bunge hili la bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe shukurani zangu za dhati kwa watumishi wa Serikali, idara mbalimbali, taasisi za Serikali na wadau kutoka sekta binafsi walioshiriki katika kuhakikisha kuwa Bunge hili linakamilika; wakiwemo wanahabari, watoa huduma mbalimbali na madereva wetu kwa kazi yao nzuri na huduma walizotoa katika kipindi ambapo Bunge letu ilikuwa likiendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninawatakiwa kila la heri Waheshimiwa Wabunge wenzangu mnapoelekea kwenye majimbo na kuwatakiwa baraka tele katika majukumu yenu ya kila siku ya kuwatumikia wananchi. Nikiwa na imani kuwa yote tuliyoyajadili hapa Bungeni yatawafikia Watanzania kupitia mikutano mbalimbali mtakayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge kwa pamoja tumeonesha umoja na utayari wakati wote katika kipindi hiki cha Bunge na hasa katika kusukuma mbele maendeleo ya Taifa letu.

Hivyo, tuendelee kushirikiana kwa pamoja katika kutekeleza na kufanikisha malengo tuliyoyadili hapa Bungeni. Serikali inapenda kuwahakikishia kuwa itaendelea kutoa ushirikiano wakati wote mnapokuwa kwenye maeneo yenu ya huduma kwa wananchi. Kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo. Sasa napenda kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 27 Agosti, 2024, Siku ya Jumanne Saa 3.00 Asubuhi tutakapokutana tena katika ukumbi huu hapa Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. Sasa kwa hii minong'ono inaashiria kwamba likizo ni fupi. Kwa hiyo, ingeongezwa kidogo. Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa majaliwa kuhusu hoja ya kuahirisha Bunge waseme ndiyo, wasioafiki waseme siyo. Nadhani walioafiki wameshinda. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana, Waheshimiwa Wabunge.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc*, – KATIBU WA BUNGE:**

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

*(Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Waheshimiwa Wabunge, ametusomea hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu hoja ya kuahirisha Bunge ikiwa inaashiria kufika kwetu mwisho katika vikao mbalimbali ambavyo tulikuwa navyo katika mkutano wetu huu ambao ni maalumu kwa ajili ya Bajeti. Mambo machache kisha tutaahirisha Bunge. La kwanza ni tangazo la wageni waliopo hapa Bungeni.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambaye ni dereva mwanamke anayeendesha *bulldozer* kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 21 wa Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari Chandama kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Chemba Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Lipo pia tangazo la kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba maandalizi ya Jarida la Bunge Toleo la Saba la mwezi Juni, 2024 yamekamilika. Jarida hili limeangazia Mkutano wa Bajeti unaoendelea, baadhi ya shughuli za Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Ushiriki wa Bunge Kimataifa pamoja na matukio mbalimbali yaliyotokea. Aidha, jarida hili limebeba makala elimishi kuhusu masuala ya kibunge.

Waheshimiwa Wabunge, jarida hilo limewekwa kwenye vishikwambi vyenu ninyi nyote Waheshiwa Wabunge kwa ajili ya rejea. Kwa hiyo ni muhimu Waheshimiwa Wabunge kulitazama. Jarida hili limeeleza mambo mengi sana humo ikiwa ni pamoja na haya ya Bajeti ya Serikali, ambayo kwa mujibu wa Jarida hili, na ninafikiri sote tutakuwa tunakubaliana nayo, inasema Bajeti ya 2024 kuleta neema kwa Watanzania. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tulipitie jarida hili. *(Makofi)*

Jambo lingine Waheshimiwa Wabunge nimeletewa ujumbe hapa kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha bado kuna changamoto ya fedha za Mfuko wa Jimbo kwa Waheshimiwa Wabunge ambao bado hizo fedha hazijawafikia. Na sasa kwa sababu ndiyo tunafika mwishoni mwa mwaka wa fedha basi

utazame namna ambavyo hilo jambo litaweza kufanyiwa kazi. Pia wakati tukivuka mwaka basi utatazama namna ya kulifanya kama ambavyo umetoa ufafanuzi mara kadhaa. Waheshimiwa Wabunge wameileta hoja kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tafadhali uifanyie kazi ili Waheshimiwa Wabunge ahadi walizozitoa kupitia fedha hizo ziweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na Serikali katika mambo ambayo pia yalizungumzwa kwa kirefu sana na Kamati zetu za Kudumu za Bunge kwa kweli mengi wameyafanyia kazi na tumeona mengi yameingia kwenye huu Muswada ambao tumeupitisha leo. Sasa pamoja na kwamba hayakupita vile ambavyo pengine yote tuliyatarajia lakini ni dhahiri Serikali imeonesha nia njema ya kuanzia mahali, halafu kuendelea kusonga na kupiga hatua. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa katika hayo yote yapo mambo ambayo yalizungumzwa kwa nguvu sana na Kamati ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi; samahani Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu Taasisi zetu za *TANAPA* na *NCAA;* na nimeona kwenye sheria Serikali imeleta marekebisho ambayo Bunge limekwishaipitisha. Ni hatua nzuri kwa kuanzia halafu nafikiri sasa ndani mwaka huu kadiri utekelezaji utakavyokuwa unaendelea tutaona kama marekebisho haya yanatosheleza kwenda na kasi ambayo Mheshimiwa Rais aliianzisha kwa *Royal Tour*. Kwa kupokea wageni wengi na fedha nyingi ambazo zinaingia, kwa mujibu wa taarifa ambazo tunaendelea tuzipokea, ni dhahiri kwamba mabadiliko yanahitaji kufanyika ili wenzetu ambao wanafanya kazi katika hili eneo ambalo Mheshimiwa Rais alianzisha hizo juhudi za kuhakikisha tunapata wageni wengi, basi na sisi tuungane nao katika kuhakikisha wanakuwa na fedha kwa ajili ya kuhudumia maeneo ambayo wageni hawa wanayatembelea.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kazi nzuri aliyoifanya kipindi chote cha Bunge hili la Bajeti. Amenisaidia pakubwa sana na kwa hiyo ninamshukuru sana. Pia wapo wasaidizi wetu wengine mimi na

Mheshimiwa Naibu Spika ambao nao kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, tunakushukuru sana. Ahsante sana. Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama tunakushukuru sana kwa kazi nzuri. Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, ahsante sana. Tunawashukuru sana kwa kweli kwa kuendesha vikao kwa umahiri kabisa, na kweli Wabunge wote wanaridhika na huduma ambayo mmeitoa hapa. Kwa hiyo ninawashukuru sana kwa usaidizi mzuri. Waheshimiwa Wabunge hawa ndio wananiwezesha kufanya na majukumu mengine pia. Kwa hiyo ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pamoja na hayo nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge; kipindi hiki kilikuwa ni kigumu kwao lakini wamefanya kazi hii kwa ufanisi mkubwa wakisaidiwa na Makamu Wenyeviti wote. Tunawashukuru kwa kazi nzuri, kwa sababu Bunge letu kwa sehemu kubwa linafanya kazi kwenye Kamati. Kwa hiyo ahsanteni sana kwa kuzisimamia Kamati. Kipindi hiki mlianza kwa kwenda kufanya ziara maeneo mbalimbali. Mliziongoza Kamati kwenda huko ili kuangalia utekelezaji wa Bajeti ya mwaka huu ambao tunamalizia. Mmefanya ziara nzuri mmetembelea miradi, mmetembelea mambo mbalimbali huko ambayo Serikali inayafanya. Tunawashukuru sana kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nanyi ninawashukuru wote kwa pamoja; ahsanteni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya. Kwa kweli mmesoma, mmesoma, mmesoma. Na katika huko kusoma sana kumewafanya muwe na michango mizito sana humu ndani; na kama mlivyosikia Serikali ilivyokuwa inafanya marekebisho hapa na pale ni kuashiria kwamba Wabunge kwa kweli wameyasoma yale waliyokuwa wanayachangia hapa ndani. Kwa hiyo, nawashukuru wote, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni mashahidi kwamba kazi hizo zote zisingewezekana kama si kazi nzuri ya Katibu wa Bunge, Ndugu yetu Nenelwa Mwihambi, tunakushukuru sana kwa kazi nzuri ambayo umeifanya. Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa bahati mbaya mimi nimesimama hapa. Kwa hiyo,

anashindwa kusimama kupokea makofi yenu lakini anawashukuru sana Katibu wa Bunge kwa heshima ya makofi mengi hayo. *(Makofi/ Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge pamoja na watumishi wote walio chini ya ofisi yako tunawashukuru sana kwa ushirikiano ambao wameutoa kipindi chote hiki bila kuchoka, na kweli wamejitahidi sana, kwa hiyo tunakushukuru sana. Lakini sasa pamoja na kwamba umepigiwa makofi mengi hayana uhusiano na kuongezewa malipo yoyote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo kwa kweli haya yote tunayoyasema hapa yasingewezekana kama ingekuwa haitoi ushirikiano ule ambao unastahili. Kwa hiyo ninawashukuru sana Serikali yote, kuanzia Mheshimiwa Rasi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunamshukuru sana kwa ushirikiano mkubwa anaotupa sisi kama Bunge na pia kwa namna ambavyo safari hii ametengeneza historia kabisa kwa kuwa pamoja nasi wakati Bajeti Kuu ya Serikali ikisomwa. Kwa hiyo tunamshukuru sana kwa kuendelea kuwa pamoja nasi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa pamoja na hayo kiongozi wetu wa shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, tunakushukuru pia kwa ushirikiano unaotupa. Ahsante sana. Katika Bunge hili pia tumeshuhudia ukiongezewa nguvu kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge viongozi wetu hawa wametusaidia upande wa Serikali kuiongoza vizuri hapa Bungeni na mambo kwa kweli yamekwenda vizuri. Mawaziri, Naibu Mawaziri wamejitahidi kwa sehemu kubwa sana kuhudhuria vikao vya Kamati na hatujapata changamoto safari hii. Kwa hiyo tunawashukuru sana, kwa usimamizi mzuri. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo niwashukuru sana Mawaziri wote kwa ushirikiano ambao mmeutoa kwa kwenye Kamati. Naibu Mawaziri na wakati mwingine Mawaziri mmejibu maswali mengi sana ya Waheshimiwa Wabunge hapa. Ninawashukuru Mawaziri kwa usimamizi wa jumla Wizara zenu pamoja na Watendaji wote wanaofanya kazi nchi yenu, ahsanteni sana kwa ushirikiano mlioutoa kwa Waheshimiwa Wabunge na Kamati zetu. Mpaka kufia hapa tulipofika leo ni dhahiri kwamba kazi nzuri imefanyika. Pia, utayari wenu wa jumla wa kusikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge na wakati mwingine wanakuja kwenye viti vyenu mnasikiliza hoja zao. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya shukurani hizo ambazo tumezitoa nitumie pia fursa hii kuwapa taarifa ya mambo machache. La kwanza kabisa ni kwamba Bunge hili limevunja rekodi kwa idadi ya wageni waliokuwa wanakuja kututembelea hapa Bungeni. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge leo hapa tumehitimisha zoezi la Mkutano wa Bunge letu hili ambalo kimsingi ni la Bajeti; na napenda kuwataarifu kwamba wageni wetu sisi Waheshimiwa Wabunge walikuwa 48,978. Kwa hiyo hawa ndio waliopata nafasi ya kutembelea Bunge, na hawa waliopo hapa ndani leo ndio wanafunga hii idadi ya hawa wageni. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili mafunzo hawa walikuwa 15,474. Kwa hiyo na wao ni wengi kwa kweli, na hawa wamekuja kutazama namna tunavyofanya kazi. Kwa hiyo kupata wageni wengi maana yake wengi wangependa kuona namna tunavyofanya kazi, lakini maana yake wanaridhika na kazi nzuri inayofanywa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wapo pia wageni waliotembelea Bunge kutoka mabunge mengine na wengine kutoka mabunge ya nje ya nchi. Hawa ni wageni 85 ambao wametoka mabunge mengine wengine walitoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wageni wengine walitoka nchi za Uganda, Zambia, Indonesia, Malawi na Namibia. Wote hawa walikuja kwenye ziara za kujifunza lakini pia kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na Wabunge wenzao hapa. Kwa hivyo wageni kwa kweli tulikuwa nao wengi. Sasa hapa ukiongeza na waliotembelea Bunge, kwa maana

taasisi za Kiserikali zilikokuja hapa kwenye maonesho hapo hawapo.

Takwimu zinaonesha jumla ya wageni 555 walikuja kutoka upande wa Serikali kuja kwenye maonesho. Pia taasisi na watu binafsi ambao wamekuja kwa ajili ya maonesho mbalimbali na kutueleza huduma wanazozitoa wanafika 54. Kwa hiyo, jumla ya wageni wote waliotutembelea hapa Bunge walikuwa 65,146. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tulikuwa na wageni wengi kwa kweli. Wageni wale ambao walikuja kwa ajili ya kufanya maonesho jumla yao ni 609. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunayo siku ya Mabunge Duniani ambayo Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kupitia Azimio lake namba *A/72/278* la tarehe 22 Mei, 2018 lilipitisha siku ya tarehe 30 Juni kuwa ni Siku ya Mabunge Duniani. Tarehe hii ni kumbumbu ya kuanzishwa kwa Umoja wa Mabunge Duniani ambao ulianzishwa mwaka 1889. Siku hii ni muhimu kutambua mchango wa mabunge katika kupaza sauti za wananchi wanaowawakilisha. Pia, ni kutambua mchango wa mabunge katika ushawishi wa uundaji wa sera, utungwaji wa sheria na kusimamia na kuishauri Serikali kwa maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nikiwa kama Mbunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, na kwa vile siku hii imeangukia siku ambayo tutakuwa tumekwisharudi majimboni ninaomba kutumia fursa hii kuwatakia Wabunge wote duniani heri ya Siku ya Mabunge Duniani. Naomba Wabunge wote duniani siku hii itukumbushe wajibu mkubwa tuliokabidhiwa na Katiba za nchi zetu ikiwa ni pamoja na kuwasilisha kikamilifu changamoto za wananchi tunao wawakilisha. Kwani isingekuwa rahisi wananchi wote kuwa Wabunge. *(Makofi)*

Siku hii itukumbushe kuwa pamoja na kuwa na wajibu kwa wananchi pia tuna wajibu kwa vyama vyetu na Taifa kwa ujumla. Mwisho ninawaasa Wabunge wote tuwe chachu ya kuhakikisha kuwa nchi zetu zinakuwa na amani kwa maendeleo na ustawi wa nchi moja moja na dunia nzima kwa ujumla. Ninawatakia Wabunge wote duniani heri ya Siku ya Mabunge Duniani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu salamu hizi inabidi zifike mbali kidogo basi mniruhusu nitoe salamu nyingine kwa lugha ya Kiingereza.

*As one of the members of parliament of the world and as the President of Interparliamentary Union, I would like to take this opportunity to wish all the Members of Parliament of the World, and the entire Interparliamentary Union family a happy International Day of Parliamentarism. Let's all use this day to reflect on our legislative, advisory and oversight role, above all these our primary representative roles. (Makofi)*

*We should all prioritize the needs, challenges, concerns and hopes of the citizens of this world. Let's all work hard to make the world a better secured and peacefully place. Once again, Happy International Day of Parliamentarism, Happy 135th Anniversary of the Interparliamentary Union. Long live IPU.* Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mwisho kabisa nitumie fursa hii kuishukuru sana Bendi yetu ambayo imetuimbia hapa Wimbo wa Taifa pamoja na Wimbo wa Afrika Mashariki, tunawashukuru sana kwa kutongoza vyema. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kabla ya kuahirisha shughuli za Bunge mpaka tarehe ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameitaja niwashukuru wananchi wote wa Tanzania ambao wametoa michango yao mbalimbali ambayo imewafanya Waheshimiwa Wabunge waweze kutoa michango hapa ambayo inatoka kwao kama wawakilishi wao. Ahsanteni sana Watanzania wote kwa kuendelea kufuatilia shughuli za Bunge na pia kuhakikisha Wabunge wenu wanawawakilisha vizuri, wanawakilisha hoja zenu na mawazo yenu pia. *(Makofi)*

Wengine mmepata nafasi ya kuja kutoa kwenye Kamati mbalimbali na wale ambao hamkupata nafasi mliwasiliana na Waheshimiwa Wabunge wenu moja kwa moja; ni jambo jema na ni jambo la heri. Ili nchi yetu iweze kusonga mbele tunahitaji

mawazo ya wananchi, kuyaweka pamoja na kutoa ushauri kwa Serikali.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge ninawatakia kila la heri kila mtu atakokuwa anasafiri kwenda, kila mtu katika uwakilishi wake na kila mtu safari njema Jimboni.

Baada ya kusema hayo naahirisha Shughuli za Bunge mpaka tarehe 27 Agosti, 2024 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 08.05 Mchana Bunge Liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 27 Agosti, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*